**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MKUTANO WA NANE**

---

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 6 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB):**

Hati za Uhamishaji Fedha Na. 1 na Na. 2 za Mwaka 2006/2007 [*Statement of Reallocation Warrants No. 1 and No. 2 of the year 2006/2007]*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa Mwaka 2005/2006 *[The Annual Report and Accounts of Arusha International Conference Centre for the year 2005/2006].*

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. ZAYNAB M. VULU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE):**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NCHI ZA NJE:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha uliopita, Pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

Na. 355

**Ujenzi wa Majengo ya Serikali – Dar es Salaam**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilishaamua kuwa Dodoma ndio Makao Makuu ya Nchi:-

Je, kwa nini Serikali inaendelea kujenga majengo ya Serikali Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Tangu uamuzi wa kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma upitishwe, awamu zote za Serikali kupitia ahadi zilizoko kwenye Ilani za Uchaguzi za Chama cha Mapinduzi zimeweza kutekeleza shughuli nyingi za Maendeleo pamoja na kuboresha huduma mbalimbali hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika Awamu hii ya Nne, Serikali iliyoko madarakani inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi (CCM), kadhalika imeendelea kutekeleza azma hii kama inavyoelekezwa kwenye Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2005, Sura ya Nane, Ibara ya 125.

Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifafanua jitihada za Serikali zinazoendelea kufanywa kutekelezwa suala hili, tarehe 2 Julai, 2007 wakati anahitimisha hoja ya Bajeti kuhusu: “Mapitio ya Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge, kwa mwaka 2007/2008”.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba ninukuu sehemu tu ya ufafanuzi huo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu inayosema, nanukuu:-

“(a) Serikali kwa wakati huu imeelekeza nguvu zake katika kuboresha mazingira mazuri ya Mji wa Dodoma na kuimarisha miundombinu ya barabara zinazounganisha Mkoa wa Dodoma na mikoa mingine ikiwemo barabara ya Iringa-Dodoma-Singida-Babati na Arusha;

(b) Tayari Serikali imeanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 40,000 kitakapokamilika na kitaanza kuchukua wanafunzi 1,000 Septemba mwaka huu. Vile vile Vyuo vingine kama *St. John’s* kitaanza mwaka huu kwa kudahili wanafunzi 700;

(c) Serikali kwa msaada wa Benki ya Dunia na nchi ya China imekamilisha mradi wa maji kwa ajili ya wakazi wa Manispaa Dodoma ambao unazalisha maji maradufu ya mahitaji halisi ya wakazi;

(d) Mfuko wa Bima ya Afya utajenga majengo katika Hospitali ya Mkoa hapa Dodoma yatakayotumika kutoa huduma ya hadhi ya daraja la kwanza kuanzia mwaka huu wa fedha; na

(e) Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* kwa mara ya kwanza imetengewa fedha shilinjgi bilioni 1 kwa mwaka 2007/2008 ili kuboresha mandhari na miundombinu ya Manispaa Dodoma na pia Serikali imepanga kuanza ujenzi wa makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Spika hapa Dodoma”.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika hatua hizi ni kubwa na zikikamilika hususan ujenzi wa miundombinu, kasi ya kuhamia Dodoma itakuwa kubwa zaidi. Majengo ya Serikali ambayo yanajengwa Dar es Salaam hivi sasa kwa kweli ni yale yenye umuhimu unaotakiwa ili kukidhi mahitaji ya utoaji wa huduma zinazotakiwa na walengwa mbalimbali kama inavyofanyika katika miji mingine hapa nchini.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kwamba katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 Serikali imetenga shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kuboresha Mji wetu wa Dodoma yaani *CDA* imetengewa shilingi bilioni moja. Je, Mheshimwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba fedha iliyotengwa shilingi bilioni moja haitoshi kabisa kuboresha miundombinu kama barabara, mifereji ya maji machafu katika Mji wa Dodoma. Je, sasa Serikali itakuwa tayari kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha Mji wetu wa Dodoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Bajeti hii 2007/2008 tumetenga takriban

shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya shughuli za kuendeleza miundombinu za Manispaa ya Dodoma na Mkoa wa Dodoma mzima ili kufungua na kuweza kuendesha kasi ya ukuaji na kuimarisha kuhamia Makao Makuu Dodoma. Lakini nakubaliana kwamba kiasi hiki kwa sasa ni kidogo lakini mwaka jana tukumbuke tu tulitenga shilingi 400,000,000 na sasa tumeongeza imekuwa ni bilioni moja na milioni mia nne (1,400,000,000). Lengo letu ni kuongeza na tunafanya hivi kwa kuwa na fungu na sasa hivi *CDA* itakuwa na kasma yake ambayo itakuwa na fungu linalojitegemea badala ya hivi sasa inatumika kama Idara tu katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Serikali imeshaamua Dodoma kuwa Makao Makuu na kwa kuwa uwanja wa ndege upo katika kuimarisha miundombinu. Je, ni kwa nini Makao Makuu yetu mpaka leo hakuna *schedule of flights* za kuja hapa Dodoma na Shirika la Ndege la Tanzania lipo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, kama mtakumbuka hapo nyuma tulikuwa na Shirika la *Eagle* ambalo lilikuwa linafanya safari zake hapa Dodoma. Lakini kutokana na ukosefu wa abiria wa kutosha katika vipindi vingine nje ya vipindi vya Bunge ilionekana kwamba sio shughuli ambayo itakuwa ni ya kibiashara. Lakini tunawahakikishia Mji unavyokuwa, *University* hii ya kwetu inavyoanza na kukaongezeka kasi katika maeneo mbalimbali kutakuwa na *schedule of flights* ambazo zitaweza kutoa huduma kwa hapa Dodoma.

Na. 356

**Kuundwa Kwa Kamati ya Jinsia Katika Halmashauri**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. DEVOTA M. LIKOKOLA**) aliuliza:-

Kwa kuwa, masuala mtambuka kama UKIMWI na Mazingira yameundiwa Kamati Maalum katika Halmashauri zetu:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuziagiza Halmashauri kuunda Kamati za Jinsia ili kuongeza nguvu ya kuleta usawa wa jinsia nchini?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa, kwenye Wizara na Halmashauri nyingi mambo hayaendi kijinsia na kwamba, hakuna dawati wala afisa anayesimamia usawa wa kijinsia katika utendaji wa shughuli za kila siku katika vyombo hivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia Sera ya Taifa ya Jinsia, Halmashauri zote nchini zimeelekezwa kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa kuandaa Sera za Jinsia za Halmashauri zao. Sera hizi zinatakiwa kuzingatia hali halisi ya mazingira ya Halmashauri husika pamoja na matarajio ya wadau katika Halmashauri hizo. Kabla ya kuandaa sera hizo, Halmashauri zinaelekezwa kuwa na Mpango Mkakati Kuhusu Uzingatiaji wa Jinsia *(Strategic Plan on Gender Mainstreaming)* wakati wa kutekeleza mipango ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haioni sababu ya kuunda Kamati za Jinsia katika Halmashauri kwa sababu mikakati ya jinsia hujadiliwa na Kamati za Kudumu zinazoshughulikia huduma za jamii kabla ya kupitishwa na Baraza la Madiwani.

Hivyo suala la kuunda Kamati ni mchakato ambao umeanza kwa baadhi ya Wizara. Kwa sasa Wizara ambazo zimekwishaanza ni Wizara ya Elimu na Mafunzo, Wizara ya Afya, Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Maliasili. Mchakato huu utaendelea kwa Mikoa na Halmashauri hatua kwa hatua.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) hapo juu, Halmashauri zilikwishaelekezwa kuzingatia jinsia katika kutekeleza shughuli zao za kila kisu. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 ya mwaka 1982 (Mamlaka za Wilaya) kifungu cha 111 (A) (2) (b). Kifungu hiki kinaeleza bayana kwamba katika kutekeleza majukumu yake Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuzingatia ushirikishwaji wa jamii na vikundi vya hiari na suala la jinsia.

Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Halmashauri 122 kati ya 133 tayari zina (*Desk Officer*) Maafisa wanaoshughulikia jinsia katika Halmashauri hizo. Halmashauri 11 zilizobaki ni zile zilizoanzishwa tarehe 1 Julai, 2007 na kwa sasa ziko kwenye mchakato wa kupata. watumishi. Kwa sasa Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu ndiyo inayoratibu na kushughulikia masuala ya jinsia. Ofisi yangu kwa mara nyingine tena inaendelea kuziagiza Halmashauri zote nchini kuzingatia suala la jinsia miongoni mwa masuala mtambuka. Aidha, Ofisi yangu kwa kushirikina na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itahakikisha kwamba kila Halmashauri inakuwa na makakati wa jinsia na masuala ya jinsia yanapewa kipaumbele wakati wa kuandaa mipango na utekelezaji wake.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nitauliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria hiyo iliyosemwa na Mheshimiwa Waziri ni Sheria Na. 7 ya Mwaka 1982 ambayo inazungumzia kifungu cha 111 (A) (2 (b) ambacho kinaunda hizo Kamati za Huduma za Jamii. Kwa kuwa Kamati hizo sasa zimeshazidiwa na majukumu mengi mengi na kushindwa kujikita katika suala zima la jinsia ukizingatia limekuwa likibadilika kuendana na wakati kwa mfano agenda *Fifty Fifty* kwa sasa hivi je Mheshimiwa Waziri haoni sasa iko haja sheria hiyo ikabadilishwa ili Kamati ya Jinsia ikaanzishwa katika Halmashauri.

Mheshismiwa Spika, swali langu la pili ni kwa takribani miaka 20 imeshapita toka Mkutano wa Beijing ufanyike ambao ulizungumzia masuala ya kuwaweka wanawake katika suala la mtazamo la kimaendeleo. Lakini kulikuwa na maazimio 10 ya Mkutano huo wa Beijing. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa hivi ni kipindi muafaka cha kuzingatia maazimio ya Beijing kwa kuyafanyia utekelezaji kwenye Halmashauri kupitia Kamati hiyo ya Jinsia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kama nilivyosema na kama alivyosema yeye ni kweli kifungu hicho kinazungumzia eneo hilo kama lilivyofafanuliwa na sheria.

Lakini nimeeleza hapa wazi wazi kabisa si kwamba Serikali haitaki au haikuunda hizo Kamati. Lakini kwa sababu ni mchakato jambo hili haliwezi kuagizwa kutoka juu kwenda kwenye *Local Authorities*. Kwa hiyo, tunachofanya sasa hivi ni kutoa hamasa kuelimisha ili jambo hili liweze kuibuka kutoka ngazi ya chini na mkifanya hivyo linaweza kuwa na manufaa zaidi kuliko kama itakuwa ni utaratibu wa kutoka juu kwenda chini. Lakini ni dhahiri kabisa kwa maelezo niliyoyatoa tumeshaanza kuzingatia jambo hili na Kamati ni sehemu tu ya kutekeleza maamuzi hayo.

Hili suala la Maazimio ya Beijing mimi nafikiri ni jukumu letu sisi wote kama Serikali na mimi najua kabisa Mheshimiwa anafahamu ni kiasi gani Serikali imejitahidi sana kujaribu kuzingatia Maazimio haya katika kutekeleza majukumu yake kama Serikali. Lakini ninachoweza kumhakikishia kwamba kwa upande wa Serikali za Mitaa sisi ni sehemu ya Serikali Kuu maagizo yote yanayohusiana na utekelezaji wa Maazimio ya Beijing na sisi ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo hayo. Kwa hiyo kama hoja ni Kamati kwa wakati muafaka, Kamati itaundwa na itaongeza chachu zaidi katika kutekeleza Maazimio ya Beijing.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa suala la kijinsia katika Halmashauri kama lilivyosemwa katika suala la msingi lina matatizo katika *level* ya Kata hasa kanuni inayomkataza Diwani wa Viti Maalum kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata wakati Diwani wa Kata anapokuwa hayupo. Kanuni inataka achaguliwe mmojawapo wa Wenyeviti wa Vijiji kuchukua nafasi ile wakati Mwenyekiti huyo wa Kijiji hahudhurii Mkutano wowote wa Halmashauri. Je, Waziri yuko tayari kanuni hiyo ikabadilishwa ili Madiwani wa Viti Maalum wakawa Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo wa Kata wakati Madiwani hawapo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, suala hili lina mambo makubwa mawili. Moja ni kwa sababu wakati Sheria ya Serikali zote mbili zinatungwa 1982 suala la Madiwani hawa wa Viti Maalum halikuwepo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo lilikuja likaibuka baadaye na ndiyo maana haliwi *reflected* vizuri kwenye sheria.

Lakini kwa upande mwingine dhana iliyokuwepo ilikuwa ni kwamba Diwani ambaye ndiye ametokana na kuchaguliwa na wananchi katika Kata katika mazingira ya kawaida liko katika nafasi nzuri zaidi ya kuweza kuwa Mwenyekiti na kuongoza mikutano hiyo kwa sababu yeye ndiye anajua mazingira yale. Lakini naomba nikubaliane naye kabisa kwamba jambo hili ni dhahiri kabisa kwamba limepitwa na wakati nafikiri tutalifanyia kazi tuone namna ya kulirekebisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kadri tunavyoendelea naomba kutoa taarifa tu kwamba mtaona mzee wetu, Mzee John Malecela leo anacheka, anafurahi sana, taarifa nilizozipata ni kwamba Serikali imeanza kutengeneza ile barabara ya Same Mashariki iliyolalamikiwa sana… (*Makofi/Kicheko)*

Na. 357

**Mahabusu Gereza la Kahama**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Gereza la Kahama wapo mahabusu wengi sana kutoka Wilaya ya Bukombe, na kwa kuwa, kuna taarifa zilizotolewa na mahabusu hao nilipotembelea Gereza hilo na Mkuu wa Wilaya tarehe 10 Oktoba, 2006 kuwa, wengi wao wamebambikizwa kesi tofauti na makosa yao na wengine hawajui makosa yaliyowafikisha hapo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kufuatilia suala la mahabusu hao la kubambikiziwa kesi za mauaji au ujambazi wa kutumia silaha ambalo limesababisha mateso katika familia zao ambazo pengine hazina hatia?

(b) Je, Serikali iko tayari kufuatilia kesi hizo ili kujua kama kweli walibambikiziwa na kama sivyo kuwachukulia hatua waliohusika kwa lengo la kukomesha tabia hiyo mbaya?

(c) Je, Serikali inaweza kukubaliana na mimi kuwa, utaratibu unaotumika wa Polisi kukamata, kupeleleza na kuendesha kesi hautendi haki kwa watuhumiwa na badala yake unasababisha ucheleweshaji wa kesi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sheria na Katiba, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Luhahula alitembelea gereza la Kahama tarehe 11 Oktoba 2006 na sio tarehe 10 Oktoba, 2006 kama inavyoonyeshwa katika swali.

Mheshimiwa Spika, siku ambayo Mheshimiwa Mbunge alitembelea gereza hilo kulikuwa na mahabusu kutoka Wilaya ya Bukombe 147, kati yao mahabusu 117 walikuwa wakikabiliwa na kesi za mauaji. Hadi kufikia tarehe 14 Juni, 2007 mahabusu katika gereza la Kahama kutoka Wilaya ya Bukombe walikuwa 89, kati yao mahabusu 85 walikuwa wanakabiliwa na kesi za mauaji. Kutokana na takwimu nilizozianisha idadi ya mahabusu kutoka Wilaya ya Bukombe imepungua kwa asilimia 34 kwa mahabusu wanaokabiliwa na kesi za mauaji na imepungua kwa asilimia 86 kwa wale wanaokabiliwa na kesi za unyang'anyi.

Mheshimiwa Spika, kupungua huku kwa idadi ya mahabusu kunatokana na juhudi za Serikali kuyafuatilia kwa umakini masuala ya watuhumiwa wa makosa mbalimbali. Baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Luhahula lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kosa la jinai na la kinidhamu kwa askari polisi kumbambikizia raia kesi. Kupitia Bunge lako Tukufu natoa wito kwa wananchi wote ambao wana malalamiko ya kubambikiziwa kesi kuwasilisha malalamiko yao kwa Wakuu wa Polisi wa Wilaya au Mikoa, Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Endapo itabainika kuwa askari polisi amembambikizia kesi raia basi Serikali haitosita kuchukua hatua kali za kinidhamu dhidi ya askari huyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa utaratibu wa sasa wa Polisi kukamata, kupeleleza na kuendesha mashtaka, Serikali imeanzisha mchakato wa kuhamishia shughuli za uendeshaji wa mashtaka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP).* Mchakato huu utaanza hivi karibuni katika mikoa sita kabla ya kuendelezwa katika mikoa mingine.*(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa jitihada za Serikali zilizofanywa kwa kupunguza mahabusu wa Bukombe walioko Gereza la Kahama. Lakini pamoja na pongezi hizo naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la mlundikano wa Mahabusu katika gereza la Kahama linasababishwa na ukosefu wa Hakimu wa Wilaya ya Bukombe. Na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Bukombe pamoja na Serikali yake wameshajitolea wakajenga jengo wakalitoa kwa ajili ya Mahakama hiyo. Lakini tangu mwaka jana mwezi Machi tuliahidiwa kupata Hakimu mpaka leo hatujapata. Je, kwa nini Serikali imetudanganya sisi wananchi wa Bukombe kutuletea Hakimu tangu mwaka jana mpaka leo haijafanya hivyo na inakusudia nini kwa wananchi hao?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa majibu mazuri sana kwa swali alilouliza Mheshimiwa Luhahula.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu na wananchi wa Bukombe kwamba Serikali haijadanganya wananchi wa Bukombe kwamba itawapelekea Hakimu. Wakati natoa hoja yangu ya Bajeti ya mwaka huu nilisema kwamba Serikali imeajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kama 47 na kati ya hao tutahakikisha mmoja anapelekwa Bukombe. Kwa hivyo narudia tena Serikali haijadanganya wananchi wa Bukombe wala haijadanganya Watanzania kwa sababu mimi nilitembelea Bukombe ili kuona matatizo ya Bukombe na ni kutokana na kuona kule matatizo tukachukua hatua za kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wengi zaidi. *(Makofi)*

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa matatizo ya Mahabusu wa Bukombe ni sawa na matatizo ya mahabusu wengine popote nchini. Je, Serikali itawasaidiaje hawa wahabusu kuweza kupata *gats* za kufuatilia makesi yao maana wengi bado wataendelea kuwa mahabusu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nilijibu swali hili siku ya Ijumaa na nikaeleza hatua ambazo Serikali imezichukua katika kujaribu kupunguza msongamano wa mahabusu na matatizo yao.

Kimsingi Serikali ilichofanya ni kuajiri kwanza Majaji wengi zaidi na Mahakimu wengi zaidi ili tuweze kusukuma kesi hizi kwa haraka. Vile vile Kamati zile za kusukuma kesi za Wilaya na Mkoa ziko mbioni sasa katika kujaribu kupunguza matatizo na uwingi wa mahabusu katika Magereza yetu. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri na kwa kuwa swali la msingi linauliza Serikali kufuatilia kesi zilizoko ikiwa ni pamoja na taratibu za uchunguzi na kwa kuwa hawa walioko mahabusu hawana nafasi ya kufuatilia na kulalamika kama walibambikiziwa au sivyo.

Je, Serikali sasa iko tayari kuunda utaratibu maalum kufanya uchunguzi wa kina kuona hawa waliobambikiziwa kama ni kweli au sivyo ikizingatiwa kuwa Tume ya Jaji Kisanga iliyotembelea Magereza 45 iliona kwamba katika robo tatu ya Magereza hayo wengi walilalamika kwamba wamebambikiziwa kesi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nimeshatembelea Magereza mengi na ni kweli kila unapofika wengi ama ni mahabusu au wafungwa hulalamika kwamba wao wamebambikiziwa kesi.

Lakini pia unapochunguza sana si wote wanaosema hivyo ni wa kweli. Kwa hiyo, Serikali inaona ugumu kidogo kuunda Tume maalum kwa ajili hiyo tu ila kwa vile utaratibu upo wa Kamati za kusukuma kesi Wilayani na Mikoani ambao hutembelea Magereza haya na wanasikiliza malalamiko ya Mahabusu na Wafungwa mara nyingi wako mara tatu pale pale.

Basi tutazisukuma Kamati hizo zifanye kazi kwa bidii zaidi ili tujaribu kupunguza tatizo hili na hasa hili suala la watu kulalamika kwamba wanabambikiziwa kesi. Lakini

zaidi ya yote Serikali kama nilivyosema imeanzisha utaratibu wa kuondoa uendeshaji wa mashtaka na kutenganisha uendeshaji wa mashtaka na upelelezi. Kwa hiyo, sasa Polisi hawatahusika na uendeshaji wa kesi hata kidogo. Polisi hawatahusika tu na kufanya upelelezi sasa wakishapata ushahidi wanapeleka kwa Mwanasheria wa Serikali ambaye ataangalia kama kuna ushahidi atashitaki, kama hakuna atawarudisha wakafanye tena. Tunadhani hii itasaidia sana kupunguza haya malalamiko ya kubambikiziwa kesi kwa wananchi.

Na. 358

**Hali ya Wakulima Nchini**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inaamini asilimia themanini (80%) ya Watanzania wanategemea kilimo na hivyo kilimo kuwa ni uti wa mgongo wa Taifa letu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kuwasaidia wakulima kupata mikopo mbalimbali katika Taasisi zetu za fedha kwa kutumia mashamba au aridhi huko vijijini kama dhamana za mikopo hiyo?

(b) Je, Serikali haioni sababu ya kulifuta kabisa jembe la mkono na badala yake iwapatie wakulima nguvu kazi ya wanyama na matrekta kwa kutumia pato litokanalo na madini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba tano ya mwaka 1999 inatoa utaratibu wa Halmashauri ya kijiji kupata cheti cha ardhi ya kijiji ili kuweza kushughulikia utoaji na usafiri wa Hati Miliki za kimila kwa watu wenye haki ya kumiliki ardhi katika maeneo ya kijiji.

Umilikaji wa ardhi kimila vijijini unarasimishwa na kuwa mtaji hai ambapo wamiliki wa ardhi wanapewa Hati za Kumiliki Ardhi Kimila na hivyo kuboresha usalama wa miliki.

Aidha wananchi wanaweza kutumia Hati hizo kama dhamana katika vyombo vya fedha, Mahakamani na hata katika kusomesha watoto wao katika vyuo vya elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara za Ardhi na Maendeleo ya Makazi,Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, TAMISEMI na wadau mbalimbali

inatekeleza mpango wa kurasimisha umilikaji wa ardhi kimila. Katika hatua ya mwanzo ya utekelezaji Wilaya tano zimehusika ambazo ni Mbozi, Iringa Vijijini, Handeni, Kilindi na Babati.

Katika Wilaya ya Mbozi zaidi ya Hati miliki 2000 zimekwishatolewa baadhi ya wananchi wameshatumia Hati miliki zao kuomba mikopo kwa ajili ya kuboresha kilimo. Wananchi wawili wamenunua matrekta kwa njia hii kwa ajili ya kupanua mashamba yao. Tunaendelea kuimarisha utaratibu huu ambao unampa uwezo mkulima kukopeshwa na vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kushirkiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI imepima jumla ya Mashamba 3,736 ya wakulima katika maeneo ya skim za umwagiliaji za Lumuma mashamba (509), Kikafu Chini (790, Msange na Mang'onyi (394) na Ruvu (2043) kwa lengo la kuandaa taratibu za umilikishaji mashamba hayo kwa wananchi.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya zana bora za kilimo katika kupunguza matumizi ya Jembe la Mkono, Wizara kupitia Mfuko wa Pembejeo imekiwa ikitoa mikopo ya matrekta yenye masharti nafuu kwa wakulima. Kiwango cha juu cha mikopo hiyo ni shilingi milioni 45. kinachotosho kuwezesha mkulima kununua trekta pamoja na dhana zake. Mikopo hiyo inarejeshwa katika kipindi cha miaka mitano kwa riba ya asilimia nane. Kuanzia mwaka 2003/2004 hadi Desemba 2006, jumla ya matrekta 116 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.3 yameshakopeshwa kwa wakulima katika Mikoa mbalimbali nchini.

Aidha, katika kuhimiza matumizi ya zana zinazokokotwa na wanyamakazi, vituo 64 vya maksai vimekarabatiwa katika Wilaya mbalimbali. Vituo hivyo vimepatiwa zana kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima. Zana hizo ni pamoja na plau, majembe ya palizi, ripa, majembe ya matuta na mashine za kupandia. Ili kuwawezesha wakulima wadogo wa aina hii kupata zana, mikopo imeanza kutolewa na mfuko wa Taifa ya pembejeo kwa ajili ya kununua zana zinazokokotwa na maksai kama vile plau, mikokoteni ripa, majembe ya palizi na majembe ya matuta kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007.

Aidha wakulima wanahimizwa sasa kujiunga katika vyama vya kuweka na kukopa ili waweze kudhaminiwa kwa ajili ya kupata mikopo ya aina hii. Fedha zinazotumika katika kugharamia mipango hiyo ya Serikali inatokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Serikali zikiwemo zile zinazotokana na mapato ya madini.

**MHE. MAGDALENA HAMIS SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya kuridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa kuna urasimu mkubwa sana wa wakulima kupata kuweza kupata mikopo hii ya matrekta kupitia Mfuko wa Pembejeo hapa nchini; na kwa kuwa pia kwa hali halisi ya Wakulima Watanzania ni wachache wenye uwezo wa kupata milioni moja kwa mwaka na hivyo kuweza kumudu kukopa mikopo ya matrekta ambayo ndiyo zana ya haraka ya kuweza kusaidia kilimo.

Je, kwanini Serikali kwa kutambua umuhimu wa kilimo isichukue jukumu la kuagiza matrekta na hivyo kuyasambaza kwenye Mikoa yote ya Tanzania ili wakulima waweze kupata zana hizo kwa urahisi na hivyo kuweza kuwa na kilimo chenye tija na Serikali hapo itahakikisha kwamba imeondoa kabisa suala la njaa hapa Tanzania.

Swali la Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri kuna Mpango wa kutoa hati miliko za kimila kwa kupitia Serikali za Mitaa, lakini kwa kuangalia majibu ya Naibu Waziri utaratibu huu unaenda taratibu sana na hapa mwenye amekiri kwamba ni Wilaya tano tu mpaka sasa hivi ambazo zimeweza kuingia kwenye mpango huu. Na kwa kuzingatia mahitaji yenyewe ya kilimo na wananchi walivyo wengi hapa Tanzania. Serikali itahakikishaje uharakishaji wa utoaji wa hati miliki ili wananchi wengi waweze kufaidika na mpango huu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Spika, kujibu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Ninaomba kusema kuwa hapakua na urasimu wala kasi ya kununua vijiji haijaenda taratibu. Serikali imejitahidi kwa mwaka wa fedha uliopita kupima vijiji 2800 kama tulivyosema katika Hotuba yetu na tumetoa kitabu kwa Wabunge ambacho kinaonyesha vijiji vyote vilivyopimwa na ambavyo tutapima kwa mwaka huu wa fedha.

Ninachoomba ni kwamba Halmshauri zisaidie katika kujenga masjala za ardhi ambazo zitawezesha kuweza kusajili zile hati miliki za kimila; na ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yetu itashilirikana na Wizara ya kilimo kuhakikisha kwamba tunapima vijiji kwa kasi iwezekanavyo pamoja na mashamba lakini tukisaidiwa na Halmashauri za Wilaya. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la kwanza la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya. Kama tunavyofahamu Serikali imekwishajitoa katika shughuli zote hizi zinazohusiana na mambo ya kibiashara. Kwa hivyo, majukumu ya kununua matrekta kwa Serikali na kuanza kuyauza kwa wananchi ukilitizama suala hili ni kwamba tunataka sasa Serikali ianze kufanya biashara hiyo ya kununua na kuuza matrekta.

Sisi tulichokiamua kiserikali ni kwamba baada ya kujitoa kwenye biashara tunataka sekta binafsi ndiyo ihusike katika shughuli hii ya kuagiza na kusambaza zana zote za kilimo pamoja na bidhaa zingine. Lakini Serikali inaendelea kutoa mazingira mazuri kwa ajili ya sekta binafsi kufanya kazi hii; na tukifanya hivi tuna hakika kwamba utaratibu wa kuagiza matrekta na kuyafikisha kwa wakulima utakuwa endelevu kuliko kuwaambia wakulima sasa Serikali inaleta matrekta 2000 halafu yakiharibika hakuna tena utaratibu wa kuweza kuyakarabati. Kwa hiyo, huu ni utaratibu mzuri wa kutumia sekta binafsi kusudi utaratibu huu uweze kuwa endelevu.

Na. 359

**Tatizo la Usafiri Maisome**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Taarifa ya Kahunda Wilayani Sengerema kuna kisiwa cha Maisome chenye wakazi wengi sana; na kwa kuwa wakazi hao ni wavuvi, wakulima na wafanyabiashara wa samaki; na kwa kuwa, kisiwani humo hakuna usafiri wa uhakika wala kivuko.

Je, Serikali itawasaidiaje wakazi wa kisiwa hicho ikiwa ni pamoja na kuwepelekea kivuko?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tarafa ya Ruhinda Wilayani Sengerema kuna kisiwa cha Maisome chenye wakazi wengi wanaojishughulisha na biashara, uvuvi na kilimo. Aidha, ni kweli pia kwamba kisiwa hicho kwa sasa hakina huduma ya kivuko kutokana na kutokuwa na maegesho ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, wakazi wa kisiwa cha Maisome wanaweza kupata usafiri wa Kivuko cha *MV Chato* kinachotoa huduma kwenye kisiwa cha Izumacheli na Nkome Wilayani Geita maeneo yaliyo karibu kabisa na eneo la Kahunda ama Maisome, endapo Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema itatengeneza maegesho (tuta) la kivuko la uhakika katika eneo la Kahunda na hali kadhalika katika Kisiwa cha Maisome.Kwa hiyo, tunamshauri Mheshimiwa Mbunge aishawishi Halmashauri ya Sengerema ili iweze kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ili kivuko cha *MV Chato* kiweze kuanza kutoa huduma kwenye kisiwa hicho.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza, Mheshimiwa Naibu Waziri amenikatisha tamaa kwa majibu yake ambayo amenipa sasa hivi. Tatizo la Maisome ni gati sasa napata wasiwasi wangu kwa Serikali ambayo naitegemea sana kunirudisha tena mimi kwenye Halmashauri yangu ya Sengerema niishawishi na wakati Serikali ni moja. Naomba sasa nielezwe leo wakazi wa Maisome watapewa lini usafiri wa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu hushughulikia magati ambayo yana barabara zinazoshughulikiwa na *TANROADS* kuelekea kwenye gati hizo. Pale ambapo gati inahudumia barabara inayohudumiwa na Halmshauri, Halmashauri ndiyo ina jukumu la kuweka gati au tuta ambalo nimesema. Kama alivyosema Serikali ni

moja na Serikali ya Sengerema ni Serikali hiyo hiyo ninayomwelekeza ajaribu kuishawishi ishughulikie suala hilo.

Na. 360

**Suala la Nyumba kwa Wafanyakazi wa Uhamiaji – Kilambo**

**MHE. MOHAMED S. SINANI** aliuliza:-

Kwa kuwa wafanyakazi wa Uhamiaji waliopo Kituo cha Kilambo katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji wanaishi katika nyumba za wananchi ambazo baadhi yake ni chakavu sana.

Je, ni lini Serikali itawajengea nyumba wafanyakazi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuona kuwa watumishi wake wanaishi katika nyumba zilizo bora wakati wakiwa kazini na hata baada ya kustaafu.

Katika kutambua jukumu hili, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia Wakala wa Majengo imeshaanzisha mpango wa kujenga nyumba katika Mikoa yote na Wilaya zake za Tanzania Bara kwa ajili ya kuwauzia au kuwapangisha watumishi wa umma. Hadi sasa nyumba zipatazo 200 zinaendelea kujengwa katika sehemu mbalimbali ikiwemo Manispaa ya Mtwara ambako nyumba 12 zinajengwa kwa madhumuni ya kuwapatia watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, katika kutambua matatizo yaliyopo kwa watumishi hao wa Kituo cha Kilambo, Wizara yangu imeanza kufanya mawasiliano na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kutambua idadi ya watumishi wa Uhamiaji wa Kituo hicho pamoja na kuainisha mahitaji yao halisi ikiwemo idadi ya nyumba zinazohitajika ili hatua za makusudi ziweze kuchukuliwa na Wizara hizi mbili za kuwajengea nyumba bora watumishi hao kwa siku za usoni.

**MHE. MOHAMED SINANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake lakini pia ningependa kufahamu Serikali inampango gani juu ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika mpaka wa Msumbiji na Tanzania pale panapojengwa daraja la Umoja sehemu ambayo inaitwa Mtambaswala?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa sasa watumishi ambao wanafanya kazi katika

eneo lile la daraja wataishi katika Kambi au majengo ambayo yanajengwa kwa ajili ya wafanyakazi wa muda. Mpaka sasa Serikali haijatenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za kudumu pale. Lakini baada ya shughuli zile kukamilika tunajua kwamba kutakuwa na ulinzi wa daraja lile na kutahitajika nyumba za watumishi kuishi katika eneo lile.

Na. 361

**Gharama za Kuzalisha Umeme**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Shiriki la Umeme Tanzania (*TANESCO*) lilinunua umeme kwa bei maalum kutoka *IPTL*, bei ambayo inafidia gharama za uzalishaji zinazobadilika (*variable costs*) na fidia pamoja na gharama maalum zisizobadilika *(fixed costs)* ambazo hujumuisha gharama za madeni ya *IPTL* kwa mtaji wao wa uwekezaji:-

(a) Je, gharama hizo zinazobadilika na zisizobadilika ni kiasi gani kwa mwezi kwa bei za shilingi ya Tanzania?

(b) Kwa kuwa *TANESCO* ndiyo inayolipia gharama za mafuta *(fuel oil 180 CST)* za kuendesha mitambo ya *IPTL* ya kuzalisha umeme *(variable costs).* Je, *TANESCO* inadhibiti vipi bei za mafuta hayo yanayoingizwa nchini kutoka nje?

(c) Je, mafuta hayo *(fuel oil 180 CST)* yanaagizwa na nani kuja nchini na kwa bei gani kwa tani kwa shehena zilizoingia nchini kati ya Julai 2005 – Machi 2006, na matumizi ya mafuta hayo ni tani ngapi kwa mwezi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Harberth James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mtambo wa kuzalisha umeme wa *IPTL* uliopo Tegeta unazalisha umeme wa Megawati 100 ambao unauzwa kwa *TANESCO*. Bei ya umeme wa *IPTL* inajumuisha gharama zinazobadilika na zisizobadilika. Gharama zinazobadilika ni pamoja na *energy charges bonus payments* na *supplementary* wakati zisizobadilika ni *capacity charges*. Licha ya *capacity charges* kuwekwa katika kundi la gharama zisizobadilika, kutokana na mkataba (*Power Purchasing Agreement*) gharama zake hubadilika tu kutokana na mabadiliko ya thamani ya sarafu *(exchange rate)*

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi Julai, 2005 hadi Machi 2006 Shirika la Tanesco lililipa shilingi 176,906,772.50 kama *bonus payment,* shilingi 56,676,019,363.00 kama *energy charges* na shilingi 34,891,705,173.00 kama *capacity charges*. Jedwali la

mchanganuo wa gharama hizo kwa kila mwezi kwa kipindi hicho linapatikana kama Mheshimiwa Mbunge akilihitaji.

(b) Mheshimiwa Spika, Shirika la *TANESCO* linafuatilia uhalali wa bei ya mafuta yanayotumiwa na *IPTL* kwa mujibu wa makubaliano katika Mkataba (*Power Purchasing Agreement*) kwa kupitia kwa makini ankara (*invoices*) za malipo ambazo zinawasilishwa na *IPTL*.

(c)Mheshimiwa Spika, chini ya mkataba wa *fuel supply*, mafuta (*fuel oil 180 CST)* yanayoendesha mitambo ya *IPTL* yanaagizwa na *IPTL* kwa kutumia Kampuni ya *TOTAL Tanzania Ltd*. Mafuta yaliyoingizwa kila mwezi kati ya Julai 2005 na Machi 2006 ni kati ya tani 6,210.48 na 15,380.72 wakati matumizi yalikuwa kati ya tani 6,383 hadi 14,584. Katika kipindi hicho bei ya mafuta hayo ilikuwa kati ya Dola za Marekani 337.49 na 403.50 kwa tani moja.

**MHE. HERBERTH J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa, lakini naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa uagizaji wa mafuta kutoka soko la dunia unahitaji utaalam maalum,utaalam ambao si fani ya *TANESCO*. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatufahamisha wakati wa majadiliano *TANESCO* iliwakilishwa na wataalam gani? La pili, kwa kuwa sasa bei za umeme zinazidi kuongezeka na gharama hizi zinakuwa mzigo mkubwa sana kwa wananchi. Je, Serikali haioni kuna haja ya kuupitia upya mikataba hii ya *IPTL* kama ambavyo Serikali imefanya katika Mikataba ya Madini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, wakati wa mchakato wa kupata *IPTL* Serikali si lazima iwe na wataalam ndani ya *TANESCO.* Kama mikataba mingine huwa inatumia washauri hata wa nje katika kuwasaidia ku- *negotiate* mikataba mahala ambapo Serikali yenyewe haina ujuzi. Juu ya kupitia mikataba kama wa *IPTL,* Serikali sasa hivi kama tulivyozungumza wakati wa Bajeti tupo katika mchakato wa kuangalia uwezekano wa kununua *IPTL* na kuibadilisha kutoka kutumia mafuta ili itumie gesi.

Na. 362

**Ukosefu wa Umeme – Kondoa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vya Dalai, Pongoi, Waida, Piho, Mapango, Nkulari na Isasa Wilayani Kondoa vipo karibu sana na njia ya umeme kutoka Kondoa Mjini hadi Kibaya Kiteto; na kwa kuwa, vijiji hivyo havina umeme mpaka sasa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia umeme vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa umeme katika vijiji vya Dalai, Pongai, Waida, Piho, Mapango, Nkulari na Isasa upo kwenye mpango wa Serikali wa usambazaji umeme vijijini. Gharama za kupeleka umeme katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge ni shilingi milioni 651.

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa umeme katika vijiji hivyo utafanyika kwa awamu kupitia mradi wa usambazaji umeme vijijini utakaotekelezwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency).* Kati ya kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara mwaka 2007/2008 ni uanzishwaji wa wakala hiyo pamoja na Mfuko wake (*Rural Energy Fund).* Kwa mwaka huu. Wizara imepanga shilingi bilioni 10 kama kianzio.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nafanya masahihisho kidogo tu kijiji alichosema Isasa, hakuna kijiji cha namna hiyo inatakiwa isomeke Isusumya. Baada ya masahihisho haya naomba niulize maswali yangu.

Kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kwamba usambazaji wa umeme vijijini utafanyika kwa awamu. Je, awamu hiyo ya kwanza utaanza lini na katika vijiji vyangu hivi Dalai, Pongai, Waida, Piho, Mapango, Nkulari na Igunga na Isusumya vitakuwepo katika awamu ya kwanza?

La pili, kwa kuwa kijiji cha Piho kipo njiani kabisa na njia ya umeme na inahitaji *transifoma* tu je, Naibu Waziri atanisaidia vipi ili tuweze kupata *transifoma* kwa ajili ya kijiji hicho?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa masahihisho ya kijiji na tunaomba radhi kwa kukosea kutaja jina sahihi kwa kijiji cha Isusumya. Kuhusu ombi la kutaka kujua ni vingapi vitakuwemo katika awamu ya utekelezaji wa usambazaji umeme vijijini, naomba niseme kwamba kwa vile Mheshimiwa Mbunge tumekua naye karibu sana na yeye anafahamu jambo hili na kwa sababu orodha ya miradi itakayotekelezwa kupitia hii awamu ya kwanza ya usambazaji umeme vijini ni kubwa nisingependa kutoa jibu ambalo linaweza kuwa na makosa ya uhalisia wa mambo. Nimkaribishe Mheshimiwa Mbunge Ofisini nimwelezee.

Lakini afahamu kwamba kuna baadhi ya vijiji vyake ambavyo tayari tumeshavifanyia upembuzi yakinifu tutawasiliana na kumhakikisha ni vipi ambavyo vitaanza katika awamu ya kwanza.

Kuhusu suala la kijiji cha Piho suala la *transifoma*, pia nimwombe kwa sababu tutahitaji kuwasiliana pia na Shirika la *TANESCO* pamoja na Wataalam wetu wa Wizara nimkaribishe ofisini tufanye mazungumzo tujue namna ya kulitekeleza. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi linahusu matatizo ya ugavi wa umeme na kwa kuwa ni asilimia kumi tu ya Watanzania wenye umeme na sababu kubwa ya hii ni ukiritimba wa *TANESCO* kwa sababu ni Shirika pekee la ugavi wa umeme hapa nchini. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwa na Mashirika mengine mbadala ya umeme kama ilivyokuwa kwa Mabenki na Makampuni ya simu ili kuleta ushindani na kuwapatia umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nifafanue kidogo ni kwanini pengine huduma za umeme haziendi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anapenda na kudhani kwamba ni kwa sababu ya ukiritimba wa *TANESCO.* Sababu za kutosambazwa umeme kwa kiwango pengine taifa tungetarajia zipo nyingi lakini si kweli kwamba ukiritimba ndiyo umesababisha.

Lakini tumekuwa tukitoa taarifa kupita Bunge hili Tukufu na kuwaarifu wananchi kwamba Wizara ya Nishati na Madini na Serikali kwa ujumla inafanya mapitio ya Sheria ya Umeme nchini lakini pia baada ya kukamilisha zoezi hilo ambalo tumeahidi kwamba itakamilika mwaka huu wa fedha 2007/2008 wigo utakuwa mpana zaidi kuwakaribisha wawekezaji binafsi. Kwa hiyo, tunaamini kwamba kama kulikuwa na mapungufu yaliyotokana na utaratibu wa sasa wa kusambaza umeme kupitia *TANESCO* tunaamini kwamba yatarekebishwa na Sheria hiyo mpya ya Nishati ambayo itazingatia pamoja na mambo mengine kwamba Sekta ya binafsi inashiriki ipasavyo. *(Makofi)*

Na. 362

**Umuhimu wa Kufungua Ofisi za Consulate – Mumbai**

**MHE. IBRAHIM MOHAMMED SANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jiji la Mumbai nchini India ni moja ya sehemu zinazofikiwa na raia wwengi wa Tanzania kwa ajili ya biashara na matibabu; na kwa kuwa raia wan chi yetu wanapopata dharura au matatizo ya kibinadamu hushindwa kupata msaada kutoka Ofisi za Ubalozi wetu zilizoko katika Mji Mkuu wa India (New Delhi) kwa vile uko mbali na Mumbai:

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wea kufungua *Consulate* katika Jiji la Mumbai kama baadhi ya nchi za wenzetu walivyofanya?

(b) Je, ni lini Serikali itatengeneza nakala zenye anuani ya Mabalozi wetu wote walioko nje ya nchi zikagawiwa kwa Watanzania wanaosafiri katika Viwanja vya Ndege na Mipakani japo kwa kulipia gharama kidogo ili ziwasaidie wakipata dharura wanapokuwa nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA – MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Mohammed Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao kuhusu aina za *Consulate*. Zipo aina mbili za *Consulate*:- Aina ya kwanza ni ya *Consulate General* au Ubalozi Mdogo. Ofisi hii huwa inaendeshwa na *Consul General* ambaye anakuwa ni mwajiriwa wa Serikali ya Tanzania huteuliwa na Serikali ya Tanzania kwenda nje kufungua Ubalozi Mdogo. Mfano ni Ubalozi wetu Mdogo uliopo Dubai.

Mheshimiwa Spika, aina ya pili ni ile ya Ubalozi wa Heshima *(Honorary Consulate)*. Hii ni kazi ya kujitolea na anayeongoza Ubalozi wa Heshima anaitwa Balozi wa Heshima *(Honorary Consul)*. Kimsingi huyu siyo raia wa Tanzania, ni raia wa nchi ambayo Serikali yetu ina nia ya kuwa na uwakilishi wa iana hiyo. Mfano mzuri wa *Honorary Consulate* zetu zilizoko Uholanzi, Hong Kong, Australia, Ujerumani na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Mohammed Sanya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Jiji la Mumbai hutembelewa na raia wengi kutoka nchi mbali mbali ikiwemo Tanzania kwa ajili ya shughuli za kibiashara na matibabu. Kwa sababu hiyo, Mumbai ni sehemu muhimu kwa Tanzaznia kuwa na Ubalozi Mdogo *(Consulate General)* na Serikali ingependa sana kufungua Ubalozi huo huko Mumbai na sehemu nyingine nyingi zenye umuhimu kama huo au zaidi.

Lakini, hili limetuwia vigumu kutokana na ufinyu wa Bajeti ambao unatokana na matatizo ya kuichumi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba endapo hali ya kiuchumi itaruhusu, Serikali haitasita kufungua uwakilishi wenye hadhi ya *Consulate General* huko Mumbai.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara inavyo vitabu vinavyoonyesha majina ya Balozi zetu zote, anuani, namba za simu za Balozi na Maafisa wa Ubalozi wote. Vitabu hivi ni kwa matumizi ya Wizara.

Hata hivyo, kwa kuelewa umuhimu wa kutoa taarifa kama hiyo kwa wananchi, Wizara imeamua kuanzisha tovuti ya Wizara yenye taarifa mbali mbali ikiwemo ya Mabalozi wetu wote wanaotuwakilisha nchi za nje. Watanzania wanaweza kupata taarifa hizo kutoka kwenye tovuti hiyo *www.foreign.go.tz* kwa nia ya kupata msaada kutoka kwenye Balozi zetu na kuwasaidia katika shughuli zao mbali mbali wanapokuwa nje ya nchi. Aidha, Wizara yangu imelizingatia wazo la kuweka vitabu hivyo kwenye viwanja vyetu vya Ndege na Vituo vyetu mbali mbali vya mipakani.

**MHE. IBRAHIM MOHAMMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili tu madogo ya nyongeza:-

(a) Ni taratibu gani ambazo mtu anatakiwa afuate ili apate kibali cha kufungua Ubalozi wa Heshima sehemu nyingine yoyote ile?

(b) Ni faida gani anazozipata mtu anayefungua Ubalozi wa aina hiyo katika Miji kama hiyo? Ahsante sana!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA – MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI:** Mheshimiwa Spika, mtu anayetaka kufungua Ofisi ya Ubalozi wa Heshima katika Mji wowote ule, anatuandikia kupitia Ubalozi wetu ulioko katika eneo hilo, akileta na *CV* yake. Wizarani, tunamchekecha kwa kutumia vyombo vyetu mbali mbali na baada ya hapo tukiridhika, tunaipelekea Serikali ambayo mwombaji anataka afungue hiyo *Honorary Consulate*.

Serikali ile ikisharidhika, kwa hiyo, inamwandikia barua ya uteuzi mwombaji mhusika *(Letter of Commission)* Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na baada ya hapo anaanza kazi yake kama Balozi wa Heshima katika Mji unaohusika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu faida, katika jibu langu la msingi nimesema hii ni kazi ya kujitolea. Mwombaji lazima awe na kipato cha uhakika au awe mfanyabishara. Faida anayoweza kupata ni ile heshima kwamba anaiwakilisha nchi katika nchi ile na kule anatambulika kama Balozi wa Heshima na katika shughuli zote za kitaifa anaalikwa. Kwa hiyo, hiyo ndiyo faida kubwa ambayo anaipata, lakini hakuna faida zaidi ya hiyo. *(Makofi)*

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kabla sijauliza swali la nyongeza, ningependa kukushukuru sana kwa taarifa uliyoitoa ya barabara za Same Mashariki. Ningependa kuchukua nafasi hii kupitia kwako kuishukuru Serikali kwa kuitikia wito haraka na kwenda kuondoa kero hizo za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ningependa kuuliza swali la nyongeza: Kwa kuwa wenye shida ni sisi Tanzania ambao tunatafuta biashara na Dunia, kwa nini tungoje mpaka mtu atuandikie barua ili kutafuta Ubalozi wa Heshima? Mimi nilifikiri pengine ni muhimu kwamba sisi wenyewe Watanzania, ili kuongeza biashara na uhusiano na nchi nyingine, sisi tuwatafute hao Mabalozi wa Heshima badala ya kungoja kuandikiwa barua.

Je, Waziri atakubaliana nami kwamba kazi hiyo ya kuwatafuta tuifanye sisi wenyewe badala ya kungoja mtu aombe? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo yameendelea kumiminika kutoka kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara yangu katika

kipindi cha mika miwili iliyopita imeanza mchakato wa kutafuta maeneo ambayo kwa busara ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaona ni mazuri kufungua aina hizo za balozi ambazo tumezisema. Maeneo hayo ni pamoja na maeneo kadhaa ya ya Marekani kama vile Jiji kubwa la Los Angels, kwenye sehemu Fulani pia za nchi za Ulaya na upande wa Malaysia na upande wa Amerika ya Kusini.

Maeneo yote ambayo tunadhani yana vitega uchumi, yana biashara na yana shughuli muhimu ambazo tunadhani zitakuwa na maslahi kwa taifa letu, Serikali inazitafuta sehemu hizo na kuwatafuta watu wanaoweza kufanya shughuli hizo ili kwenda sambamba na jitihada za wenzetu wanaojituma kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, napenda kushukuru kwa swali hilo, Serikali inalishughulikia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtagundua kwamba muda wa maswali umepita. Lakini tumalize hili swali la mwisho kwa sababu kama kawaida tulichelewa kuanza kutokana na kuwasilisha taarifa ambazo zilikuwa zinawekwa mezani. Kwa hiyo, swali la mwisho la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii linaulizwa na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir.

Na. 364

**Ruzuku kwa Hospitali ya Ikonda**

**MHE. AMEIR ALI AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Makete Mkoani Iringa ni Hospitali inayoendeshwa na Kanisa la *Roman Catholic* na ina uwezo wa vitanda mia mbili hamsini (250) vya kulaza wagonjwa; na kwa kuwa Hospitali hiyo hutoa huduma nzuri kwa jamii ikiwa ni pamoja na kutoa huduma bora kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano, watoto yatima na wazee wasiojiweza; na kwa kuwa Serikali huipatia Hospitali hiyo ruzuku ya vitanda arobaini tu (40):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuiongezea ruzuku Hospitali hiyo ili kuiongezea uwezo zaidi wa kuhudumia jamii?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu wa Nane wakati nikijibu swali Na. 145 lililoulizwa na Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, Serikali inashirikiana na Hospitali za Mashirika ya Dini na Mashirika ya Hiari katika kutoa huduma za afya hapa nchini. Serikali inatoa ruzuku ya vitanda na mishahara ya watumishi kiasi cha shilingi bilioni 54.5 kwa mwaka kwa Hospitali 87 za Mashirika ya Dini ikiwemo Hospitali ya Ikonda – Makete pamoja na Hospitali Teule 20.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mwongozo wa utoaji huduma za afya nchini, kitanda kimoja kinatakiwa kuhudumia wagonjwa 1000 kwa mwaka. Wilaya ya Makete ina Hospitali tatu zenye jumla ya vitanda 295 vinavyopatiwa ruzuku na Serikali. Vitanda hivi vina uwezo wa kuhudumia takriban watu 219,335 ambao ni wakazi wa Wilaya hiyo. Hivyo, basi Wilaya ya Makete tayari ina vitanda vya kutosha na inapata mgao wake stahili yake.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si sahihi kwamba Serikali inaipatia Hospitali ya Ikonda ruzuku ya vitanda 40 tu. Naomba kumfahamisha Mheshimia Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inaipatia Hospitali ya Ikonda ruzuku ya Vitanda 140 pamoja na ruzuku ya mishahara ya watumishi. Jumla ya fedha za ruzuku zilizotolewa mwaka wa fedha uliopita 2006/2007 ni shilingi 220,793,272/=.

Hata hivyo, Hospitali kadhaa za Hiari zinazopatiwa ruzuku zimeiandikia Serikali kupitia Wizara yangu kuomba ruzuku hiyo iongezwe. Wataalam wa Wizara ya Afya wanazitembelea Hospitali hizo kwa nia ya kuvifanyia mapitio viwango vilivyopo sasa, na Hospitali ya Ikonda ilitembelewa mwezi uliopita.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na pia niipongeze Serikali kwa hatua kubwa waliyochukua.

Lakini, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Kamati ya Maendeleo ya Jamii tulipotembelea Hospitalini hapo, tulielezwa kuwa ni vitanda 40 tu ndivyo vinavyohudumiwa na Serikali. Je, Mheshimiwa Waziri atatuambia kuanzia lini Serikali imeanza kushughulikia hiyo nyongeza aliyotutajia?

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri humwamini eh? Haya! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa nimpongeze Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, yeye ni Mbunge wa Jimbo la Fuoni kule Zanzibar, lakini ameguswa na Masuala ya Muungano na anaulizia Hopsitali ambayo iko kilomita 75 kutoka Njombe na kilomita 30 kutoka Makete. Nampongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitanda ambavyo tumekuwa tukivitolea ruzuku kwa zaidi ya miaka mitano sasa ni 140.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita sana na maswali yamekwisha. Matangazo, nikianza na wageni: Kwanza ni Watendaji Wakuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi Patrick Mombo, yule pale. Ahsante sana Katibu Mkuu.

Pia yupo Balozi Charles Sanga, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Ahsante sana. Naona sifa za kuwa Mtendaji katika Wizara hii ni kwamba lazima uwe Balozi! Yupo Bwana Elichilia Kaaya, Mkurugenzi wa *AICC*, yule pale. Ahsante sana kwa kuwaleta wageni hapa Tanzania. Riziki Ngwali, mwakilishi wa Mkuu wa Chuo cha Diplomasia, yule pale. Ahsante sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pia anao wageni mahsusi wafuatao ambao ni:- Kwanza, Mkewe, Mama Dorcas Membe, yule pale. Ahsante sana! Mtoto wao Denis Membe, yule pale. Ahsante sana, anajua ku-*bow* kabisa. Amekwishaanza kufundishwa mambo ya Itifaki huyo naona! Kaka yake Mheshimiwa Waziri, Simon Membe, yule kule. *(Makofi)*

Hataki kukaa karibu na shemeji yake, ni vizuri tu natumaini ni mila za kule Mtama, Lindi. Bwana Anthony Membe ambaye ni Mjomba wake Waziri. Ahsante sana na Esther Membe, dada yake Waziri. Huyu ameamua akae karibu na wifi! *(Makofi)*

Pamoja na hao, tunao wageni mashuhuri wafuatao:- Wa kwanza ni rafiki yetu wa mara kwa mara Mheshimiwa Balozi Philip Palm, Balozi wa Uingereza hapa nchini.

Naona ametoka kidogo, ana udhuru. Basi, wasaidizi wake Bwana John Bladshow, Afisa Siasa wa Ubalozi wa Uingereza *(Political Officer)* na Ian Shapiro, *Senior Governance Advicer (DFID). We are happy to welcome you all to the National Assembly here in Dodoma. And we look forward to the Seminar at 01.00 this afternoon. MPs are rearing to go to listen to whatever presentation you have. Welcome! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi ana mgeni wake ambaye ni mwanaye anaitwa Mariam Ramadhan Mahamoud, yule pale. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Godfrey W. Zambi ana wageni kutoka Jimboni kwake ni Wenyeviti wanane (8) wa Kata kutoka kule Mbozi, Makatibu wa Kata wawili (2), Diwani mmoja (1), Katibu Mwenezi na Katibu wa Mbunge. Wageni kutoka Mbozi wale pale! Mmoja naona amevaa rasmi sana! Ahsante sana, tunawashukuru sana kwa safari ndefu kutoka Mbozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, William Ngeleja ana mgeni wake Bwana Juma Nkamia, ambaye ni maarufu, ni Mtangazaji huyu wa Radio Tanzania, Dar es Salaam lakini inaelekea wana uhusiano pia na Mheshimiwa Ngeleja. Hajasimama, yuko wapi sijui! Ah, basi ahsante! *(Makofi)*

Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis ana wageni 22 kutoka Jimbo la Magogoni, Zanzibar, kati yao ni viongozi na wafanya kampeni. Naomba wageni wetu kutoka Zanzibar wasimame. Wale pale mkono wa kulia. Ahsante karibuni sana na uwakilishi huu kutoka Zanzibar, nashukuru sana unazingatia jinsia. *(Makofi)*

Kuna wageni watano wa Mheshimiwa Haroun Suleiman, Waziri wa Elimu wa Zanzibar, lakini hawakutajwa ni nani. Ni wageni tu. Wale wageni wa Mheshimiwa Haroun au ndio wale wale tena! Ahsante. Ahsante sana, samahani sana, mnakaribishwa sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi nao hawakutajwa ni nani - Wageni kutoka Lindi. Wageni wanne wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambao nao hawakutajwa ni nani, lakini watajitambua wenyewe. Kuna wageni wa Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Madiwani sita kutoka Muheza, wamefuatana na viongozi wengine watatu. Madiwani wa Muheza, wale pale! Karibubni sana. Naomba mfahamu kwamba Mheshimiwa Spika anapenda sana machungwa, kwa hiyo safari ijayo ni vizuri kuzingatia hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Wapo wageni saba wa Mheshimiwa Lwanji. Wale pale, karibuni sana. Tunao wanafunzi kama ifuatavyo:- Wanafunzi 30 kutoka Shule ya Msingi Mbwanga, Dodoma, wasimame na walimu. Naona kama hawakupata nafasi. Pia kuna Wanafunzi 33 kutoka *City High Shool* pamoja na walimu. Wale pale! Ahsanteni karibuni sana. Wanafunzi 40 kutoka Jamhuri *Sekondary School,* Dodoma, wale pale, ahsante sana. Wanafunzi 50 kutoka Msalato Sekondari Dodoma. Naona hawapo. Wanafunzi 36 kutoka Jimbo la Kibakwe, Kata ya Chipogolo, wageni wa Mheshimiwa Simbachawene. Karibuni sana, karibuni sana, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mwisho, ingawa siyo mwisho kwa umuhimu, wapo wageni wa Mheshimwa Prof. Philemon Sarungi, Mbunge wa Rorya ambao ni viongozi 8 wa *Club* ya Mpira ya Simba, wakiongozwa na Mheshimiwa Hassan Dalali. Mheshimiwa Dalali uko wapi? Aah, ahsante sana, wale pale.

Pia wapo wachezaji 30 wa *Simba Sports Club* pamoja Kombe la Ligi Kuu waliloshinda. Napenda Ndugu yetu Dalali nikupongeze tu, chini ya uongozi wako, umeendeleza utamaduniuliozoeleka wa kuifunga Yanga. Ahsante sana! *(Makofi/Kicheko)*

Tunao Madiwani kutoka Jimbo la Mtama ambao kwenye Orodha hii walikuwa wamerukwa. Kwa hiyo, nawaomba sana Madiwani wa Jimbo la Mtama pamoja na viongozi wengine wa Lindi wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mtwara,

Mama Akina Msungo. Tafadhali wasimame tuweze kuwatambua! Ni wale pale, samahani sana. Ahsante sana!

Matangazo ya Mikutano, hatuna mikutano ya Kamati ila tu tangazo la Semina: Waheshimiwa Wabunge, leo mchana kama nilivyotangaza siku ya Ijumaa, kutakuwa na Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote inayohusu *General Budget Support* kwa maana ya kuonyesha jinsi gani mataifa tunayoshirikiana nao katika Maendeleo wanavyoleta misaada katika nchi yetu na matazamio yao juu ya nafasi ya Wabunge katika kufuatilia matumizi ya misaada hiyo. Ni jambo zuri, saa 7.30 katika Ukumbi wa Pius Msekwa. *(Makofi)*

Kutakuwa na viburudisho, chakula na kadhalika ili kuendelea na semina hiyo kwa muda wa saa moja/mbili hivi. Mnaombwa sana kuwepo pale saa 7.30. Saa 7.00 tutaanza chakula na viburudisho, halafu baadaye inaendelea semina. Kwa hiyo, ni vizuri tukitoka tu hapa kuweza kuwahi.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba wale wote wenye hisa za *TATEPA*, Chai Bora, wamwone kwa nafasi yao, kuna habari nzuri zinawahusu.

Mheshimiwa Waziri wa Elimu wa Zanzibar (SMZ) anasema hao wageni waliosimama kumbe ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Zanzibar. Nashukuru sana tuliwatambulisha. Ahsante sana.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008
### Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyotolewa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje chini ya uongozi imara wa Mwenyekiti Mheshimiwa Anna M. Abdallah imefanya kazi kubwa ya kustahili pongezi. Kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu kwake Mwenyekiti na kupitia kwake, kwa wajumbe wa Kamati anayoiongoza kwa maoni, ushauri na changamoto ambazo zimetuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa mafanikio. Tutaendelea kuchota hekima na busara za Kamati hii katika kutekeleza kazi za Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara yangu, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi na Mheshimiwa Dr. Cyril August Chami, kwa msaada wao wa karibu katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Mheshimiwa Rais.

Hali kadhalika nitambue mchango wa Katibu Mkuu, Balozi Patrick C. Mombo, Naibu Katibu Mkuu, Balozi Charles A. Sanga, Wakurugenzi, Mabalozi wetu wanaotuwakilisha nje pamoja na wafanyakazi wenzetu wote wa Wizara. Kwa pamoja nasema nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, familia yangu imeendelea kuwa mhimili muhimu katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa yanayonilazimu kuwa mbali nayo kwa kipindi kirefu. Shukrani na tuzo jema anastahili mke wangu, Mama Dorcas Membe na wanangu kwa uvumilivu na upendo wanaonipatia. Kwa wananchi wa Jimbo la Mtama hasa Madiwani ambao leo wamefika 20 wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Jimbo la Mtama, Mheshimiwa Mbonde pamoja na *Dc* wa Wilaya ya Lindi, Bwana Martin Shigela Na Mwenyekiti wa UWT (Wilaya) na UWT (Mkoa) na viongozi wote wako hapa. Napenda niwapongeze na kuwatamkia kwamba nisingefika hapa bila wao kunipa nguvu zao zote. Napenda pia kuwapongeza ndugu na marafiki wote Watanzania kwa ujumla na nawashukuru kwa imani yao na naahidi kutowaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, kwa heshima, taadhima na unyenyekevu mkubwa napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini, kuniona na kuniteua kuiongoza Wizara hii nyeti katika kutafsiri, kutetea na kulinda maslahi ya Taifa letu. Nami naahidi kulitumikia Taifa letu hili kwa kasi, ari, nguvu na unyenyekevu mkubwa katika wadhifa huu mpya na wenye majukumu mazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuungana na Mawaziri wenzangu walionitangulia kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa hotuba yake yenye kutoa taswira nzima ya utendaji Serikalini. Aidha, niwapongeze pia Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa hotuba zao ambazo zimetoa dira na ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitakuwa nimetenda haki nisipowashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri wote walionitangulia kwa kuzungumzia kwa ufasaha maeneo ya ushirikiano wa kimataifa wanayoyashughulikia katika Wizara zao. Utendaji wao unasaidia kwa kiasi kikubwa Wizara yangu kutekeleza dhima yake ya kuratibu utekelezaji wa Sera yetu ya Mambo ya Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa dhati wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Watumishi wote wa Bunge lako tukufu kwa umahiri wenu katika kufanikisha shughuli za Bunge hili. Aidha, nawapongeza kwa ushirikiano wenu mkubwa unaotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kama Wabunge. *(Makofi)*

Napenda niungane na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu aliyekupongeza asubuhi na kuipongeza Timu yetu ya Bunge kwa kazi nzuri waliyoifanya siku ya Jumamosi kwa kuwaondolea mbali Timu ya *NSSF* kwa mabao mawili kwa bila. Sikujua kwamba Mheshimiwa Spika, upo katika Kamati ya Ufundi na ulitabiri vilivyo kwamba wangeshindwa na kwa kweli wameshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwenye husuda nisipotumia fursa hii kuwapongeza Wanawake Watanzania waliotutoa kimasomaso katika medani za Kidiplomasia Ulimwenguni. Nampongeza kwa dhati kabisa dada yangu, Mwanazuoni na Mwanasiasa, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kutoka la Afrika kushika wadhifa huu wa juu wa kimataifa. *(Makofi)*

Vile vile napenda kumpongeza dada langu Balozi Beatha Mulamaula kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Pili wa Wakuu wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika Nairobi Kenya, Desemba 2006, kuwa Katibu Mtendaji wa Kwanza wa Sekretarieti ya Maziwa Makuu. Umma wa Watanzania una imani kubwa nao kwamba watamudu vyema majukumu yao mapya. Wizara yangu inaahidi kutoa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao wateuliwa hawa katika medani za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Mawaziri wenzangu na Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa hivi karibuni kujumuika nasi katika Bunge lako hili Tukufu. Ninawapongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Dr. Christina Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile niungane na Mawaziri walionitangulia kuwapongeza Wabunge walichaguliwa kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki. Kuchaguliwa kwao kunathibitisha imani kubwa ambayo Wabunge na Watanzania kwa ujumla wanayo kwao. Tunawatakiwa kila la heri katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008 pamoja na heri nyingi ulikuwa wa huzuni kwa Bunge lako Tukufu na Taifa kwa ujumla. Kwa ruhusa yako naomba nami niungane na wenzangu kuipa pole familia ya Marehemu Juma Jamaldin Akukweti na watani wangu wa jadi Wayao na wananchi wa Jimbo la Tunduru kwa kupita katika kipindi kigumu cha msiba wa mpendwa wetu.

Aidha, nichukue nafasi hii pia kutoa pole kwa vijana na wanawake wa Tanzania kwa kumpoteza mwanamama chipukizi katika medani ya siasa, Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Kuzima kwa taa hizi ni pigo kubwa kwa CCM na Taifa kwa ujumla. Naomba vilevile kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge ambao wamepatwa na misiba akiwemo Mheshimiwa Waziri Pombe Magufuli ambaye amempoteza baba yake mzazi jana asubuhi na majanga mbalimbali. Tunaomba Mwenyezi Mungu awape ahueni wale wanaougua na kuuguliwa na azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari katika miongoni mwa kazi tulizopanga kufanya katika Mwaka wa Fedha 2006/2007 ni kama zifuatazo:-

(i) Kuwavutia wafanyabiashara, wawekezaji wenye mitaji na teknolojia ya kisasa kuja kuwekeza nchini.

(ii) Kusaidiana na Wizara ya Utalii kuvutia na kutangaza utalii.

(iii) Kudumisha ujirani mwema.

(iv) Kuendeleza jitihada za kutatua migogoro katika nchi za jirani na Afrika kwa ujumla ili kuleta amani, utulivu na usalama.

(v) Kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*), Umoja wa Afrika (*UA*), Jumuiya ya Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (*NAM*) na Umoja wa Mataifa (*UN*).

(vi) Kuitangaza nchi yetu na kutetea heshima yake miongoni mwa mataifa.

(vii) Kuendelea kudai mageuzi katika Umoja wa Mataifa hasa kwa lengo la kupata viti viwili na nguvu za veto kwenye Baraza la Usalama; na

(viii) Kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchi za nje, na kuweka utaratibu utakaowezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/07 hali ya dunia kiusalama, kisiasa, kiuchumi, kimazingira, kisanyansi, kiafya na kiutawala ni ya kuridhisha na kutia moyo. Hata hivyo, Dunia imeendelea kugubikwa na changamoto mbalimbali zinazowanyima Viongozi wetu usingizi. Hali ya kiusalama imeendelea kuwa ya kutia mashaka kutokana na vitendo vingi vya kigaidi hasa mashariki ya kati na kuendelea kwa migogoro na vita vya wenyewe kwa wenyewe *(civil wars).* Dunia imeshuhudia hali ya machafuko, migogoro na vita vya wenyewe kwa wenyewe isiyopungua 36. Migogoro 13 kati ya hiyo ipo Barani Afrika. Idadi hii inaweza kuongezeka iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya kiuchumi nayo siyo nzuri sana kwa nchi zinazoendelea. Ingawa kasi ya ukuaji wa uchumi imekuwa ikiongezeka, tofauti kati ya nchi tajiri na maskini inazidi kuwa kubwa. Tanzania bado ipo kwenye kundi la nchi 31 maskini. Katika kundi hili sisi ni nchi ya 16. Kwa vigezo mbalimbali vilivyotumika katika mpangilio wa maendeleo duniani, nchi yetu imeshika nafasi ya 162 kati 177 za dunia. Si haba tunazidi kupanda! Ni matumaini yangu kuwa kutokana na utajiri wa rasilimali tulizonazo, Tanzania daima itasonga mbele na kwa kasi katika kujiondoa kutoka kwenye lindi la umaskini. Kama wenzetu wa Bara la Asia wameweza kupiga hatua kubwa katika kuvutia mitaji na wawekezaji hakuna sababu ya Afrika au Tanzania kubaki nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, vifo vinavyosababishwa na malaria na ukimwi vimeendelea kuondoa nguvu kazi, hasa ya vijana duniani ikiwemo Tanzania. Aidha, ongezeko la vifo vya watoto wachanga na akina mama wajawazito vimezidi

kuitikisa Afrika na Tanzania, na inatia moyo kujua kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Waziri Mkuu wa *Norway* wamelivalia njuga tatizo la vifo vya watoto na akina mama wajawazito kwa kuanzisha rasmi kampeni maalumu dhidi ya matatizo haya mwezi Machi mwezi huu. Jitihada hizi zinapaswa kuungwa mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kushuhudia jinsi Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEKNOHAMA*) inavyozidi kutamba. Tofauti na huko nyuma ambako uhusiano wa Kimataifa ulikuwa kati ya nchi na nchi, sasa ni uhusiano baina ya Serikali na Serikali, au makampuni kwa makampuni. Dunia ya *TEKNOHAMA* imefanya uhusiano wa kimataifa kuwa baina ya mtu na mtu na hivyo kuifanya dunia ionekane ndogo na tambarare mithili ya meza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Umoja wa Mataifa, vuguvugu la mageuzi ndani ya Umoja wa Mataifa katika kurekebisha muundo wake ili kukidhi mahitaji ya leo ya nchi wanachama lingali linaendelea. Itakumbukwa kuwa kufuatia maombi ya Wakuu wa Nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa katika Mkutano wa Kimataifa wa mwaka 2005, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliunda Kamati ya kuangalia ni kwa kiasi gani Umoja wa Mataifa umefanikiwa kuoanisha masuala ya maendeleo, misaada ya kibinadamu na mazingira. Taarifa hiyo ilipewa jina la *Delivering as One* na ilielezea namna Umoja wa Mataifa unavyoweza kutoa huduma zake kwa ufanisi mkubwa na katika mfumo wa chombo kimoja *(One UN).* Hatua hiyo itaepusha kuugawa Umoja huo katika sehemu nyingi ndogo ndogo na zisizo na ufanisi wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu yake katika ngazi ya taifa. Mpango wa miaka miwili wa majaribio umeanza kutekelezwa katika nchi nane duniani ikiwemo Tanzania. Nchi nyingine ni Albania, Msumbiji, Pakistan, Rwanda, Visiwa vya *Cape Verde, Vietnam* na *Uruguay.*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, dunia ilishuhudia kuundwa kwa Tume ya Kujenga Amani *(Peace Building Commission).* Tume hiyo ambayo ni sehemu ya marekebisho ya mfumo wa Umoja wa Mataifa ina lengo la kusaidia nchi zinazotoka kwenye migogoro kutorejea tena katika hali ya awali kwa kusaidia katika kurekebisha na kujenga mifumo ya kitaasisi na miundombinu kwa ajili ya kurejesha hali ya amani na ustawi. Kwa kazi ya kuanzia, Tume hii imeelekeza nguvu zake katika kusaidia jitihada za kujenga amani nchini Burundi. Tanzania na *Denmark* zikiwa wanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, zilisimamia na kuongoza mchakato wa uanzishwaji wa Tume hiyo. Uanachama wa Tanzania katika Tume hiyo ulikoma Desemba, 2006 baada ya kumaliza uanachama wetu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Mataifa, umeendelea na dhima yake katika kutafuta suluhu ya migogoro katika Mashariki ya Kati. Migogoro kati ya Israel na Palestina, Wasuni na Washia nchini *Iraq* na ule kati ya *Lebanon* na Israel inaendelea kuzizima na kutishia amani katika eneo hilo na uchumi wa dunia kwa jumla. Nchi yetu haiwezi kujiweka kando na migogoro hii ambayo imekuwa ikiathiri nchi maskini kutokana na kuyumba kwa bei ya mafuta. Kwa mantiki hiyo, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu pamoja na nchi nyingine chini ya mwavuli wa Umoja wa Mataifa kutafuta suluhu ya migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, hali katika Nchi za Jumuiya ya Madola zimeendelea kuimarika na kutoa matumaini. Hivi sasa, nchi wanachama wa Jumuiya hiyo wako katika mchakato wa kujiandaa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya hiyo utakaofanyika jijini Kampala, Uganda kuanzia tarehe 23 hadi 25 Novemba, 2007.

Kauli mbiu ya Mkutano huo itakuwa Uwezeshaji wa Jumuiya ya Madola kupata Maendeleo ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii *(Transforming Commonwealth Societies to Achieve Political, Economic and Human Development).* Pamoja na mambo mengine Mkutano huo utafanya uchaguzi wa kujaza nafasi ya Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Jumuiya hiyo. Hadi sasa, nchi za India, Malta na Malaysia zimesimamisha wagombea wa nafasi hiyo. Kwa kuwa Mkutano huo utafanyika ndani ya Afrika ya Mashariki, tutatumia fursa hiyo kutangaza vivutio vya utalii vya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tukio kubwa lililogubika bara la Afrika katika mwaka wa fedha 2006/2007 lilikuwa ni mchakato wa kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Afrika *(African Union Goverment).* Mjadala wa kuanzishwa kwa Serikali hiyo ulifikishwa mbele ya Wakuu wa Nchi katika Mkutano wa Tisa wa Umoja wa Afrika (*UA*) uliofanyika *Accra*, Ghana kuanzia tarehe 1-3 Julai, 2007. Mjadala huo ulihusisha pande mbili, wale waliotaka uanzishwaji wa haraka wa Serikali ya Umoja wa Afrika na wale waliotaka uanzishwaji wa Serikali hiyo uwe wa hatua kwa hatua wakihuisha msimamo wa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mkutano huo uliazimia kuwa uanzishwaji wa Serikali ya Umoja wa Afrika ufanyike hatua kwa hatua. Tanzania inaunga mkono msimamo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Bara la Afrika lina nchi hamsini na tatu ambazo ni wanachama wa Umoja wa Mataifa. Hata hivyo, Afrika ni Bara pekee ambalo halina uwakilishi wa kudumu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Kilio cha Afrika kimeendelea kuwa ni kupatiwa viti viwili vya kudumu na kuongezewa viti viwili vya muda ili kuwa na jumla ya viti vitano vya muda. Kwakuwa wanachama wa kudumu wa Baraza hilo wana kura ya turufu na kama kura hii itaendelea kuwepo, basi Afrika nayo itaendelea kudai haki hiyo. Huu ni msimamo wa Afrika na pia ni msimamo wetu.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Afrika, umendelea kusimamia utatuzi wa migogoro mbalimbali Barani Afrika ikiwemo ile ya *Darfur* na Visiwa vya *Comoro*. Licha ya utekelezaji wa Mkataba wa Amani Kusini mwa Sudan *(Comprehensive Peace Agreement),* hali imeendelea kuwa ya mashaka katika jimbo la *Darfur*. Mgogoro wa *Darfur* umesababisha uhasama baina ya Sudani na majirani zake, Chadi na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Nchi hizo zinashutumiana kusaidia waasi wanaotaka kuangusha Serikali zao. Katika jitihada za kutatua mgogoro wa *Darfur*, Umoja wa Mataifa umeomba Sudani ikubali kupelekwa wanajeshi takribani 20,000 na polisi 3,000 huko *Darfur* ili kuungana na askari 7,000 wa Jeshi la Kulinda Amani la Umoja wa Afrika walioko *Darfur*, chini ya mpango uliokubalika mwezi Novemba , 2006. Serikali ya Sudani imekubaliana na mpango huo.

Aidha, Mheshimiwa Dk. Salim Ahmed Salim, Mwakilishi Maalumu wa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika ameendelea na juhudi za kuvishawishi vikundi ambavyo havijatia saini Mkataba wa amani wa *Darfur* kufanya hivyo. Kwa kutambua umuhimu wa upatikanaji wa amani katika jimbo la *Darfur*, Tanzania itakuwa tayari kupeleka kikosi cha jeshi lake huko *Darfur* chini ya mwavuli wa Umoja wa Mataifa ikiwa itapewa msaada wa hali na mali kukiwezesha kikosi hicho kupata huduma za kutosha kukidhi mahitaji yao ili waweze kutoa ulinzi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kumezuka mgogoro mkubwa wa kikatiba katika Visiwa vya Comoro unaotishia kuvunjika kwa muungano wa Visiwa hivyo unaundwa na visiwa vitatu vya *Mohel, Grand Comore* na *Anjouan*. Umoja wa Visiwa vya Comoro vilipanga kufanya uchaguzi wa ndani wa visiwa hivyo tarehe 10 Juni, 2007. Uchaguzi huo uliweza kufanyika katika visiwa vya *Grand Comore* na *Mohel*. Katika Kisiwa cha *Anjouan* uchaguzi uliahirishwa kutokana na maagizo maalumu ya Rais wa Serikali ya Muungano kwa sababu za kiusalama. Umoja wa Afrika uliafiki pendekezo hilo la kuahirisha uchaguzi huo. Hata hivyo, Bw. Mohammed Bacar, Rais wa *Anjouan* alipinga kuahirishwa kwa uchaguzi huo na kuendesha uchaguzi wake binafsi na baadae kujitangaza kuwa Rais wa Kisiwa cha *Anjouan*. Mahakama ya Katiba ya Visiwa vya *Comoro* ilibatilisha uchaguzi uliofanyika tarehe 10 Juni, 2007. Umoja wa Afrika umelaani hatua ya Bw. Bacar kuendelea na uchaguzi na imesisitiza kutotambua matokeo ya uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania kwa kuombwa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika ilipeleka askari wake huko *Grand Comoro* kusimamia amani wakati wa uchaguzi uliofanyika tarehe 10 Juni, 2007. Nchi za Kanda zinazoshughulikia mgogoro huo, Tanzania ikiwemo, zinaendelea na juhudi za kuhakikisha uchaguzi huo wa *Anjouan* unafanyika katika mazingira ya huru na haki kabla ya mwisho wa mwezi Agosti, 2007. Nchi nyingine zinazohusika na mchakato huo ni Kenya, Afrika Kusini, Msumbiji, *Madagascar,* Visiwa vya Shelisheli na *Mauritius*. Majeshi yetu yatarejea nyumbani mara baada ya uchaguzi. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Askari wetu kwa kazi nzuri na ya heshima wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania kuanzia mwezi Juni, 2006, imekuwa mwanachama wa kikundi cha kimataifa kinachoshughulikia suala la Somalia *(International Contact Group on Somalia)*. Lengo kuu la kikundi hiki ni kufuatilia kwa karibu hali ndani ya Somalia na kuishauri Jumuiya ya Kimataifa namna ya kusaidia nchi hiyo. Aidha, Kikundi hicho kimeitaka Serikali ya Somalia kuanzisha mazungumzo na makundi yote ya ndani ya Somalia kwa madhumuni ya kuleta amani ya kudumu. Tanzania pia inaungana na Umoja wa Afrika kuziomba nchi za kiafrika kutoa michango yao ya kupeleka askari Somalia ili kulinda amani. Tanzania inaziunga mkono Serikali za Ethiopia na Uganda kwa kupeleka majeshi yake Somalia. Serikali ya Tanzania imeahidi kutoa mchango wa mafunzo ya askari 1,000 wa Jeshi la Kitaifa la Somalia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini katika ngazi ya kanda, tumeshuhudia matukio mawili makubwa ambayo yanatoa matumaini ya wakati ujao ambayo ni

kusainiwa kwa Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu; na kujiunga kwa nchi za Burundi na Rwanda katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa kiasi kikubwa, matukio haya yameidhihirishia jumuiya ya kimataifa kuwa mbali na migogoro ya kisiasa, kanda hii imedhamiria kubadilisha taswira yake katika ramani ya dunia na kuifanya migogoro na umasikini kuwa simulizi za kihistroria.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Nchi Kumi na Moja wa Ukanda wa Maziwa Makuu walitia saini Mkataba wa Usalama wa Amani na Maendeleo wa Ukanda huu tarehe 15 Desemba, 2006 huko Nairobi, Kenya. Kwa kutia saini Mkataba huo, Wakuu hao wamedhamiria pamoja na mambo mengine kushirikiana kurejesha hali ya amani na usalama, kukuza ushirikiano wa kiuchumi na hatimaye kuligeuza Eneo la Ukanda wa Maziwa Makuu kuwa Eneo Maalumu la Ustawishaji na Maendeleo *(Special Zone for Reconstruction and Development).*

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika eneo la Maziwa Makuu imeendelea kuwa ya mashaka kutokana na changamoto za ujenzi wa amani ndani ya nchi zilizotoka kwenye migogoro ya wenyewe kwa wenyewe. Wizara yangu imeendelea na juhudi za kuvishawishi vyama vya *CNDD-FDD na Palipehutu-FNL* vya Burundi kufikia makubaliano kwa kushirikiana na mpatanishi, Bw. Charles Mqakula, kutoka Afrika ya Kusini na Mwenyekiti wa Kanda, Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Uganda. Kutokana na ushawishi huo pande hizo mbili ziliweza kufikia makubaliano tarehe 7 Septemba, 2006, Jijini Dar es Salaam. Viongozi wa *Palipehutu-FNL* walirejea Burundi ili kuanza hatua ya utekelezaji wa Mkataba huo mwezi Februari, 2007.

Hata hivyo, kumekuwepo na kulegalega katika utekelezaji wake. Katika Mkutano wa tarehe 17 Juni, 2007 uliofanyika Dar es Salaam, Rais wa Burundi, Mheshimiwa Pierre Nkurunziza na kiongozi wa Palipehutu- *FNL*, Bw. Agathon Rwasa, walikubaliana kuipa Kamati ya Pamoja ya Kusimamia Utekelezaji wa Mkataba wa Amani mamlaka kamili ya kusimamia utekelezaji wake. Aidha, waliahidi kuwa endapo kutatokea tatizo lolote, viongozi hao wawili watakuwa tayari kulipatia ufumbuzi. Serikali imesikitishwa sana na habari za hivi karibuni kuwa viongozi wa Palipehutu-*FNL* wameamua kuondoka Bujumbura na kwenda tena porini tayari kwa vita. Msimamo wetu ni kuona kuwa pande hizo mbili zinamaliza mgogoro huo kwa njia ya amani na inakitaka chama hicho cha upinzani kurejea kwenye meza ya mazungumzo ya amani na kumaliza tofauti zao.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ameeleza kwa undani utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki, na hivyo hakuna sababu ya kurudia. Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Afrika Mashariki ulifanyika Kampala, Uganda tarehe 18 Juni, 2007. Moja ya matukio ya kusisimua katika Mkutano huo ilikuwa ni kusainiwa kwa Mkataba wa Kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa nchi za Burundi na Rwanda kuanzia tarehe 1 Julai, 2007 na hivyo kufanya nchi wanachama wa Jumuiya hiyo kuwa ni tano. Itoshe tu kusema kuwa Tanzania inaamini kuwa kujiunga kwa Burundi na Rwanda katika Jumuiya hii kutasaidia kwa kiasi kikubwa kukuza biashara na hatimaye kusaidia kumaliza migogoro ya ndani ya kisiasa katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika imeendelea kuimarika kufuatia Wakuu wa Nchi kuipa uzito ajenda ya kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi katika Mkutano wao uliofanyika Agosti 2006 jijini Maseru, Lesotho. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi walirudia azma yao ya kuifanya Jumuiya hiyo kuwa Soko Huru ifikapo 2008; kuwa Umoja wa Forodha ifikapo 2015; na kuwa na sarafu moja ifikapo 2018. Aidha, ni katika Mkutano huo Tanzania iliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya hiyo kwa kipindi cha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, ”Jungu kuu halikosi ukoko”. Katika kipindi cha 2006/2007 hali ya siasa na usalama katika nchi kumi na nne wanachama wa *SADC* ilikuwa tulivu kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, palikuwa na changamoto nyingi za kisiasa katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*), Zimbabwe na Falme ya Lesotho. Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya *SADC (SADC Organ)* chini ya uenyekiti wa Tanzania ilihusika sana katika kusaidia kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizi. Changamoto hizo ziliilazimu Tanzania kuitisha Mkutano Maalumu wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika jijini Dar es Salaam, tarehe 29 Machi, 2007 chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *DRC, SADC Organ* ilianza kushughulikia matatizo ya kisiasa kabla ya duru ya pili ya uchaguzi uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2006 kwa njia mbalimbali. Hii ikiwa ni pamoja na kukutana na waliokuwa wagombea wa kiti cha Rais na wadau wote wa siasa nchini humo kwa kuwahimiza kuendesha shughuli za siasa kwa njia za amani na kwa kuheshimu sheria za nchi. Duru ya pili ya uchaguzi ilifanyika kwa uhuru na usalama.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchaguzi pamekuwa na jitihada kubwa katika kurejesha amani na utulivu. Pamoja na mafanikio hayo, matatizo ya kisiasa yanayoendelea kuikabili nchi hii yanatokana na kuendelea kuwepo kwa makundi binafsi yenye silaha hasa katika upande wa Mashariki (Ituri na Kivu) ambayo yanakataa kusalimisha silaha hizo. *SADC* inaunga mkono juhudi za Serikali kuwa na jeshi moja imara la kulinda nchi na inahimiza vikundi vyote vyenye silaha kusalimisha silaha zao na kujiunga na jeshi au kujiunga na maisha ya kiraia kwa utaratibu uliowekwa. Kwa sasa *SADC* inawasiliana na Serikali ya *DRC* kwa lengo la kubaini maeneo ya kipaumbele ambayo *SADC* itaweza kuisaidia *DRC* ili kujiimarisha kisiasa na kiusalama. Tanzania ni sehemu ya msimamo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zimbabwe, matatizo makubwa yametokana na uhasama kati ya Serikali na chama cha upinzani ’*Movement for Democratic Change* ’(*MDC*) yaliyopelekea ghasia za tarehe 11 na 18 Februari, 2007; Uhusiano usio mzuri kati ya Zimbabwe na baadhi ya nchi za magharibi zinazoshinikiza mabadiliko ya kiuongozi na kuiwekea Zimbabwe vikwazo vya kiuchumi. Matokeo yake ni kuendelea kwa mvutano wa kisiasa na kuzorota kwa hali ya uchumi ambapo kumesababisha mfumuko mkubwa wa bei; ukosefu wa bidhaa na ajira na baadhi ya raia kukimbilia nchi jirani. Hatua za hivi karibuni zilizochukuliwa na Serikali ya Zimbabwe za kuamuru wafanyabiashara kupunguza bei kwa asilimia hamsini (50%) bado hazijasaidia na zinazidi kuifanya hali ya uchumi kuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa *SADC* umetolewa na Mkutano Maalumu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC* uliofanyika mjini Dar es Salaam, tarehe 29 Machi, 2007. Mkutano huo ulimteua Mheshimiwa Thabo Mbeki, Rais wa Afrika Kusini kuendelea kuratibu majadiliano kati ya Serikali na Upinzani na kutoa taarifa kwa Troika; ulitamka kwamba jukumu la kuchagua uongozi wa Zimbabwe ni la wananchi wa Zimbabwe pekee; na uliwataka wananchi wa Zimbabwe na wadau wa siasa nchini humo kushughulikia na kumaliza tofauti zao za kisiasa kwa njia ya amani. Mazungumzo hayo bado yanaendelea. Aidha, Tanzania inaendelea na jitihada zake za kuiomba Jumuiya ya Ulaya (*EU*) kuiondolea vikwazo vya kiuchumi Zimbabwe na kutoitenga nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Lesotho ilifanya uchaguzi wake tarehe 17 Februari, 2007. Pamoja na uchaguzi huo kufanyika kwa uhuru na haki, pamekuwepo na mvutano mkubwa wa kisiasa kati ya Serikali na vyama vya upinzani.. Vyama hivyo vimelalamikia jinsi ambavyo viti arobaini vya uwiano vilivyogawanywa. Vyama vya Upinzani vinataka mgawanyo huo upitiwe upya, mtazamo ambao ni tofauti na ule wa Serikali. Serikali inaona viti vimegawanywa kwa misingi ya haki na kufuata sheria, na endapo yapo malalamiko basi yashughulikiwe kwa misingi ya sheria na taratibu za kimahakama. Mvutano huu umekuwa mkubwa na hata kuhatarisha amani.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa *SADC Organ*, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameshughulikia suala hili kwa karibu kwa kuwakutanisha wadau wote wa kisiasa nchini Lesotho ili waweze kumaliza tofauti zao. Wadau wote walikubali Mwenyekiti wa *Organ* ateue mtu mashuhuri kutoka kanda ya *SADC* ili asimamie majadiliano hayo. Mwenyekiti wa *Organ*, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, amemteua Mheshimiwa Ketumile Masire, Rais Mstaafu wa Botswana kusimamia zoezi hili. Mheshimiwa Masire ameanza zoezi hili na anaendelea vizuri na kazi ya usuluhishi. Tunachosisitiza ni kuwa wadau wote wa siasa nchini Lesotho, wamalize tofauti zao za kisiasa kwa njia za majadiliano kwani matokeo ya tofauti hizo ni kuchochea mivutano na vurugu zenye athari kubwa kwa jamii na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nafasi na dhima ya Tanzania Kimataifa na Kikanda, mwezi Desemba, 2006 Tanzania ilimaliza kipindi chake cha miaka miwili kama mjumbe asiye wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Miaka miwili ya uanachama wetu imekuwa ni ya mafanikio makubwa. Katika kipindi hicho nchi yetu imekuwa sehemu ya mafanikio katika kurejesha na kudumisha amani na usalama duniani na hususan katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Katika kipindi cha Urais wetu wa Baraza hilo mwezi Januari 2006, tulifanikiwa kupenyeza na kuipa umuhimu wa kipekee agenda ya Amani na Usalama katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza timu yetu iliyotuwakilisha kikamilifu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Balozi Dr. Augustine Mahiga. Hakika wameijengea heshima kubwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nguvu ndogo kiuchumi, nyota ya Tanzania imeendelea kung’ara na kuheshimika katika Jumuiya ya Kimataifa. Hali hii imetoa msukumo mkubwa katika kuboresha mahusiano mazuri na mataifa mengine, mashirika

ya kimataifa na nchi wahisani. Aidha, Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ameendelea kukubalika na kuheshimiwa kutokana na nguvu kubwa ya ushawishi aliyokuwa nayo si tu hapa nyumbani bali pia katika Jumuiya ya Kimataifa. Mashirika ya Kimataifa, Jumuiya ya Kimataifa na Jumuiya za Kikanda zimekuwa zikimwalika na kumshirikisha katika masuala mbalimbali yahusuyo maendeleo, jamii na utatuzi wa migogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio tuliyoyapata katika maeneo ya utawala bora, demokrasia, na utekelezaji wa malengo ya milenia hususan katika masuala ya elimu, afya na jinsia, yamekuwa chachu katika kupandisha heshima ya nchi yetu. Heshima hii imetoa mwanya kwa Watanzania kuendelea kuaminiwa na kutumainika katika nyanja ya uongozi katika ngazi ya kimataifa. Watanzania wanaoendelea kutulindia heshima hiyo kwa sasa mbali na Dr. Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Getrude Mongella, Balozi Liberata Mulamula, Prof. Anna Tibaijuka, Mheshimiwa Amina Salum Ally aliteuliwa kuwa Mwakilishi wa *AU* mjini *Washington DC* na Mheshimiwa William Shija aliyechaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kulitangaza jina la nchi yetu nje wamo wale ambao hawavumi lakini wamo. Vijana wetu wa timu ya Taifa ya soka ya Tanzania *(Taifa Stars)* wameweza kuipeperusha vyema bendera ya Taifa na kurudisha heshima ya Taifa letu barani Afrika. Tunawaunga mkono mabalozi hawa, pamoja na wengine wanaojitoa muhanga kuiletea sifa nchi yetu. Tunatambua mchango mkubwa wa Mheshimiwa Rais katika kuwatia nguvu wanamichezo wetu na tunawaomba wananchi wote waendelee kuunga mkono juhudi hizo. Tunawatia shime waendelee na ari hiyo na waipeleke bendera ya nchi yetu Ghana mwaka 2008 na mwaka 2010 waipeleke Bendera Afrika Kusini ambako kutafanyika mashindano ya Kombe la Dunia. *Inshallah* Mwenyezi Mungu Mkubwa. Tutafika ! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kutumainiwa si tu na Jumuiya ya Kimataifa bali hata na nchi jirani katika utatuzi wa migogoro na kulinda amani. Kwa sasa Tanzania ina jumla ya wanajeshi mia tatu na nne wanaoshiriki katika majeshi ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika katika nchi za *Comoro*; *Cote d' Ivoire; Ethiopia; Lebanon* na Sudan. Hali kadhalika, tumeendelea kujijengea nguvu ya ushawishi katika mijadala mbalimbali ya kimataifa. Hii imetufanya kuendelea kuwa na mahusiano mazuri na nchi jirani zinazotuzunguka, Jumuiya za Kikanda, Jumuiya ya Kimataifa na Mashirika ya Wahisani. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza askari wetu hao kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hawa nao pia ni mabalozi wa kujivunia.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na heshima kubwa nchi yetu iliyonayo ya kuwepo kwa mazingira ya amani na utulivu inayojivunia, Tanzania imechaguliwa kuwa moja ya nchi kumi na moja Barani Afrika ambazo zimeingizwa katika mpango wa Vijiji vya Milenia, mpango unaoratibiwa na Taasisi ya Dunia *(The Earth Institute)* iliyopo mjini *New York*, Marekani. Taasisi hii ambayo inajikita zaidi katika kuondoa umaskini imevutiwa na ushirikiano wa wananchi wetu wa vijijini kutokana na upeo na ufahamu wao wa MKUKUTA katika kujikomboa kiuchumi. Katika hili, kijiji cha Mbola kilichopo

katika Wilaya ya Uyui mkoani Tabora tayari kinafaidika na mpango huu na tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Wakati huo huo Taasisi hiyo ya Dunia imeridhia ombi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kukifanya kijiji cha Micheweni kilichopo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba kuwa kijiji cha Milenia visiwani Zanzibar. Madhumuni ya uanzishwaji wa vijiji hivi ni kuonyesha jamii na nchi zao kwamba Malengo ya Milenia yanaweza kukamilishwa ikiwa wananchi watashirikishwa ipasavyo katika maamuzi kwa yale yanayowagusa na kupata rasilimali za kuwaendeleza katika kupunguza na hatimaye kuondoa umasikini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, Tanzania imepewa heshima ya kuwa moja ya nchi nane zinazoshiriki katika majarabio ya *One UN* kwa kipindi cha miezi kumi na nane. Majaribio haya yatahusisha Mashirika 17 ya Umoja wa Mataifa katika kutekeleza Programu sita ambazo zimepewa kipaumbele na Serikali yetu kwa kuzingatia Sera za MKUKUTA na MKUZA na pia kuzingatia Mkakati wa Pamoja wa Kusimamia Misaada *(Joint Assistance Strategy for Tanzania- JAST).* Programu ya majaribio inategemewa kuanza kutekelezwa mwezi Septemba, 2007 baada ya kufunguliwa kwa mfuko wa pamoja na kuingizwa kwa fedha za wafadhili katika mfuko huo na itamalizika mwezi Disemba, 2008. Mafanikio ya Programu hii ya majaribio yataleta tija kubwa kwetu kiuchumi lakini pia yatachangia kwa kiasi kikubwa katika harakati za mageuzi ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza, Mheshimiwa *Tony Blair*, aliunda jopo linalofahamika kama (*Investment Climate Facility for Africa-ICF)*, ambapo Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alishiriki kama mjumbe wa jopo hilo. Kama ilivyoahidi, Wizara yangu imefanikiwa kuratibu uanzishwaji wa Makao Makuu ya Taasisi hiyo ya Kimataifa nchini kwetu. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania ilisaini Mkataba wa kuanzisha Makao Makuu ya Taasisi ya Kimataifa ya Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji Afrika (*International Climate Facility-ICF*) tarehe 5 Aprili, 2007. Lengo kuu la taasisi hii ni kuboresha mazingira ya uwekezaji na kusaidia kupunguza umaskini barani Afrika. Kuwepo kwa Makao Makuu ya Taasisi hiyo nchini ni heshima kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imeendelea kutafsiri kwa vitendo Sera ya Mambo ya Nje yenye msisitizo katika Diplomasia ya Uchumi. Mkazo umeendelea kuwekwa katika kutafuta masoko, kuvutia wawekezaji, utalii, kufutiwa madeni pamoja na kushirikisha wadau katika utekelezaji wa sera hiyo. Juhudi hizi zimefanywa kwa pamoja na Balozi zetu, zikiratibiwa na Makao Makuu. Kazi hii imefanywa kuwa rahisi kwetu kufuatia jitihada binafsi za Mheshimiwa Rais ambaye amedhihirisha kuwa kweli ni Mwanadiplomasia namba moja wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ziara za Wakuu wa Nchi ni moja ya nyenzo muhimu katika kufungua fursa mbalimbali za kiuchumi na ushirikiano baina ya nchi marafiki.

Ziara alizofanya Mheshimiwa Rais, katika Bara la Asia, Marekani, Ulaya na Mashariki ya Kati zimeliletea taifa letu manufaa makubwa ya kiuchumi. Napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu mafanikio hayo japo kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Rais katika nchi za Japani, China na Korea Kusini kuanzia tarehe 30 Oktoba hadi 9 Novemba, 2006 iliyofuatiwa na ziara niliyoifanya katika nchi hizo mwezi Mei, 2007, zimewezesha pamoja na mambo mengine kuanza kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Daraja la Malagarasi lenye urefu wa kilomita 2.7 kwa udhamini wa Serikali ya Jamhuri ya Korea.

Kukamilika kwa daraja hilo siyo tu kutapunguza umbali wa kilomita 300 kati ya Kigoma na Tabora, bali pia kutapunguza adha ya usafiri na ukosefu wa huduma mbalimbali unaowakabili kwa muda mrefu wananchi wa mikoa ya Magharibi mwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Japani imeonesha nia yake ya kuanza ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 54 kutoka Masasi hadi Mangaka mkoani Mtwara. Ujenzi huo utaanza mwanzoni mwa 2008.

Aidha, mradi wa upanuzi wa Barabara ya Kilwa yenye urefu wa kilomita 11 kutoka Mivinjeni hadi Mbagala Rangi Tatu nao umeshaanza kutekelezwa kwa msaada wa Serikali ya Japani. Hali kadhalika, Serikali ya Japani ilikubali kusaidia Mradi wa Maji jijini Dar es Salaam na mkoani Pwani ambao unatarajia kutekelezwa mwaka 2008, ikiwa ni pamoja na Mradi wa Maji Zanzibar unaoendelea kutekelezwa tangu mwaka 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akiwa nchini Japani, Mheshimiwa Rais aliishawishi Kampuni kubwa ya Karatasi ijulikanayo kama *OJI Paper* ya nchini Japani kuja kuwekeza nchini Tanzania. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu, kwamba Kampuni hiyo imeshakuja Tanzania na tayari imeanza kufanya majaribio ya kuotesha mikaratusi katika Mikoa ya Mtwara na Lindi kwa ajili ya utengenezaji wa karatasi.

Mradi huu unalenga kupanda msitu wa hekta 20,000 na kuwashawishi wananchi wapande misitu yao hadi ifike hekta 30,000. Kwa pamoja itakuwa ni eneo la hekta 50,000. Aidha, Kampuni ya *OJI Paper* kwa kushirikiana na Kampuni ya Katani ya Tanga zipo katika majadilian juu ya namna ya kutumia zao la mkonge kuzalisha karatasi na umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mahusiano yetu na China yameendelea kuwa mazuri siku hadi siku. Mnamo tarehe 4 hadi 5 Novemba, 2006 Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alishiriki katika *Forum on China-Africa Cooperation (FOCAC)* ambapo makubaliano yaliyofikiwa yalikuwa ni kuongeza idadi ya bidhaa za Afrika ziingiazo kwenye soko la China bila kulipia ushuru kutoka 187 hadi 440, pamoja na kuongeza misaada ya China maradufu kwa nchi za Afrika ifikapo 2009.

Aidha, Mheshimiwa *Huang Hai*, Naibu Waziri wa Biashara wa Serikali ya Jamhuri ya watu wa China, alifanya ziara nchini tarehe 29 Mei, 2007 na kutia saini makubaliano ya kujenga ukumbi wa mikutano wa kimataifa Jijini Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ziara ya Mheshimiwa Rais katika bara la Ulaya ilimfikisha katika nchi mbalimbali zikiwemo Norway na Makao Makuu ya Jumuiya ya Ulaya yaliyoko *Brussels*, Ubelgiji. Akiwa nchini Norway mwezi Machi, 2007, Mheshimiwa Rais alishuhudia kutiwa saini kwa Mkataba wa Ushirikiano kati ya nchi hizi mbili ambapo Norway itaipatia Serikali ya Tanzania zaidi ya dola za kimarekani milioni thelathini (*USD* milioni 30) kwa ajili ya kutekeleza mpango wa kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto katika kipindi cha miaka mitano.

Aidha, kufuatia kurishidhwa na mwenendo wa Tanzania kisera, Umoja wa Ulaya umepitisha asilimia sitini ya misaada yake kwenye bajeti ya Tanzania. Hali kadhalika, Umoja huo utaendelea kuisadia Tanzania katika miradi mbalimbali ya maendeleo na kuahidi kuongeza misaada yake kwa Tanzania kwa karibu *Euro* milioni 100 kwa miaka mitano ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa majumuisho, ziara za Mheshimiwa Rais zilitoa mwanya kwa wafanyabiashara wetu kupata fursa ya kujenga mahusiano na wenzao katika nchi alizotembelea. Mahusiano hayo mapya yana nia ya kufungua milango ya ushirikiano na ubia wa kibiashara katika sekta mbalimbali kama vile madini, utalii, kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Spika, mahusiano baina ya nchi ya *Qatar* yalichukua sura mpya mwaka 2006/2007. Katika juhudi za kuimarisha mahusiano yetu ya kibiashara na kukuza utalii, Shirika la Ndege la *Qatar* lilianzisha safari za ndege kati ya Doha na Dar es Salaam mnamo Februari, 2007. Ni matumaini yetu kwamba kupitia fursa hii uhusiano wa kibiashara, kiuchumi, kiutalii na kijamii baina ya nchi hizi mbili utaimarika zaidi kutokana na kuanzishwa kwa huduma hii.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ubalozi wetu wa *Muscat* nchini *Oman* umefanikisha kupata kibali kwa Shirika la Ndege la *Precision Air* linalomilikiwa na Watanzania kufanya safari zake kati ya miji ya *Muscat* na Dar es Salaam.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mazungumzo yanaendelea kati ya Ubalozi wetu ulioko *Muscat* na Shirika la Ndege la *Oman (Oman Air)* na Shirika la Ndege la Ghuba *(Gulf Air)* kurejesha safari zake za ndege kati ya *Oman* na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, sekta binafsi na wadau wengine imekuwa mstari wa mbele katika kuwavutia watalii na wawekezaji wenye teknolojia ya kisasa katika maeneo mbalimbali.

Aidha, kwa kushirikiana na Balozi zetu, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) na kwa ushirikiano na wadau wengine muhimu tumekuwa tukialika wafanyabiashara kutoka

nchi mbalimbali kuitembelea Tanzania ili waelewe fursa za kuwekeza katika maeneo ya huduma na biashara. Nyenzo zinazotumika kufanikisha jukumu hili ni pamoja na kuandaa semina mbalimbali; kushirikisha wafanyabiashara wa Tanzania katika ziara za nje ya nchi za viongozi wa kitaifa. Aidha, kupitia mikutano mbalimbali ya Kimataifa, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wengine katika kuitangaza nchi yetu *(Conference Diplomacy).*

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine ya Wizara ,Tume za pamoja za Ushirikiano, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mwaka 2006/2007, Tanzania ilisaini mikataba miwili na nchi ya Msumbiji. Mikataba hiyo ni "Mkataba wa Kuondoa Mahitaji ya Viza kati ya Tanzania na Msumbiji na Mkataba wa Ushirikiano Katika Sekta ya Afya.

Katika kipindi hicho hicho Tanzania ilisaini Mkataba wa Kuondoa Viza kwa Pasi za Kidiplomasia na Kiserikali na nchi ya Afrika Kusini. Lengo ni kurahisisha mwingiliano baina ya Serikali hizi mbili na kukuza mahusiano yatakayosababisha kukua kwa biashara. Huu ni mwanzo mzuri. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kufuatilia kwa karibu mikataba hii kwa lengo la kurahisisha mwingiliano kati ya wananchi wa nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imeendelea kutekeleza makubaliano ya Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na *Cuba*. Mnamo Novemba, 2006 Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, alifanya ziara ya kikazi nchini Cuba.

Kutokana na ziara hiyo, Zanzibar imefanikiwa kupata madaktari wanane zaidi, na kufanya idadi ya madaktari wa *Cuba* walioko Zanzibar sasa kuwa ni kumi na wanane na kufanya idadi ya madaktari walio nchini kuwa ni ishirini na wanne. Madaktari wanane walioongezwa Zanzibar watatumika pia kuanzisha Chuo cha Madaktari Zanzibar. Ni matarajio yetu kuwa kuanzishwa kwa Chuo hicho, kutapunguza gharama ya kuwasomesha wanafunzi wa fani ya udaktari nchini *Cuba* na hivyo kuongeza idadi ya madaktari nchini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama mwanachama wa Jumuiya ya Kimataifa ina wajibu wa kusaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo imekubalika kimsingi kwa manufaa ya mataifa yote. Mikataba hiyo ni Baina ya Nchi, Kikanda na Kimataifa.

Wizara imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kusimamia na kuhamasisha mchakato mzima wa utiaji saini na kuridhiwa kwa mikataba ya kimataifa. Miongoni mwa mikataba iliyosainiwa au kuridhiwa katika kipindi cha fedha cha 2006/2007 ni kama ifuatavyo:

Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu; Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo; Marekebisho ya Mkataba wa Afrika Mashariki; Mkataba wa Shirika la Afya Duniani Juu ya Kuzuia Matumizi ya

Tumbaku; na Marekebisho ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya na Nchi za Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara yangu itaendelea na dhima hii kwa kuwa kuweka saini mikataba na kuiridhia. Hili ni jambo linaloashiria nia ya dhati katika kukubaliana na misimamo na maazimio mbalimbali hususan inayogusa maslahi adhimu ya Taifa letu. Aidha, katika mwaka huu, Wizara yangu inatarajia kuwasilisha Bungeni kwa uridhiaji mikataba ifuatayo: Mkataba wa Kimataifa wa Kinga na Upendeleo kwa Maafisa wa Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai; Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu; Mkataba wa Utatuzi wa Migogoro ya Kimataifa kwa Njia ya Amani; na Mkataba wa Upendeleo na Kinga kwa Mahakama ya Kimataifa ya Sheria ya Bahari.

Mchakato wa *APRM*, Tanzania inatekeleza Mpango Mpya wa Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika *(NEPAD)* unaoshughulikia masuala ya uchumi, maendeleo na utawala bora kufuatia kutiwa saini kwa Mkataba wa Makubaliano mwezi Juni 2006 mjini, Dodoma.Mheshimiwa Rais tayari amekwishateua Wajumbe 20 wa Kamati ya Kitaifa itakayoratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Nchi za Kiafrika Kujipima kwa kutumia Vigezo vya Utawala Bora (*APRM*), chini ya Uenyekiti wa Profesa Hasa Mlawa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, Wizara yangu imemwajiri Profesa Daudi Mukangara kuwa Katibu Mtendaji wa Sekretariati hii, na mchakato mzima wa kujitathmini utaanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Uanzishwaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara yangu ililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Makao makuu yake yatakuwa mjini Arusha.

Wizara yangu imeendelea kusimamia mchakato wa kuanzishwa kwa Mahakama hiyo. Mahakama hii ina hatua mbili. Hatua ya muda mfupi ni ya ununuzi na ukodishwaji wa majengo yatakayokuwa Makao Makuu ya Mahakama.

Majengo yamepatikana Tengeru, Jijini Arusha, na shughuli za Mahakama zitaanza mwezi Septemba, 2007. Jumla ya shilingi bilioni 19.3 zinahitajika kwa ajili ya ununuzi wa eneo na majengo yake, kodi za pango kwa ajili ya nyumba za kuishi Rais na Msajili wa Mahakama, pamoja na ununuzi wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, hatua ya muda mrefu itakuwa ni ya kupata kiwanja na kujenga Jengo maalumu litakalofanana na hadhi ya Umoja wa Afrika. Wizara yangu tayari imeanza mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mkutano mkubwa wa Jumuiya ya Wamarekani wenye asili ya Afrika maarufu kama Mkutano wa *Sullivan*. Mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na wajumbe wapatao 3000, Wakuu wa Nchi 30 na watu muhimu *(VIP)* wapatao 40. Mkutano huo utafanyika mjini Arusha, tarehe 2 hadi 6 Juni, 2008.

Mkutano huo utakaoshirikisha wawekezaji, wataalamu na wasomi wa Kimarekani wenye asili ya kiafrika *(African American),* una lengo la kutoa fursa kwa watu wenye asili ya kiafrika waishio nje ya bara hili kusaidia maendeleo ya kiuchumi katika Bara la Afrika kwa njia ya kutafuta rasilimali, kuendeleza sekta binafsi, kujenga miundombinu na kuwekeza teknolojia na mitaji katika Bara hili.

Tangu kuanzishwa kwa mikutano hii Barani Afrika mwaka 1991, zaidi ya dola za kimarekani mia saba hamsini milioni (*USD* 750 milioni) zimeelekezwa katika miradi mbalimbali katika sekta ya afya, elimu, kilimo, madini na biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara yangu itaendelea na maandalizi ya Mkutano huo mkubwa kwa kuwashirikisha wadau wa ndani na wa nje. Haiyumkini, Mkutano huu utachangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha miundombinu, kukuza utalii, kushamirisha shughuli za ugavi na biashara mjini Arusha na Tanzania kwa ujumla. Huu ndio mrabaha wa Diplomasia ya Mikutano.

Kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchi za nje *(Tanzanians in the Diaspora),* kwa kipindi cha miaka mingi sasa, Watanzania wengi wamehamia nchi za nje kwa ajili ya kutafuta maslahi bora. Hali hii inatoa changamoto kubwa kwa Taifa katika kubuni mikakati na sera ya kuwatambua Watanzania wanaoishi nje na hatimaye kuweka utaratibu wa kuchangia maendeleo ya Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeunda kamati inayoshirikisha Wizara yangu na zile za Mambo ya Ndani; Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na; Ofisi ya Rais ili kuangalia mambo yafuatayo:

(i) Kuwashirikisha Watanzania waliopo nje ya nchi katika kujenga uchumi wa nchi yetu katika mfumo rasmi yaani *(National Institutional Framework for Engaging Diaspora for Economic Development).*

(ii) Kufanya mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu *(Central Bank Act)* na Sheria ya Kubadili Fedha *(Exchange Rate Act)* ili kuruhusu Watanzania hao kufungua akaunti maalumu na kuweza kutuma fedha nyumbani kwa kutumia mfumo rasmi. Jambo hili litasaidia pia kupata takwimu za mchango wao katika pato la Taifa.

(iii) Kupitia upya Sheria ya Uraia ya Tanzania ili kuona uwezekano wa kuruhusu uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imejizatiti kuendeleza jukumu la kuhamasisha Watanzania wanaoishi nchi za nje kwenda katika Ofisi zetu za Ubalozi kujiandikisha ili kujua idadi ya Watanzania wanaoishi katika nchi tunazowakilishwa. Aidha, Wizara pia inaendelea kuhamasisha Watanzania hao kuunda Jumuiya zitakazotambulika ili kurahisisha mawasiliano na Serikali yao ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, kutasaidia kuwafanya Watanzania hao kuwa huru kuja kuwekeza nchini na kuwashawishi wawekezaji kutoka nchi hizo kuwekeza Tanzania. Katika kufanikisha azma iliyokusudiwa, viongozi wakuu wa nchi akiwamo Mheshimiwa Rais, wakati wa ziara zao nje ya nchi walikutana na Watanzania na wale wenye asili ya kitanzania waishio nchi hizo kwa nia ya kuwahamasisha juu ya umuhimu wa kuwa na Jumuiya hizo katika kuchangia maendeleo ya Taifa letu.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008 tutaelekeza nguvu katika kuimarisha mshikamano kupitia Balozi zetu kwa kuendelea kuzungumza na Watanzania hao kwa nia ya kuimarisha mshikamano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu imeendelea na jukumu lake la kuratibu na kutoa huduma zake za kiitifaki na kikonseli. Huduma hizi zinahusisha uratibu wa safari za viongozi wa kitaifa kwenda nje kwa ziara za kikazi, kirafiki na kuwapokea na kuwakirimu viongozi kutoka nje wanaoitembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia imeendelea kutoa huduma za kiitifaki kwa mabalozi wanaowasilisha Hati zao za Utambulisho (*Credentials*), huduma ambayo hutolewa kwa mabalozi wanaowakilisha nchi zao nchini mwetu. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Tanzania imepokea mabalozi wapya wanane kutoka nchi za Italia, *Norway*, Ufaransa, *Denmark,* Burundi, Kenya, Korea ya Kusini na Japani. Aidha, Wizara imeendelea kuandaa Hati za Utambulisho za mabalozi wetu wanaokwenda kuiwakilisha Tanzania nje ya nchi na kutumia njia za kidiplomasia kurekebisha kasoro zinazosababisha kuchelewa kwa uwasilishaji wa hati za utambulisho za mabalozi wetu wanaowakilisha Tanzania kwenye nchi zaidi ya moja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara iliratibu ziara thelathini na mbili za viongozi wa juu wa kitaifa nje ya nchi. Aidha, Wizara iliratibu mapokezi ya Viongozi Wakuu wa Nchi na Serikali kumi na watatu ambao waliitembelea Tanzania kwa ziara za kitaifa na kikazi. Viongozi hao ni kutoka nchi za Afrika ya Kusini, Burundi, China, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Lesotho, Malawi, Msumbiji, Namibia, *Swaziland, Trinidad na Tobago,* Umoja wa Falme za Kiarabu, Zambia na Zimbabwe. Ziara zote hizi zimekuwa za mafanikio makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za kikonseli, Wizara imeendelea kusimamia huduma hizo kwa jamii za kibalozi nchini ili kuhakikisha kwamba kinga na upendeleo maalumu unaombatana na stahili ya hadhi ya jamii ya kibalozi zinatumiwa kwa kufuata sheria, mikataba ya kimataifa na taratibu za nchi yetu. Hili linakwenda sanjari na jitihada za kidiplomasia kutatua tatizo la upatikanaji wa hati za ukazi yaani viza kwa wananchi wetu kutoka baadhi ya Balozi za nchi za Magharibi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia katika mwaka wa fedha 2006/2007 imetoa mwongozo kwa watu wote wanaostahili kutumia ukumbi wa wageni mashuhuri *(VIP)* katika viwanja vyetu vya ndege.

Wizara imelazimika kuandaa utaratibu wa kutoa vibali kwa matumizi ya ukumbi huo ili kuhakikisha usalama wa viongozi, faragha, na kuzuia matumizi mabaya ya ukumbi huo. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Wizara yangu inafanya juhudi za kukusanya nguvu za wadau kwa ajili ya kujenga ukumbi mpya wa viongozi na wageni mashuhuri.

Mheshimiwa Spika, Uimarishaji wa Utendaji Katika Wizara, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu imeendeleza mchakato wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara wa kada zote. Wizara kwa kushirikiana na Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliandaa mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathimini ya Utendaji Kazi (MWAMTUKA).

Lengo kuu la mafunzo haya ni kuimarisha uelewa na umuhimu wa mfumo huu katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Wizara. Jumla ya watumishi mia moja hamsini na wanne (154) wamekwishapatiwa mafunzo hayo kati ya watumishi mia tatu themanini na wanane (388). Zoezi hili linaendelea na litawafikia watumishi wote.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliitikia wito wa Bunge lako Tukufu juu ya kuboresha usimamizi wa mali na fedha za umma katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza juhudi hizi, Wizara yangu iliandaa semina ya mafunzo elekezi kwa Wakuu wa Utawala na Fedha katika Balozi zetu zote. Jumla ya Wakuu wa Utawala na Waambata Fedha sitini na wanne kutoka katika Balozi zetu thelathini walishiriki katika mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imedhamiria kuhakikisha kuwa kuanzia sasa inapata hati safi ya matumizi ya fedha kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Tunashirikiana kwa karibu na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mkaguzi Mkuu kuweka utaratibu mpya wa kila Ubalozi kupatiwa hati yake badala ya Wizara kubebeshwa mzigo wa hati hasa chafu kwa niaba yao. Kila Ubalozi utabeba msalaba wake.

Sambamba na hatua hiyo, tuko katika mchakato wa kuhakiki sifa za wahasibu wetu walioko ubalozini na tayari tuko katika zoezi la kuwarudisha nyumbani wahasibu ishirini, ikiwa ni pamoja na kuwaandaa wahasibu wapya wenye sifa kwenda kujaza nafasi zitakazoachwa wazi. Hadi sasa tayari Wizara yangu imerudisha nyumbani na kuwapeleka wahasibu wapya wanane wenye sifa stahili katika Balozi zetu ili kuimarisha utendaji wao wa kazi na usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia inaandaa Mkutano wa Mabalozi wetu na Wadau wenye lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera yetu ya Mambo ya Nje utakaofanyika hapa nchini mwezi Novemba, 2007. Tumeazimia kutumia fursa ya Mkutano huo kuwekana sawa na kusisitiza juu ya umuhimu wa uwajibikaji wa kila Balozi katika usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoalihidi Bunge lako Tukufu mwaka jana, Wizara yangu imefungua tovuti yake mwezi Mei, 2007 na inapatikatikana kwa anwani *www.mfaic.go.tz.* Kwa sasa tovuti hiyo ina uwezo wa kuwapa wananchi na wadau wetu taarifa zote muhimu kuhusu muundo wa Wizara na Idara zake, Balozi au uwakilishi hapa Tanzania, mashirika ya kimataifa yaliyopo nchini na taarifa za Balozi zetu zilizopo nje ya nchi. Wizara inakaribisha maoni ya Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine katika kuboresha tovuti hii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuanzishwa kwa tovuti hiyo, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara imeazimia kuanzisha Jarida la Mambo ya Nje litakalojulikana kwa jina la *Foreign Affairs Bulletin* litakalochapishwa mara nne kwa mwaka. Lengo la jarida hili ni kuboresha upashanaji habari kati ya Wizara, Balozi zetu na wadau wetu wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Wizara, Utumishi, Maslahi ya Watumishi na Vitendea Kazi kama ilivyoelezwa kwenye hotuba ya bajeti kwa mwaka 2006/2007, Muundo wa Wizara yangu umekuwa ukirekebishwa kila inapobidi ili kukidhi haja ya kuwa na utendaji mzuri na wenye tija, pamoja na kwenda na mabadiliko yanayotokea kila siku duniani. Wizara ipo katika mchakato wa kuwateua Wakurugenzi Wasaidizi kwa kila Idara ambapo zoezi hili litafanyika kwa awamu katika mwaka wa fedha 2007/2008 na 2008/2009, kutegemeana na hali ya upatikanaji wa fedha za mishahara.

Mheshimiwa Spika, licha ya nafasi hizo za uteuzi, Wizara bado ina upungufu wa watumishi ambapo katika ikama ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara imeomba nafasi sitini za ajira mpya kwa kada mbalimbali, hii ikiwa ni pamoja na kuziba mapengo ya wastaafu waliohamishwa na waliofariki dunia.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa diplomasia yetu ya uchumi, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tumefungua Balozi mpya nchini Malaysia na Brazili kama ilivyoridhiwa na Bunge lako katika mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri ufunguzi wa Balozi hizi utaleta manufaa kwa nchi yetu ikizingatiwa kuwa maeneo ya Kusini Mashariki mwa Asia na Amerika ya Kusini ni vitovu vya ukuaji wa uchumi na uwekezaji kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imeweza kununua Jengo la Ubalozi "*Chancery*" nchini *Sweden - Stockholm*, kwa gharama ya Korona za kiswidi milioni kumi na laki tano (*SEK*, 10,500,000.00) ambayo ni sawa na dola za kimarekani takribani milioni moja na laki tatu (*USD* 1,300,000.00).

Vile vile Wizara yangu imeweza kukamilisha ujenzi wa jengo lake lenyewe katika Ubalozi wetu *New Delhi*, India. Jengo hili lina thamani ya Dola za kimarekani milioni bili na kaki nane ( *USD* 2.8*Mil*.). Ujenzi huo ulihusisha nyumba za kuishi familia tatu, ambazo ni "*Apartments*".

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo ya Serikali ya kumiliki jengo la ubalozi huko *New Delhi-India*, Serikali imeweza kuokoa takriban dola za kimarekani Laki Mbili (*USD* 200,000) kwa mwaka ambazo zingelipwa kama kodi ya pango.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inazo taasisi mbili zilizo chini yake. Moja ya Taasisi hizo ni Chuo Cha Diplomasia *(Centre for Foreign Relations).* Chuo hiki kimeendelea kutoa mafunzo katika fani za Itifaki, Uhusiano wa Kimataifa, Diplomasia, pamoja na aina mbalimbali za mafunzo elekezi. Idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi mia mbili na arobaini na mmoja mwaka 2005/2006 hadi kufikia wanafunzi mia tatu sabini na watano katika mwaka 2006/2007. Hili ni ongezeko la asilimia hamsini na tano nukta sita (55.6%).

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kujizatiti kutekeleza matakwa ya Tume ya Vyuo Vikuu *(Tanzania Commission for Universities).* Aidha, Wizara yangu imeanza mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Msumbiji kuhusu mkataba unaoanzisha Chuo hicho. Mazungumzo haya ni muhimu kwa ajili ya marekebisho ya Mkataba wenyewe, utungaji wa sheria mpya na hatimaye mchakato mzima wa kubadilisha hadhi ya Chuo na ithibati ya tunzo zake. Mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Msumbiji yanafanyika sambamba na shughuli za Kamati Ongozi inayoangalia mchakato mzima wa mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, taasisi nyingine iliyo chini ya Wizara yangu ni Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (*AICC*) ambacho kinaendelea kufanya kazi vyema na kutoa mchango wake katika pato la Taifa. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Kituo kiliweza kuwa mwenyeji wa mikutano 120, asilimia arobaini ikiwa ni mikutano ya kimataifa na asilimia sitini ni ya kitaifa. Mikutano hii ilikutanisha wajumbe wapatao elfu kumi na wanne mjini Arusha.Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Kituo kimeweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni nne, milioni mia tisa hamsini na sita, mia tatu na nne elfu (4,956,304,000/=) kutokana na mikutano pamoja na vyanzo vingine vya mapato na kupata ziada ghafi ya shilingi milioni mia sita arobaini na nane mia saba kumi na tano elfu (648,715,000/=).

Mheshimiwa Spika, malengo na nia ya Wizara ni kuona Kituo hiki kinakuwa Kituo cha Kisasa katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Hii inatulazimu kuongeza kasi katika kuvutia mikutano mingi ya kimataifa kufanyika katika Kituo hiki. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Kituo hiki kinatarajiwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa wa Waongoza Ndege (*International Association of Air Traffic Controllers*) utakaofanyika mwezi Mei, 2008. Mkutano huo utakaohudhuriwa na washiriki kutoka nje wapatao mia saba hamsini utakuwa unafanyika kwa mara ya pili barani Afrika baada ya miaka thelathini. Mkutano wa kwanza kufanyika barani Afrika ulifanyika Jijini Nairobi, Kenya mwaka 1978.

Mwaka 2007/2008, kituo kinatarajia kuingiza mapato ya shilingi bilioni tano thelathini na nne milioni na sabini na mbili elfu mia tisa sabini na tano (5,034,072,975/=) ambalo ni ongezeko la asilimia kumi na nne kutoka katika mikutano na vyanzo vyake

mbalimbali vya mapato. Malengo na matarajio ya Kituo ni kuongeza idadi ya mikutano kwa kujitangaza na kutoa huduma bora zaidi. Azma hii inalenga kuifanikisha kauli mbiu ya kituo ambayo ni: "Tunaileta Dunia Tanzania*"(We Bring the World to Tanzania).*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Kituo kinalifanyia kazi wazo la ujenzi wa kituo kipya cha kisasa cha mikutano kitakachoweza kukidhi mahitaji ya nchi kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Wizara yangu ilipangiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni hamsini na mbili mia saba thelathini na sita milioni mia mbili tisini na nane elfu (52,736,298,000/=). Kati ya fedha hizo shilingi bilioni hamsini mia tatu na kumi na saba milioni mia nane na sabini elfu na mia tatu (50,317,870,300/=) ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni mbili na mia nne na kumi na nane milioni, mia nne na ishirini na saba elfu na mia saba (2,418,427,700/=) ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizi Wizara ilitegemea kukusanya kiasi cha shilingi bilioni nane na milioni mia nne (8,400,000,000/=) kupitia Balozi zake kutokana na maduhuli yatokanayo na Viza. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2007, kiasi cha shilingi bilioni nane mia tisa themanini na nne milioni mia nne themanini na saba elfu mia tatu tisini na nane (8,984,487,398/-) kilikuwa kimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, hili ni ongezeko la shilingi mia tano themanini na nne milioni mia nne themanini na saba elfu mia tatu tisini na nane (584,487,398/-) sawa na ongezeko la asilimia saba, zaidi ya makadirio ya makusanyo. Ongezeko hili limesababishwa na jitihada za Balozi zetu katika kuitangaza nchi yetu na fursa mbalimbali za uwekezaji, utalii na biashara zilizopo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni sitini na tatu milioni mia moja tisini na nane mia sita na tisa elfu mia nane kumi na tano (63,198,608,815.00) kutoka Hazina kama sehemu ya mgao wake wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kiasi hiki cha fedha ni zaidi ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa kutumika kwa jumla ya bilioni kumi milioni mia nne sitini na mbili mia tatu kumi na moja elfu mia nane kumi na tano (10,462,311,815.00) likiwa ni ongezeko la asilimia 19 kutoka makadirio ya awali. Hata hivyo, Wizara pamoja na balozi hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2007 ilikwisha tumia kiasi cha shilingi bilioni sabini na mbili milioni mia tatu hamsini na tatu mia nane hamsini na saba elfu mia mbili themanini na moja (72,353,857,231.00).

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili la bajeti limechangiwa na mahitaji muhimu yaliyojitokeza kama maandalizi ya Mkutano wa *Sullivan*, mchakato wa *APRM (African Peer Review Mechanism)* maandalizi ya awali ya kuwa mwenyeji wa Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu wa Afrika, shughuli za *SADC Organ,* michango yetu katika Sekretarieti ya Ukanda wa Maziwa Makuu na nyongeza za gharama katika safari za

viongozi wakuu wa kitaifa. Baadhi ya maeneo haya hayakuwa yametengewa fedha chini ya Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Wizara Katika Mwaka wa Fedha Wa 007/2008 pamoja na kazi na malengo ambayo nimeyataja katika vifungu mbalimbali vya hotuba yangu, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2007/2008, itatekeleza, pamoja na kazi nyingine, malengo makuu muhimu kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 kama ifuatavyo:

Kuendelea kuiletea nchi yetu maslahi ya kiuchumi kwa kuwavutia wawekezaji wenye mitaji, teknolojia ya kisasa, kukuza biashara na watalii; kuendeleza Sera ya Ujirani mwema; kuendelea kushiriki katika kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*), Umoja wa Afrika (*UA*), Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (*NAM*) na Umoja wa Mataifa (*UN*).

Malengo mengine ni kuendelea kuitangaza nchi yetu na kutetea heshima yake miongoni mwa Mataifa; kuendelea kudai mageuzi katika Umoja wa Mataifa kwa lengo la kuongeza sauti za nchi zinazoendelea; kujikita katika Diplomasia ya Mikutano; na kutambua Jumuiya ya Watu Wenye Asili ya Kitanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2007/2008, ili kuweza kutekeleza kazi zilizotajwa hapo juu, Wizara yangu imepangiwa kiasi cha shilingi bilioni hamsini na tisa arobaini na moja milioni mia moja tisini na mbili elfu (59,041,192,000/=) katika mwaka wa fedha 2007/2008.

Kati ya fedha hizo bilioni arobaini na saba mia tano na kumi milioni na sabini na mbili elfu (47,510,072,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha bilioni mbili mia tano thelathini na moja milioni mia moja ishirini elfu (2,531,120,000/-) kwa ajili ya mishahara.

Aidha, kiasi cha bilioni tano (5,000,000,000/-) ni kwa ajili ya Mkutano wa *Sullivan*, bilioni mbili (2,000,000,000/-) kwa ajili ya mchakato wa *APRM* na bilioni mbili (2,000,000,000/-) zingine ni kwa ajili ya uanzishaji wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara yangu ina lengo la kukusanya kiasi cha shilingi bilioni tisa, mia moja milioni na elfu hamsini (9,100,050,000/-) kama maduhuli ya Serikali. Kwa maana ya utekelezaji wa bajeti, kiasi hiki tayari kimehesabiwa kama sehemu ya matumizi ya kawaida ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH: - (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni na. 88(11) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema mimi mwenyewe, wewe Mheshimiwa Spika, na wabunge wenzangu wote wa Bunge hili Tukufu.

Pia naomba nitumie fursa hii kuwapongeza wapiga kura wangu wa Jimbo la Iramba Magharibi, kwa ushirikiano wanaonipa na kuniwezesha kufanya kazi yangu vizuri ya kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Aidha, naishukuru familia yangu, mke wangu Hajra, wanangu Sitti, Latifa, Faisal na Fahad kwa kunipa moyo muda wote katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, kwa hekima na uzoefu wao kuhusiana na masuala mbali mbali katika nyanja za kimataifa ambao umesaidia kujadili na kuchambua mapendekezo ya bajeti na masuala mengine yanayohusu Wizara hii ikiwa ni pamoja na bajeti ya mambo ya nje na ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba niwatambue wajumbe wa Kamati yangu kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Annah M. Abdallah, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mohamed G. Dewji , Mheshimiwa Dk. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Yono S.Kevela.

Wengine ni Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Muhonga S.Ruhwanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Dk James M. Wanyancha, na Mheshimiwa Zainab M.Vulu, *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe, na Naibu Mawaziri , Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi na Mheshimiwa Cyril August Chami. Aidha, nawapongeza, Katibu Mkuu wa Wizara, Balozi Patrick Mombo na wataalamu wengine kwa kuwasilisha mbele ya Kamati mapendekezo ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuzingatia kiasi cha fedha iliyokabidhiwa kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007. Aidha, Kamati imeridhishwa na namna Wizara ilivyotekeleza ushauri wa Kamati wakati wa kupitia mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyoelezwa na Mheshimiwa Waziri kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 Wizara inaomba jumla ya Sh. 59,041,192,000/= kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mishahara sh. 2,531,120,000 na matumizi ya kawaida sh 47,510,000,000/= kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Wizara na majukumu ya kimataifa Sh. 9,000,000,000/= .

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea na kujadili mapendekezo hayo, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kamati inasisitiza Wizara hii ipewe kasma ya maendeleo kwa kuwa ina majukumu mengi na makubwa katika ujenzi na ukarabati wa nyumba za balozi zetu nje ya nchi. Kukosekana kwa kasma hii kunaigharimu sana serikali kwa mabalozi na maofisa wao kulazimika kuishi katika majumba ya kupanga ikiwa ni pamoja na balozi zenyewe kuwa katika majumba ya kupanga kutokana na kukosekana kwa nyumba tunazozimiliki au uchakavu wa nyumba hizo.

Kasma ya Wizara hii ikithamanishwa na Dola za Kimarekani, imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka pamoja na kwamba majukumu yake yanazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka ikiwemo kuongezeka kwa balozi nje ya nchi. Hali hii inaonyesha kuwa serikali yetu haina fedha za kutosha kwa ajili ya kuiwezesha wizara hii kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inashauri idadi ya balozi zetu nje ya nchi zipunguzwe ili zitakazobaki zihudumiwe kikamilifu kwa kutumia fedha chache zilizopo.

Wizara hii pia inabeba majukumu mengine ambayo hayahusiani moja kwa moja na shughuli za wizara hii ikiwemo michango ya makubaliano ya kimkataba (*contractual obligations*) ambayo ni pamoja na *African Peer Review Mechanism (APRM),* maandalizi na kuhudumia Mkutano wa *Sullivan*, uanzishaji wa Mahakama ya Afrika. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya majukumu hayo ni sh. 9,000,000,000/= ambazo pia hazitoshi kwani kiasi ambacho kingekidhi kutekeleza majukumu hayo kikamilifu kinakadiriwa kufikia Sh.30,786,700,000/=.

Kamati inashauri michango na fedha za kuhudumia majukumu ya kimataifa kama haya zikae Hazina badala ya kuziweka kwenye bajeti ya Wizara hii na kuonekana kuwa imepewa fedha nyingi wakati si kweli.

Kamati inasikitishwa na majukumu makubwa ambayo baadhi ya mabalozi wetu wamekabidhiwa tofauti na jinsi wanavyowezeshwa. Kwa mfano balozi wa Tanzania nchi za Skandinavia anawakilisha nchi nane (8) ambazo ni *Norway, Sweeden, Denmark, Finland, Luxemburg, Iceland, Estonia na Latvia*. Aidha balozi wa Tanzania aliyeko nchini Japan anawakilisha nchi za Japani, *New Zealand*, Australia, Korea ya Kusini,

Philippines na Visiwa vidogo vidogo vya *Pacific* licha ya ukweli kwamba nchi hizi zote ziko mbalimbali sana.

Watendaji wa balozi hizi na zingine zinazofanana na hizi ni wachache na vitendea kazi pia havitoshi, hali hii inawakatisha tamaa watendaji hao na inarudisha nyuma utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi ambayo ndiyo Sera ya Mambo ya Nje kwa sasa. Kamati inashauri mabalozi wetu wakabidhiwe mzigo unaobebeka kwa kuwawezesha na kuwapa maeneo madogo ya uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, katika kuchagua nchi za kuwa na uwakilishi serikali iangalie nchi ambazo zina umuhimu kiuchumi badala ya uendelea kufungua balozi mpya kwa mtazamo wa kisiasa kama ilivyo enzi za ukombozi wa Bara la Afrika na enzi za vita baridi. Kwa mantiki hiyo kamati inashauri kuwa iwapo itahajika kufungua balozi mpya balozi hizo zifunguliwe katika nchi zenye mwelekeo wa kukua kiuchumi kama vile Korea Kusini, *Vietnam* na kadhalika kwa kuwa nchi yetu inaweza kunufaika zaidi kiuchumi kwa kushirikiana nazo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inakusanya mapato kupitia mauzo ya viza nje ya nchi ambapo mwaka 2007/2008 inatarajia kukusanya jumla ya Sh.8,925,000,000/=. Kamati inashauri fedha hii iwe nyongeza ya bajeti ya Wizara ya mwaka huu ambayo itaongezwa na Shilingi bilioni 59 zilizopangwa kwa ajili ya Wizara hii badala ya ilivyo sasa kwani makusanyo hayo yanatumika na Wizara lakini ndani ya bilioni 59 zilizokubaliwa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikiria kuanzisha sheria itakayoruhusu Mtanzania kuwa na uraia wa nchi mbili kwani kuna Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi na wanataka kuwekeza katika mabenki yetu lakini wanashindwa kutokana na taratibu za kibenki.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuhimiza Watanzania wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi kuwekeza nchini mwao kwani hiyo ndiyo imekuwa sera ya nchi nyingi duniani katika zama hizi za Diplomasia ya Uchumi. Katika baadhi ya nchi ikiwemo nchi jirani ya Kenya imewekwa mikakati maalumu ya kuwatafutia watu wao ajira nje ya nchi yao na kwa kufanya hivyo wanapata fedha nyingi za kigeni. Hivyo tunashauri nchi yetu iweke mkakati maalumu wa kuwahimiza Watanzania kutafuta kazi nje ya nchi kwa utaratibu unaokubalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kuhusu mapendekezo ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka huu wa fedha wa 2007/2008. Ni kweli kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara hii hazitoshi, hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa kuweko na nidhamu ya hali ya juu katika kutumia fedha iliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa kuandaa taarifa hii na kunipa heshima ya kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Nashauri Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kupitisha mapendekezo ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika bajeti hiyo ambayo ni jumla ya shilingi 59,041,192,000/=.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena, vilevile nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Killimbah kwa kuwasilisha vizuri na kwa utaalamu Taarifa ya Kamati. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Khalifa, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwenye masuala ya Mambo ya Nje.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, na mimi napenda kutoa shukurani kwa niaba ya Kambi yetu kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kama Kanuni za Bunge zinavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na neema na uzima. Aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa jimbo la Gando kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono kwa dhamana hii nzito. *(Makofi)* .

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa viongozi wetu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kutoa mwongozo sahihi wa Kambi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Pia niwashukuru wenzetu wote katika Kambi ya Upinzani kwa msaada na maelekezo mazuri. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ushauri na michango mbalimbali walionipa. Sina budi kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Manaibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano, misaada na ushauri mbalimbali wanaonipa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana familia yangu kwa kunivumilia katika muda mrefu ambao ninakuwa sipo nao katika kutekeleza majukumu ya Taifa letu. Kwa kweli uvumilivu wao kwangu mimi unanipa moyo sana na nawatakia waendelee kuwa na subira mpaka pale ambapo tutafikia katika malengo tuliyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine niungane na wenzangu kutoa pole kwa wale wote waliofikwa na misiba mbalimbali katika ajali na vifo vingine vya kawaida katika kipindi hiki chote tukiwa hapa Bungeni. Mungu awafariji katika wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Spika, nianze na kuongelea juu ya Mpasuku wa kisiasa – Zanzibar. Nchi yetu imepata sifa nyingi kwa kusuluhisha migogoro ya nchi jirani, aidha, imepata sifa kwa kuhifadhi wakimbizi. Lakini pia nchi yetu imekumbwa na migogoro ya kisiasa ambayo ilitokana na chaguzi za 1995,2000 na huu wa 2005,hadi Jumuiya ya kimataifa kupitia Jumuiya ya Madola ikaingilia kati na kupatikana muafaka wa 1999,ambao haukutekelezwa na kuipelekea Nchi yetu kuingia katika mgogoro mwingine 2000 hadi kupelekea watu wetu kupoteza maisha. Kwa mara ya kwanza Nchi yetu ikazalisha wakimbizi.Vyama vyetu vya CCM na CUF,mara hii vikaamua kuutatuta mgogoro huo kwa nia ya mazungumzo bila ya msuluhishi kutoka nje.

Muafaka huu tuliuita *"Home Made*". Ili kutoa indhari ya hatima ya nchi juu ya amani na usalama wake, vyama vyetu vilisema"Kwamba kumekuwepo na Mgogoro wa Kisiasa hapa nchini ambao chimbuko lake ni Uchaguzi Mkuu wa 1995 na kuendelea katika Uchaguzi Mkuu wa 2000 hadi kufikia matukio ya tarehe 26 na 27 Januari 2001 yaliosababisha watu kadhaa kupoteza maisha na wengine kujeruhiwa. Aidha, vyama vyetu vilisema "Kwamba vyama vyetu viwili vimejifunza kwamba kuna haja ya kutekeleza makubaliano yanayofikiwa kwani kinyume cha hayo ni wananchi kupoteza imani na njia ya mazungumzo kama ndiyo njia sahihi ya kutatuta migogoro katika jamii."

Mheshimiwa Spika, Rais wetu baada ya matokeo ya uchaguzi wa 2005,ameanzisha mazungumzo ambayo vyama vya CCM na CUF kwa mujibu wa makubaliano ya Makatibu wa Kuu wa vyama hivyo yatakuwa yamemalizika ifikapo tarehe 15.08.07.

Kambi ya Upinzani inapenda kuuungana na Mjumbe wa Halimashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Dr.Salim Ahmed Salim pale aliposema "Kitendo cha Kubeza Upatikanaji wa Muafaka Zanzibar, ni cha hatari kwa kuwa hakiwezi kuvuruga amani na utulivu visiwani humo peke yake, bali Tanzania nzima. "Aliendelea,"Muafaka ni jambo la msingi. Kwa sababu utaiweka nchi katika utulivu. Utulivu wa nchi ni muhimu

sana.Wanaobeza muafaka watembelee nchi nyingi duniani waoene jinsi zilivyosambaratika".

Mheshimiwa Spika, lengo la Rais Kikwete kuamua kuwepo kwa mazungumzo ya muafaka, ni kuhakikisha amani na utulivu nchini vinadumu. Hatuwezi kupatanisha wenzetu na kuwategemea waheshimu makubaliano wakati walimu wao ndio mabingwa wa kutoheshimu na kutekeleza kikamilifu tunayokubaliana. Kambi ya Upinzani inaomba kutoa indhari kuwa ni vyema mazungumzo yakamalizika,na kukawa na chombo kitakachohakikisha utekelezaji wa makubaliano hayo kabla ya uchaguzi 2010 kwani kama vilivyosema vyama vyetu katika miafaka iliopita kwamba chanzo cha migogoro hiyo ni chaguzi. Kinga ni Bora Kuliko Tiba.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje kwa muhtasari, ni Wizara kubwa na ya muhimu sana kwani mageuzi yote ya kiuchumi yanayotokea hapa nchini, na sifa tunazojivunia zinatokana na mafanikio ya Wizara hii. Pindi sera zake zikishindwa kuwa na mtazamo endelevu basi nchi yetu itakuwa na sura isiyopendeza.

Aidha, kama watendaji wake wakiweka mbele maslahi binafsi kuliko ya Taifa katika utendaji, matokeo yake ni hasara kwa taifa letu. Hii ndiyo Wizara inayotoa taswira ya nchi yetu katika nyanja za kimataifa. Wizara hii imepewa jukumu la kulinda na kutetea maslahi ya taifa letu (kiusalama na maendeleo ya kiuchumi) katika nyanja za kimataifa. Na kwa kweli kwa kiwango kikubwa inajitahidi kutekeleza jukumu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuundwa kwa Sera Mpya ya Mambo ya Nje hapo mwaka 2001 bado misingi yake ilikuwa imara kulitetea taifa letu. Moja ya msingi wa Sera yetu ya Nje ni suala la usalama wa taifa letu. Hili liangaliwe kwa dhana pana sana.

Usalama si tu hofu ya kuvamiwa kijeshi bali pia usalama wa maliasili zetu kama vile ardhi, madini na misitu yetu, wanyama wetu, tamaduni na fikira zetu, na maslahi ya taifa letu kiuchumi. Pia msingi mwingine mkuu wa sera yetu ni maslahi ya wananchi wetu *(people's welfare),* kuona kwamba wananufaika na sera zetu za uhusiano wa kimataifa katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Misingi hii miwili yaani usalama wa taifa letu na maslahi ya wananchi wetu huunda nguzo kuu ya sera yetu ya nje yaani maslahi ya taifa *(national interest),* ambayo Wizara hii iko mstari wa mbele kuitetea.

Mheshimiwa Spika, dhana ya utandawazi iliyotuweka karibu na washiriki wetu wa maendeleo isituzibe mdomo au kutufumba macho kuyaona na kuyasemea maslahi ya taifa letu. Kanuni zilizo ndani ya sera yetu ni nzuri lakini kuna tatizo linapokuja suala la utekelezaji wa sera hizo. Naomba niyazungumzie machache katika Wizara hii ambayo ni vikwazo vya maendeleo yetu. Ubadhirifu wa fedha, ni moja ya tatizo kuu linalorudisha nyuma maendeleo ya nchi zinazoendelea ni kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha wa hali ya juu. Ubadhirifu huo huonekana katika sura mbali mbali zikiwemo; masurufu yasiyorejeshwa, matumizi ya fedha bila ya kufuata utaratibu, matumizi ya fedha yasiyo na hati au maelezo ya kutosha, upotevu wa fedha, upotevu wa vifaa, na matumizi ya fedha za umma kwa maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ubadhirifu wa namna hii Serikali zetu hushindwa kufikia malengo yaliyopangwa katika Bajeti za kila mwaka. Inasikitisha sana kuona kuwa nchi masikini ambazo bado zimegubikwa na utegemezi wa hali ya juu zinashindwa kutumia vyema hata hicho kidogo kilichopo kwa ajili ya maendeleo yetu wenyewe hatua kwa hatua. Si kweli kuwa nchi hizi haziwezi kutumia kichache kilichopo kwa ajili ya kusukuma gurudumu la maendeleo, bali mtindo uliopo ni ule wa "kuchota maji kwa kutumia pakacha" wakati tunakoelekea ni mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2006 iliyotolewa Machi 2007, ipo tuhuma ya matumizi mabaya na ubadhirifu wa fedha katika baadhi ya ofisi za kibalozi. Kwa mfano, ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini unadaiwa kutumia shilingi 312,260,173 kwa ajili ya kununulia nyumba namba 818 iliyopo katika barabara ya *Moveleta Park* mjini *Pretoria* bila ya kufuata taratibu. Ubalozi huo pia unaelezwa kuwa umetumia shilingi 20,572,143 kwa ajili ya matumizi ambayo sio ya kawaida na masurufu yasiyorejeshwa ya shilingi 38,662,493. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza nao umetumia shilingi 128.5 kumwajiri mkandarasi bila ya kufuata taratibu sahihi za uajri. Pia ubalozi huo umebainika kutumia shilingi 56,681,914 kwa ajili ya matengenezo na huduma za ulinzi bila ya kuwepo mkataba na kwamba ubalozi huo haujarejesha masurufu ya shilingi 17.1 iliyopewa. *(Makofi)*

Ubalozi wa Zambia nao umeripotiwa kutoa shilingi 56.6 kwa ajili ya matumizi ya huduma na matengenezo bila ya mikataba. Vilevile, ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani unadaiwa kushindwa kukusanya maduhuli ya thamani ya shilingi bilioni 1.Balozi nyingine ambazo zimeripotiwa kwa ubadhirifu wa fedha hasa kwa kutorejesha masurufu ni ubalozi wa Tanzania *Addis Ababa* kiasi cha shilingi 11.2 milioni na ubalozi wa Tanzania *Moscow* kiasi cha shilingi milioni 8.0. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ubadhirifu wa fedha katika Wizara, Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mku wa Hesabu za Serikali imeonyesha kuwa malipo katika Ofisi za Balozi ya shilingi bilioni 10, hayakurekebishwa kukidhi matumizi halisi katika akaunti ya matumizi ya Wizara. Vilevile, imegundulika kuwa kuna tofauti isiyolingana ya shilingi bilioni 3.1 katika marejesho ya matumizi yasiyowasilishwa Wizarani na kiasi kilichoingizwa katika akaunti ya matumizi. Pia kiasi cha masurufu maalumu yasiyorejeshwa katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni shilingi milioni 64.1.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaelezwa kuwa imetumia kiasi cha shilingi 245,031,107 bila ya kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano. Pia ruzuku ya shilingi 1,640,088,800 hazikukaguliwa na matumizi ya shilingi 192,769,919 hazikutolewa maelezo. Pia ikumbukwe kuwa kulikuwepo na upotevu wa fedha taslimu, kiasi cha shilingi 14,793,740 katika Wizara ya Mambo ya Nje kwa mwaka 2005/2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yetu kuwa hatua mwafaka zinachukuliwa kwa wote wanaohusika na ubadhirifu huu, hatua hizo zichukuliwe mara tu baada ya taarifa zinapotolewa na kuthibitika. Hata kama hati hizi hatimaye hupatikana haina maana kuwa hapakuwa na ubadhirifu, na hati hizo hutungwa kutimiza masharti ya ukaguzi. Izingatiwe kuwa Mkaguzi kwa kawaida hutoa tahadhari kwani yeye hatafuti wizi wala ubadhirifu bali huangalia tu kama taratibu za kihasibu zimefuatwa.

Kazi ya kutafuta kama kuna wizi au ubadhirifu ni ya msimamizi, na msimamizi mkuu wa Wizara na Serikali kwa ujumla ni Bunge hili.

Tunatakiwa kuwa makini na tusiridhike tu kauli za kueleza kuwa 'hati zote zimepatikana na hoja zimefungwa'. Hili ni jambo la hatari sana. Kwa kuzingatiwa hilo, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara ilieleze Bunge hili ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wote waliothibitika kusababisha matumizi mabaya ya fedha. Maduhuli yatokanayo na viza, moja ya chanzo muhimu cha mapato ndani ya Wizara hii ni uuzaji wa Viza kwa Wageni waingiao nchini mwetu. Mapato haya ni muhimu kwani husaidia kuiwezesha bajeti ya Wizara hii. Kambi ya upinzani ingependa kujua ni viza ngapi ziliuzwa na ofisi zetu za kibalozi kwa mchanganuo maalum kwa mwaka uliopita na ni kiasi gani cha pesa kilipatikana kutokana na viza hizo katika kila balozi?

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Haki za Binadamu, tunaelewa kuwa Tanzania imepata heshima kubwa ya kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa Mahakama ya Haki ya Afrika. Kambi ya Upinzani inaipongeza Serikali yetu kwa heshima hii kubwa. Tunaamini kuwa tutaitunza heshima hii kwa kuwa mstari wa mbele katika kuheshimu haki za binadamu, utawala wa sheria, amani na utulivu, na kwamba Serikali yetu itahakikisha kuwa dosari na rekodi mbovu za uvunjaji wa haki za Binadamu nchini mwetu hazijirudii tena ili kujijengea heshima miongoni mwa mataifa mengine. Tanzania kama mwenyeji wa Mahakama hii inahitaji kufanya maandalizi makubwa ili kufanikisha uanzishwaji wake. Katika mwaka 2006/2007, Wizara iliahidi kufanya maandalizi yote yanayohitajika ili azma ya kuanzishwa Mahakama hiyo mjini Arusha itimie haraka. Je, Wizara imekamilisha maandalizi hayo ili mahakama hiyo itakapoanzishwa iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi?

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Kikanda, Kambi ya Upinzani inatambua ushiriki mzuri ambao umekuwa ukionyeshwa na Serikali yetu kama mwanachama wa *SADC.* Tunapongeza juhudi za nchi yetu kuweza kuchangia kiasi cha dola 500,000 za kimarekani kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu huko *Gaborone*, Botswana na kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Chombo cha *SADC* kinachohusika na kuratibu masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama. Kambi ya Upinzani inaomba juhudi hizi zisirudi nyuma bali ziongezwe kwa heshima ya Taifa. Upo mpango wa kuanzishwa kwa Viza moja kwa nchi wanachama wa *SADC*, mpango huu una lengo la kuwafanya wananchi wa nchi hizi kuwa huru kwenda nchi yoyote bila ya matatizo yoyote. Kambi ya Upinzani inapenda kupata tamko la Serikali kuhusu jambo hili, hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania pia ina utaratibu kama huo katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki, na wakati huo huo tamko rasmi halijatolewa kuhusu ushiriki wa Tanzania katika *COMESA*.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu pia ipo katika ushirikiano na nchi za Uganda na Kenya, na kwa sasa pamoja na Burundi na Rwanda chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi yetu imepania katika kuboresha ushirikiano huu kiasi cha kuunda Wizara mahususi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara ya Mambo ya Nje ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa misingi ya Sera yetu ya Nje *(Foreign Policy)* inazingatiwa. Mtazamo wetu ni kwamba, harakati hizi kwa upande wa nchi yetu ni lazima ziweke mbele maslahi ya taifa letu *(National interests)* kwa tafsiri iliyopana zaidi.

Mheshimiwa Spika, haya yanajumuisha pia kuzingatiwa kwa maslahi ya ajira kwa vijana wetu, manufaa na hasara za ushindani wa kiuchumi endapo tukiwa na soko moja, kuondoa matatizo ndani ya nchi yetu, na kujitayarisha kiuchumi ili kunufaika kama nchi. Yote yanahitaji muda wa kutosha wa kutathmini hatua moja baada ya nyingine tunazoafikiana. Tunahitaji kujifunza kutoka Jumuiya ya Ulaya, ambayo kwa kiwango fulani imepiga hatua kubwa, lakini imekwama katika kuunda Katiba ya Umoja huo inapoelekea kwenye Umoja wa Kisiasa. Sisi hatuna sababu kabisa ya kwenda kwa haraka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa, haya unayoyasoma yako wapi, hayapo Mezani!! Ni ukurasa wa ngapi, Taarifa ni hapa.!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, yamo ndani ya marekebisho madogo niliyoyafanya na nimeyagawa.

**SPIKA:** Hayako Mezani hapa! Huwezi kusoma kitu ambacho hakipo Mezani, una-*table* kitu Mezani, ndicho unachokisoma ndiyo utaratibu, ndiyo Kanuni zetu. Ukirekebisha tu peke yako halafu ukasoma kitu hata Spika hana, mimi nafuatilia. Kwa sababu ndiyo wajibu wangu huo.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Ahsante Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Kwa hiyo, hayo ambayo hayapo hayataingia *Hansard.* Na unapoteza muda kuyasoma.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Nilitoa Mheshimiwa Spika, niliwasilisha Mezani. Sijui labda haikufikishwa hiyo *copy* yenye masahihisho kwako wewe.

**SPIKA:** Haipo hapa!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Sijui imekuwaje nimetoa hiyo *copy* yenye masahihisho kwako wewe.

**SPIKA:** Basi rejea kwenye Mambo ya Nje.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ushirikiano na mataifa mengine, jitihada za Wizara za kuboresha mahusiano na nchi nyingine ni za kupongezwa kwa sababu si tu jitihada hizi huliweka taifa letu katika mahusiano mema na nchi nyingine lakini pia taifa letu hupata misaada ya kimaendeleo kutoka mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, pia China iliahidi kufungua zaidi masoko yake kwa bidhaa kutoka nchi za Kiafrika na kuongeza orodha ya mazao na bidhaazitakazoingia soko hilo bila ya kulipia ushuru kutoka 187 hadi 440. Ahadi nyengine ni pamoja na kujenga vituo 30 vya kuzuia na kutibu ugonjwa wa malaria barani Afrika, kuleta vijana wa kujitolea wapatao 300 barani Afrika, na kujenga shule za msingi vijijini zipatazo 100 barani Afrika.

Kwa mfano, nchi yetu pamoja na nchi nyingine za Kiafrika zimekuwa na China chini ya uhusiano wa kidiplomasia uitwao *"Forum on China-Africa Cooperation (FOCAC)"*.

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2006 ulifanyika mkutano wa wakuu wa nchi na Serikali ya China na nchi za Kiafrika ambapo Serikali ya Jamhuri ya watu wa China ilitoa ahadi kwa nchi za Kiafrika. Miongoni mwa ahadi hizo ni kutoa dola bilioni 3 za kimarekani kwa ajili ya *preferential loans*, na dola bilioni 2 za Kimarekani kwa ajili ya *preferential buyers credit* kwa nchi za kiafrika katika kipindi cha miaka 3 (2007-2009).

Vile vile, waliahidi kuanzisha mfuko wa maendeleo kati ya China na Afrika *(China-Africa Development Fund).* Mfuko huo utakaokuwa na dola bilioni 5 za kimarekani utatumika kuhamasisha na kuyasaidia makampuni ya Kichina kuwekeza katika nchi za Kiafrika. Ili kunufaika na mfuko huu, nchi za Kiafrika zilitakiwa kupanga na kuwasilisha miradi ya kupewa kipaumbele katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa nafasi hii kwa Tanzania bado Serikali yetu haionekani kuwa makini katika kuchangamkia bahati hii adhimu kutokana na wadau kuchelewa au kushindwa kuandika na kuwasilisha miradi mapema wakati nchi nyingine za Kiafrika zimeshawasilisha miradi yao. Kushindwa kupanga na kuwasilisha mapema miradi yenye tija kubwa kwa taifa kutatufanya tuendelee kulalamika kuwa juhudi za wawekezaji kutoka nje zimekuwa zikielekezwa katika miradi isiyo na mchango mkubwa katika maendeleo ya uchumi wetu. Kambi ya Upinzani inahoji sababu za uzorotaji unaofanywa na baadhi ya wadau.

Mheshimiwa Spika, vile vile, tunapendekeza kuwa miradi itakayowasilishwa isiwe tu ni kutekeleza wito bali iwe ni yenye malengo makubwa ya kuinua uchumi wetu. Ongezeko la idadi ya bidhaa ziruhusiwazo kupelekewa nchini China na kuondolewa ushuru ni bahati ya pekee ambayo itainufaisha Serikali yetu na wanachi wetu ikiwa tutaitumia vizuri.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ichukue juhudi za kuwaelimisha wajasiriamali wadogo na wakubwa juu ya bidhaa zinazotakiwa kupelekwa huko na utaratibu unaopaswa kufuatwa. Hiyo tu haitoshi, bali Serikali ina jukumu kubwa la kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa bidhaa ambazo zinatakiwa na zinapatikana nchini zinapelekwa kwa wingi zikiwa katika ubora ulio juu ili kupambana na ushindani wa soko hilo.

Mheshimiwa Spika, mahusiano mengine ambayo ni muhimu katika kunufaisha taifa letu ni yale kati ya nchi yetu na Brazili hususan baada ya uzinduzi wa tume mpya ya pamoja ya ushirikiano kati ya nchi hizi mbili hapo Mei, 2006. Maeneo ambayo Tanzania ilitarajia kunufaika ni pamoja na nishati, madini, michezo, kilimo, utalii na afya. Ushirikiano huu una umri wa mwaka mmoja sasa, na kwa kuwa Wizara iliahidi kufuatilia kwa karibu utekelezwaji wa makubaliano ya tume hiyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kambi ya Upinzani inapenda kujua kiasi cha mafanikio ambayo yamekwishapatikana kutokana na ushirikiano huu. Tuna imani kabisa ushirikiano wa aina hiyo hiyo ni muhimu na nchi kama *Trindad* na *Tobago*, hasa ikizingatiwa kuwa Waziri Mkuu wao alikuwa mgeni rasmi hapa kwetu hivi karibuni na tuna imani Rais wetu pia atapata nafasi ya kutembelea nchi hiyo hapo baadaye mwaka huu.

Mapitio ya bajeti ya Wizara 2007/2008, yanaonyesha kuwa nchi yetu imekuwa na mahusiano mazuri na wenzetu. Hivyo basi, kutokana na hali hiyo, Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa ni nyeti inayohitaji kuwezeshwa kibajeti ili kuboresha utendaji wake wa kazi ili kutuweka karibu na mataifa mengine miongoni mwake wakiwemo wahisani wetu.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inayoonyesha vipaumbele katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 imeainishwa kuwa Wizara imepangiwa kiasi cha shilingi milioni 59.0 ya Bajeti. Kiasi hiki kinaonesha kuwa ni kidogo kulingana na majukumu ambayo Wizara imepanga kuyatekeleza katika mwaka 2007/2008. Kulingana na maelezo ya Wizara kiasi kinachohitajika ni shilingi bilioni 70.5 ili kuweza kuyamudu majukumu ya mwaka jana kwa kiwango kile kile.

Pia zinahitajika kiasi cha shilingi bilioni 10.8 kugharamia majukumu mengine mapya kwa mwaka huu. Vilevile, kiasi cha shilingi milioni 36.3 kinahitajika kwa matumizi ya lazima ili balozi zetu ziweze kufanya kazi zake za kimsingi na kulinda heshima ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia inaelezwa kuwa maeneo mapya pamoja na matumizi ya lazima yanagharimu kiasi cha shilingi milioni 47 kiasi ambacho ni sawa na asilimia 86.6 ya Bajeti yote ya Wizara. Hivyo basi, kazi zote za Wizara zinabakiziwa asilimia 13.4. Kinachojitokeza ni kwamba Wizara haikupewa fedha za kukidhi mahitaji yake sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa ni haki kabisa Wizara hii kutengewa fungu la kutosha ili kuweza kuliwakisha vyema taifa letu miongoni mwa mataifa mengine. Tunaiomba Serikali izingatie umuhimu wa Wizara hii katika Bajeti zake ili kuiwezesha kufanya shughuli zake kwa ufanisi zaidi hasa ukizingatia mchango wa Wizara hii katika maendeleo ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Haki za Binadamu katika Sheria za Kimataifa, Tanzania imetia saini Tamko la Ulimwengu juu ya Haki za Binadamu *(Universal Declaration of Human Rights),* vilevile imeridhia mikataba mikubwa ya kimataifa ya Haki za Binadamu. Hivyo basi Tanzania ina jukumu la kuhakikisha kuwepo kwa misingi ya haki za binadamu kupitia mikataba ya kitaifa na kimataifa. cha kushangaza ni kuwa kumekuwepo na tofauti kati ya sera na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imetia saini mikataba kadhaa ya kimataifa lakini imeshindwa kutimiza baadhi ya masharti husika, kama vile kuwasilisha ripoti, kitendo ambacho kinaionyesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi ambazo hazitilii maanani sana masuala ya haki za binadamu. Kwa mfano, mwaka 1985 Tanzania iliridhia mkataba uitwao "*The International Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination Against Women, 1979 (CEDAW)"* ambapo Tanzania inatakiwa kuwasilisha ripoti kila baada ya miaka minne. Cha kushangaza hakuna ripoti ambayo imewasilishwa tangu mwaka 1998. Vilevile, mkataba uitwao *"The International Convention on the Rights of the Child, 1989 (CRC)"* ambao uliridhiwa na Tanzania mwaka 1991, ripoti yake toka Tanzania imekuwa ya kusuasua. Aidha, kila baada ya miaka mitano kamati ya haki za mtoto hutakiwa kupokea ripoti, wakati ripoti ya Tanzania ya mwaka 1998 ilipokelewa mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, nimetoa mifano michache tu kati ya mingi kama ripoti ya "*Legal and Human Right Centre"* iliyopewa jina *"Tanzania Human Rights Report 2005"* inavyoonyesha. Hii inamaanisha nini? Au nchi yetu inaona aibu kudhihirisha kuwepo kwa baadhi ya vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu katika nchi yetu inayosifika kwa Amani? Au ndio tunasema hakuna uvunjaji wa haki hizi unaotendeka? Basi angalau iandikwe ripoti ya kusifia jinsi nchi yetu inavyozingatia haki za binadamu ili tujenge heshima miongoni mwa mataifa. Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa nchi yetu ijitahidi sana katika kulinda uhuru na haki za msingi za kila mwanadamu, na kwa kuwa Tanzania imesharidhia mikataba hiyo basi haina budi kuwajibika kama inavyopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia si tu ni msingi imara wa kuiletea Wizara ufanisi kiutendaji kwa kuwa ni chemchemi ya rasilimali ya watu waliobobea katika fani za kidiplomasia, bali pia huwanufaisha vijana wanaotaka kujiendeleza katika

elimu ya kidiplomasia kujijengea nafasi za ajira na hapo baadae kuwa wawakilishi wema wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hadhi ya chuo hiki bado si ya kuridhisha kulingana na vyuo vingine. Kambi ya Upinzani ingependa kujua Wizara imesaidiaje mpaka sasa Chuo cha Diplomasia kutambulika kwa vyeti vyake na kuwa na hadhi inayoridhisha. Pia ni nini kimefanyika kusaidia Chuo hiki ili kudhaminiwa na vyuo vingine *(Validation).*

Mheshimiwa Spika, uwekezaji ni sekta nyeti na yenye mchango mkubwa katika pato la taifa letu na maendeleo kwa ujumla. Sekta ya uwekezaji inaweza kujenga ama kubomoa maslahi ya taifa kutegemeana na umakini wa Serikali katika kuendesha, kudhibiti na Kuboresha sekta hii.

Hii ni kutokana na kuwa wawekezaji walio wengi (hasa wa kigeni walio na mitaji mikubwa) wanaweka mbele maslahi yao binafsi kwa kujilimbikizia faida. Kwa upande mwengine, pale Serikali inapoweza kuidhibiti sekta ya uwekezaji kwa sera zilizo sahihi, kufanya maamuzi sahihi na kuingia mikataba yenye kuzingatia maslahi ya taifa letu, sekta hii huwa chachu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nililizungumzia suala la uwekezaji na bado naendelea kulizungumzia kutokana na umuhimu wake. Kambi ya Upinzani inatambua juhudi ambazo zimefanyika kurekebisha baadhi ya makosa kama vile kupitia upya baadhi ya mikataba kwa maslahi ya taifa, lakini pia tutaendelea kukemea maamuzi mabovu yanayoendelea kufanywa na Serikali yetu katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, moja ya maamuzi yanayohitaji kupewa umakini wa hali ya juu ni misamaha ya kodi wanazopewa wawekezaji kutoka nje wanapoanzisha biashara zao nchini. Serikali hupoteza mapato makubwa kutokana na ujanja na hila zinazofanywa na wawekezaji kutoka nje. Katika kuzingatia maslahi ya taifa letu ndio maana Bajeti mbadala iliyotolewa na Kambi yetu ikaishauri Serikali kupunguza misamaha ya kodi kwa asilimia hamsini ili kujiongezea Taifa pato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya ahadi ya Wizara katika mwaka 2006/2007 ilikuwa ni kuiletea nchi maslahi ya kiuchumi kwa kuwavutia wawekezaji wenye mitaji na teknolojia ya kisasa na watalii, na katika taarifa ya utekelezaji wa ahadi hizo Wizara imeeleza kuwa imeshiriki makongamano ya uwekezaji na maonesho ya biashara kwa nia ya kuitangaza Tanzania kiuchumi.

Pia taarifa imetolewa kuwa Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE)* ulituma ujumbe wake Oktoba, 2006 kutathmini maeneo ya uwekezaji nchini. Taarifa inaeleza zaidi kuwa mapema 2007 ujumbe maalumu wa wafanyabiashara kutoka *UAE* ulitarajiwa kufika nchini. Juhudi hizi ni nzuri na Kambi ya Upinzani haina budi kuzipongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, je, Wizara iko tayari kutueleza ujio wa wafanyabiashara hao? Na kama walikuja ni nini kilijiri katika ujio huo ama ni maeneo gani wafanyabiashara

hao wamepanga au kuamua kuwekeza? Mashaka tuliyonayo ni juu ya namna maslahi ya taifa letu yalivyozingatiwa. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kupanga maeneo yanayostahili kupewa kipaumbele katika uwekezaji ili kutumia nafasi kama hizi kuwaelekeza wawekezaji maeneo hayo ambayo kimsingi yanapaswa kugusa maisha ya walio wengi na kuliletea taifa mafanikio.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba wapo Watanzania wengi waliotawanyika katika nchi nyingi ulimwenguni kote. Kambi ya Upinzani inatambua juhudi ambazo tayari zimeanza kuchukuliwa kuwaleta karibu Watanzania wenzetu waishio nje, kama vile maongezi kati ya Mheshimiwa Rais wetu na Watanzania waishio Japani, China, Korea na Uingereza, Ghana na kadhalika. Juhudi za Balozi zetu kuhamasisha Watanzania waishio nje kuja kuwekeza nchini, pamoja na jitihada za kuandikishwa na kuweka taarifa za Watanzania waishio nje *(Data Bank)* kwa baadhi ya Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, kujua idadi na kuwahamasisha waje kuwekeza nchini tu haitoshi. Hii ni kwa sababu baadhi yao wameshapoteza uraia wao na kupata uraia wa nchi nyingine na hivyo kutojisikia amani tena kurudi nchini kuwekeza kama Watanzania. Jambo la msingi ni kuwajengea mazingira bora ambayo yatawapa haki kama Watanzania wajapo kuwekeza, ndio maana kambi ya Upinzani kupitia Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani ilipendekeza kupitisha sheria inayoruhusu uraia wa nchi mbili *(Dual Citizenship)*.

Mheshimiwa Spika, tumesikia hapa kuwa juhudi zinafanyaika Serikalini ili kuleta jambo hilo. Tunaomba basi liharakishwe ili kuondoa usumbufu ambao unajitokeza. Ikumbukwe kuwa miongoni mwa Watanzania hawa ni wawekezaji wazuri na wenye mitaji mikubwa na hivyo basi hatua hii itawapa haki wao na kujiona huru kwa kuchukuliwa kama wazawa na sio wageni wajapo nchini kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko ya Wanafunzi wa Kitanzania wasomao nchi za nje kuteseka kutokana na kukosa kupatiwa huduma za msingi walizoahidiwa na Serikali yetu.

Kwa upande wa Serikali yetu imekuwa na kigugumizi kwa kukwepa jukumu la kuwasaidia wanafunzi hao. Itakumbukwa kuwa malalamiko haya yalishawahi kutolewa na wanafunzi wa Kitanzania nchini Urusi na sasa hivi pia nchini *Ukraine*.

Mheshimiwa Spika, kesi ya wanafunzi wasomao *Ukraine*, pamoja na Serikali kukanusha kwa nguvu zake zote bila kujali ushahidi uliopo, inaeleweka wazi kuwa makosa yaliyofanywa na Bodi ya Mikopo ndiyo yaliyopelekea Watanzania hawa kuteseka huko nje. Pamoja na hilo, bado Serikali ina uwezo wa kulishughulikia jambo hili ili kutoa nafasi kwa wanafunzi hao kuendelea na masomo yao.

Kitendo cha Serikali kujivua mzigo huu kinaashiria kuwakana Watanzania hawa na hivyo basi kujiona kama waliotengwa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali sio tu kuwaokoa wanafunzi hao walioko nje, bali pia Serikali ihakikishe kupitia Balozi zetu kuwa wanafunzi wapatao ufadhili wa kusoma nchi za nje wanapewa msaada pale

inapohitajika. Balozi ziwe na utaratibu wa kufuatilia taarifa kamili za wanafunzi wasomao nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina imani kubwa sana na uongozi mpya wa Wizara hii, na kwa msingi huo tunategemea kuwa hatua za msingi za usimamizi wa matumizi na maduhuli ya Wizara zitazingatiwa. Kwa kumalizia, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa bajeti ya Wizara hii kuwa kubwa ni jambo la muhimu sana. Hata hivi sasa Serikali inaweza kuisaidia Wizara hii kuziba pengo lake la bajeti, kwa hazina kubeba baadhi ya gharama za kulipwa na mfuko mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa mara nyingine natoa shukurani zangu kwako kwa kunipa fursa hii, na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana, na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilipokuwa nawatambulisha wageni, Mheshimiwa Balozi wa Uingereza alikuwa ametoka, kwa hiyo, sasa naomba kumtambua Mheshimiwa Phillip Palm, balozi wetu wa Uingereza aliyeko hapa. Lakini nafurahi pia kumwona Jack, mwanae. Namfurahi sana kumtambulisha Jack, kwa sababu kijana anasoma Uingereza lakini aliniletea zawadi ya jiwe ambalo yeye amelipaka rangi za bendera ya Tanzania, ilihali alikuwa amejifunza tu, amekuwa akisoma juu ya ramani na kuona ramani ya Tanzania, basi akachora na akazipatia kabisa rangi zetu. Na jiwe lile liko nyumbani linatumika kama *paper white* yangu nyumbani.

*Thanks Jack, I am explaining to Honourable MPs about the very nice jester you made for Tanzania by drawing the National colours of Tanzania on that stone you remember which you brought when we had dinner at the residence of British High Commissioner. Thanks very much, continues keeping your interest in Tanzania, we are very proud of you thank you! (Makofi)*

Basi tunaendelea, Waheshimiwa orodha yangu ya wasemaji ni wako sita kama ifuatavyo: Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Mohamed Rished Abddallah, na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Tutaanza na Mheshimiwa Susan Lyimo na wakati huo ajiandae Mheshimia Lazaro Nyalandu.

**MHE. SUSANA A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ili kuweza kuchangia katika Wizara hii nyeti ambayo kwa kweli ni ya msingi sana katika mahusiano yetu na mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani lakini pia niwashukuru sana, Waziri Mheshimiwa Benard Membe, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Dr. Chami na Mheshimiwa Balozi Self Idd, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitaanza na suala zima la ukumbi wa *AICC* uliopo Arusha. Hakuna anayekataa kwamba ukumbi umekuwa ukikusanya watu wengi wa kimataifa na kitaifa katika masuala ya mikutano. Lakini pia ieleweke kwamba ukumbi

ule ulikuwa umejengwa mahususi kwa ajili ya ofisi wakati tukiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, nafikiri ni wazo zuri kwamba sasa tuwe na ukumbi mwingine mpya sehemu nyingine ili uweze kukidhi mahitaji ya sasa ya kimataifa uendane na hali ya utandawazi iliyopo sasa. Kwa kushauri ukumbi huu nadhani tungeweza kuujenga Bagamoyo ambapo pana historia kubwa sana ya nchi yetu na ni karibu na Zanzibar ambapo wageni pia wangeweza kwenda Zanzibar kuangalia mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala zima la mabalozi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anajali wanawake, lakini tukiangalia katika balozi zetu 32, kati ya hizo ni tatu tu ndiyo zinaongozwa na wanawake. Nakubaliana kwamba tuna wanawake ambao wako katika ngazi za kimataifa, kama Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro Balozi Dr. Getrude Ibengwe Mongela, Profesa Ana Tibaijuka, Bibi Mulamula na wengine. Lakini nazungumzia suala zima la mabalozi wetu ambapo najua Rais ndiye ana uwezo wa kuwateua. Kwa hiyo, kwa sababu mabalozi wanawake ni asilimia kumi tu ya mabolozi wote, kwa hiyo nafikiri twendako kutakuwa na wanawake wengi sana ambao wamesoma mambo ya diplomasia kama wanaume, kwa sababu hiyo kama Balozi zingine zitaundwa basi Mheshimiwa Rais angalie zaidi pia wanawake ili kuwe na usawa wa kijinsia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongelee pia masuala mazima ya uwekezaji. Kama alivyosema Mheshimiwa Khalifa, ni kweli suala la uwekezaji, wawekezaji wengi nchini sasa hivi ni kutoka nchi za nje, na nafikiri Wizara hii pia inahusika. Lakini tuangalie uwekezaji katika sehemu tatu, kuna ule uwekezaji katika makampuni makubwa kama ya simu ambayo kwa kweli watanzania wengi hawawezi. Pia kuna suala zima la madini. Utakubaliana nami kwamba sasa hivi wawekezaji karibu wote katika sekta hii nyeti ya madini ni wa kutoka nje, na hivyo kufanya Watanzania washindwe kuchimba madini yao.

Mheshimiwa Spika, ninalozungumzia zaidi ni hili la kuwekeza katika biashara ndogondogo. Ninavyoelewa mimi mtu anapokwenda nchi za nje lazima kuna kuwa na ile viza na anaeleza sababu, lakini sasa hivi ukiangalia nchini Tanzania kwa kweli kuna sekta hizi ndogo ndogo ambazo zimeshikwa na wawekezaji wa nje. Kwa hiyo, naomba Wizara iangalie suala hili kwa sababu hizo kazi zinaweza kufanywa na Watanzania na sio lazima zifanywe na watu wa kutoka nchi za nje. Nadhani ninavyosema hivi naeleweka, na siwezi kutaja nchi hizo lakini nadhani Wizara inazielewa. Nafikiri ufike wakati basi tuone ni jinsi gani tunaweza kusaidia wananchi wetu waweze kufanya zile kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la balozi zetu. Kwa kweli naipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inaendelea kuongeza balozi, lakini balozi hizi nadhani zingejikita zaidi kwenye masuala mazima ya uchumi na sio ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba nchi za Mashariki ya mbali zimendelea sana kiuchumi sasa hivi, lakini ukiangalia unakuta ubalozi tulionao ni wa China tu. Kwa hiyo, nafikiri ufike wakati sasa tuone ni jinsi gani tunaweza kufungua balozi katika nchi kama *Singapore*, *Malaysia,* ili waweze kusaidiana na balozi wa China,

ili wananchi ambao watanzania wengi wanaoenda kule kibiashara basi waweze kufanyiwa mambo yao kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia ningelee Chuo cha Diplomasia ambacho kimeongelewa na wengi. Kwa kweli Chuo hiki ni cha msingi sana na ni muhimu sana katika nyanja za kidiplomasia hapa nchini na nchi za nje na ndiyo chuo pekee ambacho kinatoa wanadiplomasia. Lakini kwa kweli chuo kile bado ni kidogo hakijapanuliwa kwa jinsi ambavyo kasi inavyoendelea Tanzania kuwa na mahusiano na nchi za nje. Pamoja na kuongeza kwa kupanua chuo hicho bado nafikiria kutokana na wale wataalamu waliopo pale, ifikie mahali sasa hivi tutengeneze kitu kinaitwa *annual lectures* za Mwalimu za Nyerere. Kwa kweli tutakubaliana kwamba Hayati Mwalimu Nyerere amefanya mambo mengi sana katika nchi yetu. Pamoja na umaskini tulionao, Tanzania imejulikana katika ramani ya dunia kutokana na mchango mkubwa wa marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere. *(Makofi)*

Kwa mfano, ukiangalia Afrika Kusini kila mwaka huwa kuna kuwa na *annual lectures* za Nelson Mandela, na hizi *lectures* zimekuwa zikiwaita watu mbalimbali maarufu kutoka nchi za nje na hata mwaka huu Kofi Anani ndiye alikuwa mgeni rasmi. Kwa hiyo, nadhani njia peke ya kumuenzi baba wa Taifa ni kuwa na hizi *lectures* kila mwaka ili watu waweze kutoa maoni mbalimbali kuhusu Nyerere na hivyo tutazidi kumuenzi baba wa Taifa. Naamini Chuo hiki kina mamlaka ya kuweza kufanya hivyo na naomba Wizara ifanye hivyo ili wajukuu wetu waendelee kumkumbuka Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala zima la ubaguzi wa rangi. Nadhani Wizara hii inahusika na hili limekuwa likijitokeza sana katika michezo. Katika mashindano ya vikombe vya dunia vya mipira yaliyokuwa yamepita na hata mashindano ya juzi, tuliona ni jinsi gani waafrika wamekuwa wakibaguliwa lakini pia sio tu kwenye kombe la dunia hata kwenye vilabu vya Ulaya ambapo waafrika wanachezea. Sasa nilikuwa naomba kujua Wizara hii inazungumziaje hili kwa sababu sijasikia tamko lolote la Serikali kuhusu suala hili. Na sasa hivi tunajua kwamba *World Cup* inakuja kuchezewa Afrika Kusini mwaka 2010, kwa hiyo , tulikuwa tunafikiri kwamba kwa kuwa wazungu hao ndiyo wanakuja na waafrika tutakuwepo sijui kama na sisi tutawazomea au tutafanyaje. Nadhani suala hili ni muhimu kwa Wizara kulitolea Tamko.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu balozi zetu na mazingira ya balozi hizo. Kwa kweli mazingira ya balozi zetu nchi za nje mengine hayaridhishi. Nakumbuka mwaka jana tulienda *Geneva* na tulikutana na Mheshimiwa Balozi kwenye ubalozi wetu *Geneva.* Kwa kweli ile ofisi ilikuwa hairidhishi kabisa lakini akatupeleka kwenye jengo jingine ambalo walikuwa wanategemea kulinunua. Sasa sielewi kama walilinunua na hali iko vipi! Nadhani pia hiyo ipo katika balozi nyingine, kwa hiyo, naomba Wizara iangalie ni jinsi gani inaweza ikasaidia wafanyakazi wanaofanya kazi katika Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuzungumzia pia mfuko wa Nyerere unaoitwa *Nyerere Foundation*. Kwa kweli hili jambo huwa naliona kama ni kero, kwa sababu naamini Serikali inamthamini Mwalimu Nyerere, kwa maana hiyo basi inatakiwa mfuko

huu udhaminiwe na Serikali na sio michango ya mtu mmoja mmoja. Napendekeza kuwe na bajeti kwa ajili ya huu mfuko ili tuone na kuiamini Serikali inayomuenzi Baba wa Taifa. Nakumbuka mwaka jana hili jambo lilizungumzwa na nilifikiria mwaka huu Waziri alipotoa hotuba angesema ni kwa jinsi gani Wizara yake imelichukua jambo hili au wana mapendekezo gani. Lakini katika hii hotuba sijaona chochote kuhusu mfuko wa Mwalimu Nyerere jinsi ambavyo utakavyokuwa unatunishwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni historia ya nchi yetu. Ni lazima historia ya nchi yetu iandikwe vizuri. Ni kweli tunajua kwamba nchi yetu ilifanya mambo makubwa katika ukombozi wa Bara la Afrika, na hapa nizungumzie jinsi gani Tanzania imezikomboa nchi nyingi. Nadhani hilo linajulikana, nchi zote za Kusini mwa Afrika zinathamini mchango wa Tanzania. Na labda niseme tu, kwa uzoefu wangu hapo majuzi tulivyokwenda *CPA*, tulienda *North Province* na kule tulimkuta Spika, ambaye yule Spika, kwa kweli anaongea Kiswahili na alikuwa Temeke. Alifurahi sana alivyoona Watanzania na hata katika hotuba yake alilitambua hilo, pamoja na kwamba tulikuwa nchi nyingi lakini aliweza kuongelea Tanzania jinsi ambavyo wanaithamini. Kwa hiyo, nadhani ni vyema basi na sisi tuandike historia yetu lakini pia Waheshimiwa Wabunge waelewe pia kwamba tulikuwa na kambi nyingi za wakimbizi, na nafikiri ifike mahali pengine Kamati mbalimbali ziwe zinapewa nafasi ya kwenda kutembelea kambi hizo ili waweze kujua jinsi gani Tanzania ilifanya mambo katika kukomboa nchi za Afrika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu gharama za Serikali. Japo hili linaweza labda likakera wengine, lakini mimi bado huo ni msimamo wangu. Wakati juzi Waziri wa Afrika Mashariki akiongea mara nyingi sana Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alikuwa anasaidia au anaongezea. Na mimi nafikiri hizi Wizara mbili zinafanana, kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba Wizara ya Afrika Mashariki iwe kitengo ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje, ili tuweze kupunguza gharama. Kwa sababu masuala ni yale yale ya kimataifa, kwa sababu Kenya, Uganda ni mataifa yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba kuungana na wenzangu kuunga mkono hoja hii ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Benard Membe kwa hotuba ambayo imekuwa na mwelekeo mpana na mzuri kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea vizuri, nchi nyingi sasa hivi ukipita ukisema wewe ni mtanzania wanakupokea vizuri, tunazidi kupata heshima. Ni jambo ambalo linafurahisha sana. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri aliposema kwamba dhana ya kwamba Tanzania ni nyota inayong'aa, inaendelea kukubalika katika mataifa mengi na kwa sisi labda niseme Wabunge na wananchi wa kawaida tukipita huko ukiwa Mtanzania heshima ya nchi iko pale pale. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa hilo.

Ningependa kuiomba Serikali na wanasema katika maisha hupati kitu unachostahili, kimsingi unapata kile unacho-*negotiate*. Nilikuwa naangalia nchi moja inaitwa *Guyano*, wao wame-*negotiate*, wananchi wao wanaweza kuingia nchi 100 dunia bila viza, na kinachotokea ni nchi ina *negotiate* na nchi moja moja. Na wengi tuseme wewe unakuja kwangu bila viza, *reciprocity* basi na watu wako na watu wangu waweze kuingia bila viza. Ni utaratibu mgumu katika sheria za kimataifa kwa sababu hizi zina uchumi unaotofautiana. Lakini nchi nyingi sasa zimeanza utaratibu kwamba kama watu wako wanaweza kuja kwangu bila viza basi na wa kwangu waje bila viza.

Ningeomba Wizara i-*comment* kwenye hili suala, hasa nchi zinawapa shida sana wananchi wetu wanaposafiri. *Mexico*, nafikiri ni mwaka jana nchi hii walianzisha sheria hiyo hiyo. Raia wao walikuwa wakifika Marekani wanapigwa *finger prints. Mexico* ikawa nchi ya kwanza dunia Mwamerika yeyote akifika naye anapigwa *finger prints*, raia wa nchi nyingine yeyote alikuwa anapita, lakini kwa sababu Marekani walikuwa wakifanya hivyo nao wakafanya hivyo. Hiyo ni gharama na hilo sio pendekezo langu, lakini ningeomba Serikali iangalie uwezekano wa ku-*negotiate* ili watu wetu kama ilivyo *Hong Kong*, Mtanzania akifika *Hong Kong* anaingia, Mkenya akifika anawekwa pembeni mpaka awe ana viza aliyoichukua Nairobi. Na ni ipongeze Serikali kwa hatua ile iliyofanya kwa sababu wafanyabiashara wetu wanapoenda *Hong Kong* na China maisha yao ni rahisi sana kuliko raia wa nchi zingine zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo napenda nizungumzie leo ni hili la *Dual Nationality* au uraia wa nchi mbili, ni dhana ngumu kidogo, na naomba nipingane na msemaji wa Kambi ya Upinzani, hili halikuwa pendekezo la Kambi ya Upinzani. Limekuwa pendekezo la Wabunge wa CCM tangu mwaka 1995, mwaka 2000 na 2003 lilijadiliwa. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na Serikali yao ndiyo wa kwanza kabisa katika kuleta hili suala *Dual Nationality*, naomba hiyo rekodi iwekwe sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Dual Nationality* inawatia watu wengine wasiwasi kwa sababu wanadhani ni dhana ambayo inamfanya mtanzania au inafanya wageni waweze kupata uraia wa Tanzania. Kinachotokea hapa ni kwamba uraia huu utamsaidia Mtanzania aliye nje kuweza kupata stahili *(privileges)* nyingi wanazopata raia wa nchi yake. Nilikuwa najaribu kuangalia nchi ngapi zimepitisha ile sheria, mataifa mawili duniani ndiyo yanaongoza kampeni ya kukataa *Dual Nationality* katika masuala mazima ya kimataifa.

Moja ni Japani, na nyingine ni Saudi Arabia na niliambiwa Saudi Arabia ukiwa na pasipoti ya nchi nyingine unatiwa ndani, it *is the criminal offence*, lakini pia nimeangalia katika sheria ya kimataifa (*international law)* hakuna mahali popote ambapo imekataza *Dual Nationality.* Mataifa mengi sasa hivi yameruhusu watu wao waweze kuwa na *Dual Nationality* kwa sababu imesaidia sana kuharakisha Mahusiano ya kimataifa na Uchumi na biashara.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa nitoe mfano wa India kwa sababu imekuwa ni mfano wa pekee wa kuigwa. Mapinduzi ya teknolojia ya India yameanzia *Selcon Valley* katika Marekani. Wale wahindi wote waliokwenda Marekani walikuwa

wanaruhusiwa kuwa na uraia wa Marekani. Katika teknolojia maalumu kama wewe sio raia wa nchi hiyo huruhusiwi kabisa kuingia katika maeneo ambayo wanaamini ni nyeti katika masuala ya usalama wa nchi, na ni pamoja na teknolojia.

Lakini Wahindi wale ambao walikuwa na fursa *(acces)* ya kuchukua uraia wa Marekani na walikuwa ni wanafunzi tu, walikwenda kusoma wakapata *acces,* wamesoma na wote wakaanza kurudi nyumbani kwao. Mfano *Microsoft*, nafikiri ni mwaka jana wameamua ku-*out source* teknolojia yao India. Wamejaribu kuangalia teknolojia za nchi nyingi na wakakutana na watu wengi ambao walikuwa na teknolojia. Bei yao ikawa rahisi, na ni *superior* tu kama ilivyo ya Marekani. Kwa sababu gani hawa vijana wa India walikuwa wanasoma *Selcon Valley,* au sehemu zingine Marekani walikuwa na *advantage* zaidi ya kijana wa Tanzania ambaye amefika kule na kuulizwa anachotaka kusoma na kuulizwa utaifa wake. Ukishasema tu utaifa wako ni Mtanzania unaambiwa *status* yako nchini Marekani ikoje. Wengine walau walikuwa na hadhi ya kuwa wakazi wa kudumu *(permanent residence)*, ni mtanzania lakini amepata haki ya kukaa pale kama mkazi wa kudumu na ikawasaidia. Na wahindi wanaiongoza dunia sasa hivi katika teknolojia zinazokuja sasa *(up coming technologies)* kwa sababu waliweza sana kutumia hii dhana ya *Dual Nationaliy*.

Mifano mingine imetolewa katika nchi ya *Hong Kong* ambayo ni sehemu ya China na *Taiwan.* Wameendelea sana kwa sababu dhana hii ya *Dual Nationality* iliweza kuwasaidia watu wao ku-*acces technologies* zilizopo mahali pengine. Ndugu zetu wale wanaofanya biashara, *Dual Nationality* kimsingi haimzui mtu na haimnyang'anyi mtu uraia wake, naomba niwatoe hofu watu wengi wanaofikiri kwamba hili suala la *Dual Nationality* litaingilia suala zima la usalama wa nchi. Mtu anapokuwa ni mzalendo anayependa nchi yake, siku zote usalama wa nchi yake na maendeleo ya nchi yake yatakuwa ni ya kwanza. Nilijaribu kuangalia nchi nyingine ndogo kama *Panama,* nchi nyingine wanaita *Sulname* iko Kusini mwa Brazili, na nchi nyingine ya *Guyana.* Nilisema na *Dominica Republic*, na *Mexico* hizi zote zimeanzisha *Dual Nationality* kwa sababu ya kuwasaidia watu wao. Jambo kubwa sana hapa ni kwamba *Dual Nationality* inawawezesha vijana wetu wanaosoma huko nje wanapofanikiwa kurudisha yale mafanikio nyumbani. Sasa kinachotokea kuna Watanzania wengi ambao wameukana uraia wa Tanzania kwa sababu wamepata nafasi ya kuwa raia wa *Canada* kwa mfano, na sheria ya Tanzania inamtaka aukane uraia wa Tanzania, na wanapoukana uraia wa Tanzania ni nani anayefaidi, kwa sababu kama amefika ameamua kuwa raia labda wa Uingereza lakini kwa kitendo cha kufanya hivyo inabidi aukane uraia wake.

Mimi sidhani kama tungekuwa na haki kama Taifa ya kuwafanya watoto wetu na ndugu zetu waukane uraia wao kwa sababu wamekubali kuwa raia wa nchi zingine kutokana na huduma wanazozipata kama huduma za afya, huduma za jamii zingine ambazo raia wa kawaida anayekaa kule anazipata. Na kama mtu amekaa nchi fulani miaka 20 nafikiri tunakubaliana kwamba ana haki ya kupata huduma zinazotokana na ile nchi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema mambo mawili, la kwanza naiomba Wizara ijadiliane na nchi nyingi hasa zile nchi ambazo Watanzania wa kawaida

wanaenda kwa biashara.  Tuwe na utaratibu mzuri zaidi na kukutana na watanzania wa kawaida, na hili Wizara ya Mambo ya Nje, inaweza ikalifanya kwa kuendelea kujadiliana na hawa *partiners* wetu. *(Makofi)*

La pili, ninaomba mjadala huu wa *Dual Nationality* ujadiliwe, na naiomba Wizara ilete Muswada wa Sheria ambao utatoa nafasi sio tu kwa Wabunge lakini na wananchi wengine wadau mbalimbali waweze kuujadili kwa uwazi kabisa. Tuangalie jambo la kwanza maslahi ya nchi yatalindwa vipi na huo Muswada wa Sheria. Kuna nchi zingine wameanzisha kinachoitwa *Multiple Nationality*, sidhani kama ni kitu ambacho Tanzania inakihitaji. Nafikiri kama mtu ameamua kuwa na uraia wa nchi nyingine moja nafikiri imetosha, *Dual Nationality* ni *principle* ambayo nchi nyingi zimeweza kuimudu kwa sababu ina kipengele ambacho lazima tukiangalie kinachohusu usalama wa nchi yetu, na sheria hiyo ije haraka na naomba Wabunge wenzangu itakapofika tuiunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, asante ninashukuru kunipa nafasi hii ya kuniwezesha kuchangia kwa ufupi sana Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, balozi zetu ambazo ziko nje ya nchi ni kioo cha Tanzania, kwa hiyo, nina imani kubwa sana kwamba ni lazima Wizara hii ifanye kazi ili kuhakikisha hiyo dhana ya balozi zilizopo kuwa kioo cha Tanzania inakwenda sambamba na utendaji wa kazi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nipongeze hotuba aliyotoa Waziri mwenye dhamana, pia nitoe pongezi kwa Bunge *Sports Club* na ushindi ulioupata juzi ikiwa ni pamoja na *NSSF.* Hii yote ni hamasa tu, kusema kweli imetufanya tuweze kuanza wiki tukiwa na ari mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mchango mdogo. Ukienda nje utakuta kuna Watanzania wengi ambao vijana wako kule, wengine wanasoma shule wengine wamemaliza kusoma, hawataki kurudi Tanzania, lakini Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika suala la madawa ya kulevya.

Wanaofanya biashara hizo ni pamoja na Watanzania wanaoishi kule nje ambao kwa hakika hili halina ubishi kwa sababu nimelifanyia kazi, nalielewa, nimeishi nje, najua mambo yanavyokwenda katika mtandao huo. Watanzania hawa ambao wanakaa kule nje ya nchi, ni chachu kubwa sana kwa Watanzania hao wanaotoka hapa Tanzania na kwenda kufanya biashara hiyo na kuingiza madawa hapa Tanzania, kitu ambacho sasa kimekuwa ni kero kubwa sana.

Lakini ukienda ndani sana utakuta Watanzania ambao wanaishi kule nje ya nchi, balozi zetu hazina takwimu zao na wanapokwenda wakiwa na matatizo kwenye balozi

zetu kupata msaada hawapati msaada unaostahili. Kwa hiyo, wengi wanaamua kujiingiza katika masuala ya mtandao wa madawa ya kulevya ama kuungana na Watanzania wanaokwenda kule kufanya hiyo biashara ambayo tunasema kwa kweli imeshakuwa ni kero kwa nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, wanajikuta wanajiunga na matajiri wakubwa wanaowafadhili hao wanaoleta madawa. Lakini tunaweza tukafanikiwa kulitatua hilo tu endapo balozi zetu zitawashughulikia ama kwa kuwa karibu na Watanzania wanaoishi nje ambao hawataki kurudi Tanzania na kama wanataka kurudi basi wanasitasita kwa sababu wameishi nje kwa muda mrefu sana.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa natoa ushauri ama tahadhari kwa Wizara hii ya Mambo ya Nje, iwasiliane na hao Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania kule nje, kuhakikisha tunapunguza au tumaliza kabisa hii kero ya dawa za kulevya kwa kuweza kuwa karibu sana na Watanzania walioko kule. Kwa sababu hata ningemwuliza Waziri hapa anieleze ni Watanzania wangapi wanaoishi nje ya nchi, nadhani hatakuwa na takwimu hiyo, kwa sababu nina uhakika Balozi zetu hazifanyi hiyo kazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana mwezi wa 11, nilipata nafasi ya kutembelea nchi kama tano hivi, unaenda South Korea unakuta Watanzania wapo na wanalilia kuja kuwekeza Tanzania, kwa sababu kule ni wafanyabiashara lakini akimwona Mtanzania ambaye ametoka huku, anamwuliza nije kuwekeza katika nini? Yeye anachojua ni kupiga simu tu lakini kitendo cha yeye kutoka South Korea kuja Tanzania, ameshaona sawa sawa na Kituo cha Polisi. Sasa nadhani kazi kubwa ielekezwe kwenye Balozi zetu na Mabalozi wetu walioko huko nje ya nchi, waweze kuwa na takwimu zilizo sahihi za Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Nia ya kuja kuwekeza Tanzania wanayo, waje wawekeze kwa sababu sasa hivi mwendo tunaotaka kwenda nao ni wa kuruka kama ndege, pamoja na uwekezaji ambao tunawakimbilia watu wa nje wakati Watanzania wana uwezo wa kuwekeza lakini hawapati nafasi, tuwape nafasi waje wawekeze.

Mheshimiwa Spika, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri pia imeonesha baadhi ya nchi au Balozi ambazo zimekusanya nchi zaidi ya tano, kwa mfano, Ubalozi wa Japan, unasimamia nchi sita wakati Ubalozi wa Tanzania, unaosimamia *Scandinavian Countries* unasimamia nchi nane. Mimi nimeshangaa sana na inasikitisha kwa sababu hata kama ni kubana matumizi, lakini huwezi ukawa Balozi wa nchi nane ukajua kinachotendeka katika kila nchi. Nadhani kwa makusudi mazima ni jambo la busara kabisa kama litatendeka kuhakikisha kwamba, hizi nchi zinapata Balozi vinginevyo, Balozi anayekuwa kule anachoka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la nyumba, Balozi nyingi unakuta wafanyakazi hawana nyumba, wanaishi nyumba za kupanga. Naishukuru Serikali, imelisimamia hili kwa kujaribu kutafuta nyumba za kununua lakini nyumba ambazo zimenunuliwa zimekuwa ni mbovu sana. Mzungumzaji aliyetangulia, ameeleza Ofisi ya Geneva, jengo la ajabu sana liko pale, ameeleza jinsi ambavyo hatua zimechukuliwa na Serikali na jengo limepatikana. Pamoja na kwamba majengo yanayonunuliwa sasa hivi yananunuliwa kwa gharama kubwa sana, kama jingo, lakini unakuta kwamba jengo ni gofu, kwenda kulitengeneza nadhani linamaliza pesa nyingi sana. Nadhani hatuna budi kuendelea kununua nyumba ili kuweza kurahisisha maisha ya hawa Watanzania, wanaofanya kazi

kwenye Ofisi za Balozi nje ya nchi. Ukienda Uingereza, London pale utakuta wafanyakazi walioko kwenye Ofisi za Ubalozi wengi hawana nyumba, nyumba inakuwa ni ya Balozi labda na msaidizi wake lakini wengine wanapanga.

Mheshimiwa Spika, kwa nini kusiwe na utaratibu wa kuwa na nyumba za wafanyakazi wa kwenye Ofisi za Balozi? Zinunuliwe, yule akihama Mtanzania anayekwenda, anajua kuna nyumba ya Tanzania, pamoja na kwamba itagharimu. Kwenye Hotuba ya Waziri, nilikuwa najaribu kuchambua nione kama kuna utaratibu wa kununua nyumba za wafanyakazi walioko kwenye Ubalozi, sikuona lakini nadhani kwenye fungu atakuwa amebajeti hili kwa sababu ni kitu ambacho kimekuwa ni kero kubwa sana kwa wafanyakazi, wanaofanya kazi kwenye Balozi kuhamishwa nchi kwenda nchi nyingine unaenda unakuta hakuna nyumba. Hii inasababisha sasa hawa maofisa wanaofanya kazi kwenye Balozi, wakati mwingine kuhama bila kuwa na familia zao na kushikilia nyumba ambazo mfanyakazi mwingine anatakiwa aingie. Tunajikuta huyu mfanyakazi anaenda anakaa hotelini, hoteli ambayo ni *very expensive* kwa sababu anaenda na hadhi ya Balozi, hawezi kwenda kukaa kwenye hoteli ya ajabu ajabu. Sasa hili nilikuwa naomba kusema, kweli Serikali ilipe kipaumbele ili kuisaidia Wizara hii kuweza kuwa na nyumba za kutosheleza watumishi wa Wizara hiyo au wa Balozi zetu ambazo ziko huko.

Mheshimiwa Spika, mbali na nyumba za kuishi, lakini nimezungumza kuhusu ofisi. Ofisi nyingi hazina hadhi, Balozi zetu nyingi zina ofisi ambazo hazina hadhi, ni Ubalozi, utakuta Bendera ya Tanzania ipo inapepea tu, lakini uwezo tunaweza tukabana matumizi. Balozi ni mtu ambaye anastahili heshima yake, heshima inaenda na kila kitu, lazima awe na gari ambalo linaenda sambamba na Balozi. Balozi hawezi kuendesha *Corolla* lakini ukienda hapa Kenya jirani zetu, kwenye Ubalozi unakuta mtu anaendesha *Corolla,* sijui kaitoa hapa Tanzania, *Pugu Road* kwenye kampuni za kwetu?

Mheshimiwa Spika, hili suala la ofisi, pamoja na vitendea kazi pia ilikuwa ni kitu ambacho kusema naomba kizingatiwe sana ili kujenga hadhi ya Mabalozi wetu au watumishi wa kwenye Ubalozi wanapokuwa nje wawe na vitu vinavyowaletea hadhi, ambayo *at the end* itakuwa ni kwa ajili ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kutokana na haya, mimi nilikuwa nadhani kwamba, hata bajeti ya Wizara hiyo kusema kweli ukiangalia pilikapilika za Wizara, hata bajeti nadhani ni kidogo sana, kwa sababu shughuli za Wizara hiyo ni nyingi sana, siyo sawa na Wizara nyingine ambazo zinafanyia kazi ofisini. Hawa wanasafiri kila wakati na katika kusafiri lazima fedha zitumike. Sasa nilikuwa nadhani kwenye bajeti hii, Mheshimiwa Waziri Mwenye Dhamana, atakuwa amejipunja kidogo, vinginevyo alitakiwa kwenye bajeti azidishe tu wala haina cha maelezo wala matatizo na sisi Waheshimiwa Wabunge humu ndani, tutaipitisha tu kwa sababu tunajua shughuli za Wizara ni nini.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kujua ni jinsi gani Watanzania wanaoishi nje ya nchi, wanavyoshirikishwa na ofisi zetu za Ubalozi. Nasema hili linaenda sambamba, kwa sababu kama nilivyozungumza, utakuta hawa Watanzania wanaoishi nje kwa sababu

hawashirikishwi na Balozi zetu, ndio tunajikuta hata tunapotafuta tukiwa na tatizo kwamba tujue Mtanzania ametoka wapi, ameenda wapi huko nje ya Tanzania, utakuta inakuwa ni vigumu kujua, kwa sababu hatuna takwimu zinazoonesha kwamba Balozi zetu zinawahusisha namna gani Watanzania walioko kule.

Mheshimiwa Spika, nina hakika kuna nchi zenye Watanzania wengi kama vile London, Uingereza na hasa *Central London,* kuna Watanzania wengi sana, ambao tunawapata siku ambayo Balozi anafurahi na kuitisha sherehe nyumbani kwake na kuwaita Watanzania ndio wanakusanyika pale na hapo ndio wanamjua hata Balozi. Unaweza ukaenda kama Mtanzania, umwulize Balozi ni nani, hajui kwa sababu Balozi hachukui ile jitihada ya kuwatafuta Watanzania ambao wako kule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Balozo ziwasaidie Watanzania walioko kule, wengi wana matatizo hasa wanafunzi, lakini mwanafunzi kwenda kupata msaada kwenye Balozi inakuwa ni sawa na Kituo cha Polisi. Naomba ziwe mstari wa mbele katika kuwasaidia Watanzania walioko huko.

Mheshimiwa Spika, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza ni jinsi gani ambavyo kule nchi ya jirani ya Burundi, Peripahutu *FNL* wameamua kuingia porini. Sasa hivi juhudi au kitu kinachofanyika ni kukamilisha mazungumzo ambayo yataleta shirikisho, ambalo tumeshazungumzia hapa na hatuogopi kuwa na shirikisho, tunachoogopa kuwa na shirikiko ni yatakayofuata baada ya shirikisho kupatikana. Napenda kusema kwamba, kwa sababu hawa watu wameingia msituni, kwa sababu ya matatizo ya ndani ya nchi yao, nina hakika kwamba, sasa hivi mfumuko wa wakimbizi utakuja. Sasa sijui nchi imejizatiti vipi kwa wimbi la wakimbizi ambalo tunalitegemea, kwa sababu hawa watu wamekimbia msituni, kinachofuata sasa wimbi la wakimbizi kurudi tena Tanzania?

Tulikuwa tunasema kwamba, *repatriation* itaendelea ili shirikisho linapokuja basi wakimbizi wawe wameisha, mwezi wa 12 wakimbizi wawe wameshaondoka. Lakini sasa mwelekeo ni kwamba, wakimbizi watazidi kuja kwa sababu hawa wanaume wameamua kwenda msituni, wakitoka kule wakiibuka ni risasi zitatembea na Mrundi akisikia risasi ndio hapo anaanza kukimbia na familia na mizigo yake.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kujua tumejiandaa namna gani, nadhani ni jukumu la Wizara, inaweza ikatoa maelezo mazuri tu kwa sababu Mheshimiwa Waziri anahudhuria vikao hivi. Lakini Waziri pia anaweza akatueleza yeye shirikisho hili Serikali inalionaje, imejiandaa vipi na kama Tanzania tumejiandaa vipi, endapo hali itakamilika kuwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nikizungumzia suala la Watanzania wanaoishi nje na hasa wanafunzi, yamekuwa yakipatikana malalamiko mengi tu kutoka kwa wanafunzi wanaosoma kwenye Vyuo Vikuu huko nje, wakilaumu sana jinsi wasivyosaidiwa na Balozi zetu. Hili nalo nilikuwa napenda kusema kweli wakati Waziri ana-*wind up* au atakapojibu hoja za Waheshimiwa Wabunge hapa, basi ajaribu kuligusia ili tujue ni jinsi gani hawa wanafunzi wanasaidiwa na Balozi zetu zilizopo nje ya nchi, kwa sababu

ukienda India utakuta wanafunzi wanahangaika ovyo. Wanafunzi wanaishi kwa kufanya vibarua, lakini ukienda India hata vibarua hakuna inabidi waondoke wakimbilie nchi nyingine ambazo wakati mwingine wanakuwa na ajira kwa ajili ya wanafunzi kama Uingereza, wana utaratibu huo, pamoja na kwamba maisha kule ni magumu zaidi ya India ilivyo. Watu wa kuwasaidia hawa watu ni Balozi zetu, ndio maana Balozi ziko kule kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania ambao wanaishi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mchango ni mdogo sana lakini nilikuwa napenda nieleze hayo ambayo nina hakika Mheshimiwa Waziri, atayatolea maelezo wakati aki-*wind up*. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana. Mchango wako haukuwa mdogo ilikaribia ugongewe kengele ya pili.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai wa kuweza kurejea tena katika Bunge hili, baada ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana maana ulijishirikisha sana na matatizo yangu na ukanisaidia nikafika pale nilipohitaji. Lakini pia ninamshukuru Katibu wako na wataalamu wake wote, kwa jinsi walivyoshughulikia mawasiliano muhimu kati ya Bunge letu, Wizara ya Afya na hata kuwasiliana nami nilipokuwa kule India, ninawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge, wengi walipofika kule New Delhi walikuja kuniona pale hospitali na mimi nilifarijika kwamba ninao marafiki, nilijisikia sana na waliweza kunieleza habari za nyumbani zinavyoendelea na mimi nikawa mwenye amani sana. Lakini pia mwisho ninawashukuru sana wapiga kura wangu katika Jimbo la Kasulu Magharibi, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wavumilivu sana na mimi sijafika kule Jimboni, lakini wao wamekuwa wakinipigia simu na kunieleza kwamba, hali ni njema, mambo yanaenda vizuri na wao wanaiombea kwa Mwenyezi Mungu, kila wakati nipate ahueni niweze kufika niende tena kule Jimboni na niwaelezeni baadhi ya wapiga kura wangu wengine wamenipigia simu hata nilipokuwa India. Ninawashukuru sana wapiga kura wangu waliofanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba na mimi nichangie kidogo Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Kwanza, ninampongeza yeye Mheshimiwa Waziri, ninawapongeza Manaibu wake; Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu katika Wizara hii, wote ni watu wenye uzoefu wa masuala ya Kimataifa na niseme wote wamebobea katika masuala haya, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kuchangia tu hoja moja juu ya mkataba kati ya Ulaya na Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific. Ninahisi hata kwenye Mkataba huo, nitachangia tu maendeleo yanavyoenda juu ya *negotiations* za *Economic Partnership Agreement.* Ametaja marekebisho yaliyofanyika mwaka jana pale ukurasa

wa 33, lakini yapo marekebisho pia yanayofanywa juu ya *EPAs* zenyewe na ambayo yanaendelea na ambayo Wizara iliombwa kushiriki kikamilifu katika kufanya *review* za *negotiation* zile zinazoendelea. Ulipoanza Mkataba huu mwaka wa 2000, watu wengi walijua sasa Afrika umaskini kwaheri na sisi tulikuwa *encouraged* kwamba, Mkataba ule ulikuwa unalenga masuala makubwa ya maendeleo ya Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific. Nchi zikagawanywa katika makundi mbalimbali, ambayo wanayaita *negotiating configurations,* ya kwetu *SADC*, *EPA* inaitwa *SADC-EU-EPA, Central Africa* wanayo *CEMAC* na kuna *West African Configuration,* kuna nyingine inayoitwa *Eastern and Southern African Configuration,* inayochukua nchi ambazo tunahusiana; Uganda na Kenya na ambazo zimesaini Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna *configuration* inayoitwa *CARICORM* na nyingine ya kule Pacific, zote hizi zinataka kuingia Mkataba na nchi za Jumuiya ya Ulaya. Ninawashukuru ninyi Waheshimiwa Wabunge, kwa kunichagua mimi kuwawakilisha katika Mabunge ya Jumuiya ya Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami niseme nimekuwa najitahidi sana nionekane kwamba ninawawakilisha vizuri, sikwenda tu kukaa na kusikiliza na kwa sababu hiyo mimi nikachaguliwa kama miaka minne iliyopita kuwa, Mwenyekiti wa majadiliano yote ya *Economic Partnership Agreements*. Lakini pili, mwaka juzi nilichaguliwa kusimamia Ripoti Maalum ya Hali ya Umaskini katika nchi za Afrika, Caribbean na Pacific, ambayo imekuwa inaendelea mpaka hivi sasa. Mimi niseme tu kwamba, ninao ufahamu kidogo, kwa *level* ile ambayo ninyi mlinichagua kuhusu masuala haya ya *EPAs*. *Configuration* yetu ina mambo matatu muhimu sana, hii ya *SADC-EU-EPA* moja ni kuwepo kwa Botswana, Lesotho, Namibia na Swaziland *(BNLS)* katika nchi za *SADC* ambao ni Wajumbe hai wa *South African Customs Union*.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, baadhi ya nchi nyingine zilikataa ku-*negotiate* chini ya mpango huu wa *SADC-EU-EPA,* Malawi, Zambia na Zimbabwe wakaja ku-*negotiate* chini ya *ESA*. Lakini wote ni wanachama halisi, wanachama hai wa *SADC* wao wana-*negotiate* chini ya Mpango wa *ESA*. Likaja swali kwamba, nchi moja haiwezi kuwa na mashirikiano ya kiforodha zaidi ya moja na sisi tukawa tumesaini Mkataba *EAC*. Nilisema hapa na nikatoa ushauri kwamba, ni mawili; tutoke kule chini *SADC* tuje kushiriki na nchi nyingine za huku juu, yaani *ESA* au tujiondoe huku juu twende moja kwa moja Kusini, lakini Kusini kuna matatizo kwamba, zile nchi za *BNLS* ziko katika Mpango Maalumu wa *Customs Union* na South Africa. Lakini ya pili ni kuwepo kwa Mkataba Maalumu wa *EU* na South Africa, unaoitwa *Trade and Development Corporation Agreement (TDCA)* ya South Africa, ambayo wamesaini moja kwa moja na *EU* na wame-*negotiate* moja kwa moja na *EU*. Kwa hiyo, wao ndani ya *SADC* ni *observers* wala siyo wajumbe.

Mheshimiwa Spika, nilikupa *brief* kwamba, mwaka jana katika kikao cha *Chief Negotiators* na *Council of Ministers,* kilichofanyika Mjini Helsinki ambako ulinipeleka, watu hawa wa Nchi hizi za Kusini za *BNLS,* wote walikuwa wameshakubali kwamba, sasa wao wanaweza wasi-*negotiate* moja kwa moja chini ya *SADC* na *EPA*. Walikuwa

wanaangalia vifungu chini ya Mkataba wa *TDCA,* ambavyo vinaweza kuwa si vizuri kwao, sasa wana-*negotiate* ili waungane na South Africa kule Kusini.

Kwa mpango huu na kwa mpango wa *South African Custom Union* kuendelea, maana yake ni kwamba, *SADC-EPA* uwezo wake ungekuwa *watered down* na nguvu isingekuwepo kwa hiyo nchi nyingine Angola, Msumbiji na Tanzania, tungebaki nje ya mpango mzima huu wa *Tariff Elimination,* ambao South Africa imeingia na ambao una-*combine* kitu kinachoitwa *Tariff Elimination Commitment* kwa South Africa, ambayo ni *substantially all trade.* Maana yake ni kwamba, biashara zote zitakuwa *liberalized* kwa kiwango cha asilimia 86 na kwa bidhaa zonazouzwa *EU.*

Mheshimiwa Spika, sasa hili likawa limeiweka Tanzania katika hali ngumu kwamba, Tanzania sasa lazima iangalie njia nyingine vinginevyo, haitakuwa na uwezo moja kwa moja wa kuingia Mkataba na *EU* na hilo limekuwa tatizo. *Recent developments* za *negotiation* kuzungumzwa chini ya *East African Community,* zilikuwa ndio hasa zinatufaa na ambazo zingetuweka katika *footing* nzuri vinginevyo, sisi itabidi tubaki chini ya mpango wa *Everything But Arms (EBA)*, ambao ndio mpango tuliokuwa nao miaka yote, sisi hatuna kitu cha *reciprocate* kwa *EU* ili tupeleke kule na wao walete huku kwetu.

Mheshimiwa Spika, cha msingi ambacho watu wetu lazima watueleze ni kwamba, wanajua gharama za kuingia *Economic Partnership Agreement?* Tukiwa katika *SADC,* maana moja kwa moja hatutakuwa *involved*, Mpango wa *EAC* ungetupeleka moja kwa moja tunge-*negotiate*, wao *EU* hawautaki kwa sababu *ESA,* itakuwa haina nguvu kama Kenya itaondoka, Uganda itaondoka na Tanzania ndio itakuwa imekaa na hawa, sasa itaanza kuchukua baadhi ya *members* wa *ESA,* Rwanda na Burundi. Nchi zinazo-*pioneer ESA* ni Mauritius na Seychelles, wakisaidiana na Kenya, ndio wanao-*pioneer* majadiliano ya *ESA* kuifanya iwe na nguvu.

Mheshimiwa Spika, yapo masuala muhimu na nyeti, ambayo tunahitaji sisi kukaa pamoja na kuyajadili vizuri zaidi na siyo kuelewa mambo kirahisi. Mkataba huu ni wa maana sana kwa maendeleo katika nchi hii. Mkataba huu ni wa maana kwa sababu yapo mambo manne ambayo yote yana gharama, tunatakiwa tuyafanye katika kuingia hizi *EPAs,* maana yake ni *free trade agreements.* Ndiyo tunajenga hiyo katika mpango mzima wa biashara huria. Maana yake ni kwamba, biashara itakuwa *liberalized* kwa kiwango kikubwa, *ESA* wana-*liberalize* kwa kiwango cha asilimia 85. Sasa hivi utaratibu wetu kwa kweli mpaka hivi sasa ni lazima kukaa tena na wenzetu wa *East African Community,* tujaribu kujenga hoja ya kwenda kuzungumza na *EU*. Wao hawawezi kusema nendeni kwa sababu sasa wamefika mbali na *ESA* katika *negotiation* na wanaona kama *ESA* itavunjika, maana yake wataanza upya na *EAC.*

Mheshimiwa Spika, yako maeneo manne ambayo ningeweza kusema katika mpango mzima *economic adjustment.* Moja ni *physical adjustment,* gharama tutakayoingia kwa ku-*adjust* kukubali hii *liberalization program.* Pili ni *trade facilitation* na *export diversification.* Tatu ni *employment and production adjustment* ambayo lazima itafanywa ili katika mchakato mzima wa *trade creation* na *trade diversion,* lazima

utaingia. Mchakato unaofuata ni ule wa *skills development and productivity enhancement,* ambayo sisi ndiyo tunazungumzia hatuna uwezo kama hao wenzetu.

Sasa tunahitaji uwezo lazima tuujenge sisi wenyewe, tusisubiri wengine watujengee. Kama hatuna leo tunaingia kwenye mashirikiano ya namna hii ni dhahiri kwamba ni lazima tujisukume twende huko. Sasa ninayo maombi kwa Wizara hii; moja, ninaomba Wizara hii iandae semina ya Wabunge waeleweshwe kisawasawa haya mambo ya *EPAs* yanavyoenda, maana tulishakubaliana kwamba, semina nzuri itaandaliwa na haya mambo yaweze kuzungumzwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, la pili, zile Kamati mbili zinazofanya kazi ya kuangalia masuala ya biashara; Kamati ya Mambo ya Nje na Kamati ya Biashara na Uwekezaji, walishaambiwa kwamba, sisi wawakilishi nchi za nje kwenye masuala ya biashara, tunatakiwa tutoe ripoti kwenye Kamati hizo. Niliwahi kuitwa mara moja nikaenda kule nikakuta wajumbe wane au watano tu. Sasa ni vizuri kama mkifanya mpango, Kamati hiyo iniite mimi niko tayari kuzungumza na baadhi ya Wabunge wa Kamati hizi, niko tayari kuzungumza nanyi na kuwaelewesha kinachoendelea hivi sasa, maana hapa muda hautoshi na yako mengi na mimi naomba ushirikiano. Serikali yetu tumeandikiwa barua nyingi sana wakiomba tushirikiane nao na yako mengi ambayo tunayajua kwa *level* yetu siyo ya Kiserikali, ambayo yangeweza kusaidia Serikali yetu, maana *we all have an interest in the development of this country.* Hatuwezi kuiacha tu iende hivyo, lakini haya tunayojua basi yasaidie katika maendeleo ya nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja mia kwa mia na mimi ninamtakia kheri Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote. Asante sana. *(Makofi)*

Siwezi kuwalaumu lakini bajeti ni ndogo.

**SPIKA:** Asante sana. Waheshimiwa Wabunge, mtaona orodha niliyoisoma awali ninaibadili badili kidogo kwanza, imo ndani ya mamlaka yangu lakini pia napenda kuchanganya jinsia.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, asante sana na ninashukuru kwa kunipa nafasi hii, kama kawaida na mimi nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Membe, kazi nzuri sana anayoifanya na pia nitoe heshima kwa aliyekuwa kabla yake, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro, kwa kazi nzuri aliyokuwa ameifanya katika Wizara hii. Aidha, niwapongeze pia Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kwa kweli wamekuwa wakitupa ushirikiano sana tangu mwanzo. Mimi niko kwenye Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, lakini vilevile nisisahau kumpongeza Katibu Mkuu na Watendaji wote Wakuu wa Wizara hiyo na hususan Balozi Sanga, huyu ninamtaja maalum kwa sababu ni mtu ambaye pamoja na wadhifa wake, ukimkuta hata kwenye *corridors* za Wizara ile unaweza ukamsimamisha na atakupa maelezo kana kwamba, hana shughuli nyingine yoyote, kwa hiyo, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kuwapongeza wanawake wa Tanzania, maana yake husemi akina mama, akina mama wako majumbani, nao ni Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Anna Tibaijuka, Mheshimiwa Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Rosebud Kurwijila, Mheshimiwa Amina Salum Ali na Mheshimiwa Liberata Mulamula, kwa nafasi kubwa ambazo wamezipata ambazo wanaiwakilisha nchi yetu na hususan jamii ya wanawake wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nipongeze Mabalozi wetu wote wa Nchi za Nje, ambao wako hapa Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa wale ambao mnahudhuria dhifa mbalimbali, ni wazi kabisa bila kificho wanashiriki mambo mbalimbali hata ya kwetu Kitaifa ya michango mbalimbali na shughuli nyingine. Ninawashukuru sana Mabalozi hawa. Lakini vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri na Ofisi yake, kwa kazi kubwa na ngumu wanayoifanya, kwenye bajeti ndogo sana, yameshaelezwa na wenzangu nadhani yamesemwa pia na wachangiaji kutoka Upinzani na sehemu nyingine kwamba, bajeti ni ndogo sana lakini kwa kweli kazi zinaendelea kwenda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, niko Kamati hii watu watashangaa kwa nini nimeamua kuchangia lakini sababu kubwa ni moja tu, ingawa nina vipengele viwili, vitatu, nitakavyoongezea. Inasikitisha pale ambapo Mtanzania anaona masuala ya Mambo ya Nchi za Nje ni ya watu fulani fulani, hii inadhihirisha kwamba, inapokuja masuala ya Mambo ya Nchi za Nje, utaona watu wengi wanatoweka, inabaki dhana labda hii ni Wizara ya fulani, kwa utafiti wangu wa muda mfupi ni kwamba, sekta yenyewe ilivyokaa, siwezi kuwalaumu kwani bajeti ni ndogo.

Wamekuwa hawawezi kuchangamana sana kwa jinsi inavyotakiwa kuweza kutoa taarifa mbalimbali hata humu ndani ya Bunge lako Tukufu ni taarifa nyingi sana kama leo kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, ametoa maelezo mengi sana. Sisi kwenye Kamati ni kweli kabisa tunapewa taarifa zote, lakini kwa wengine inakuwa kwamba, hizi taarifa hawazipati ambazo ni muhimu kiasi kwamba, imefikia mahali watu wanaona mambo ya nchi za nje ni mambo ya nchi za nje na kuona, kwanza mimi sina nauli ya kwenda huko, hata Kiingereza sikijui, wala sifikirii kwenda na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, tunakokwenda katika Karne hii ya 21, nadhani kuna haja kabisa haya masuala ya nchi za nje yakasogezwa yakarudishwa nyumbani. Tunazungumzia Mabalozi kutangaza Tanzania nchi za nje basi na wenyewe watangaze zile habari huku Tanzania tujue kinachoendelea, watu wengi wanakosa fursa. Sisi ambao tunatembelea nje ya nchi, ambao Mungu ametujalia, unakutana na fursa mbalimbali ambazo zingeweza kutukwamua kiuchumi. Sasa hili ndiyo nalisemea, kwa kweli ninaomba sana sana Wizara hii pamoja na bajeti pungufu, lakini mjitahidi sana hizi taarifa au kwa kushirikiana na Sekta tofauti tofauti au *NGOs* mbalimbali au kwa njia mbalimbali kama makongamano na sehemu mbalimbali ili angalau Watanzania wengi wajue sehemu ya masuala ya nchi za nje yanawahusu wote.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nichukue fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Bernard K. Membe, Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Uongozi uliohusika

katika uteuzi uliofanyika hivi karibuni wa Mabalozi. Nadhani mwaka jana nilisema kwa uchungu kidogo, katika mchango wangu kuhusu sura ya Mabalozi na Ubalozi, lakini nashukuru sana kwa kazi ambayo mmeifanya, japo yapo mapungufu ya hapa na pale, lakini Rome haikujengwa siku moja. Bado tunaona sura za Mabalozi wenye uzoefu hasa tukizingatia *Economic Diplomacy* ambayo ndiyo sasa hivi inahitaji kuonekana kwenye Balozi zetu. Lakini bado utaona wanapitapita pale Wizarani, najua Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, kwa umakini wake siyo kwamba ameacha na ameishia hapo, bali ilikuwa mwanzo wa mchakato mzito. Namwomba pia kwamba na Mabalozi Wanawake angeweza kuwaangalia zaidi, kwa sababu kama wenzangu walivyosema, wapo wenye uwezo kwa kweli bado ile sura haijajionesha kwa udhahiri japo umejitahidi kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninapenda nipongeze sana uteuzi wa Mkurugenzi wa *AICC*, Bwana Kaaya. Kwa muda mrefu sana Kamati tulikuwa tunadai ateuliwe Mkurugenzi kwa sababu alikuwa anakaimu kwa muda mrefu, tunashukuru kwamba, hiyo imefanyika chini ya bodi ile mahiri.

Lakini vilevile nichukue fursa hii kuipongeza sana hii Taasisi ya *AICC*, kwani mimi ambaye nilikuwa katika Bunge la Afrika Mashariki, ambalo lipo mahali pale, kwa kweli ninapokwenda siku hadi siku ninaona mabadiliko. Nimeona hapa takwimu 2006/2007, wamekuwa na mikutano 120 na wameweza kuingiza shilingi bilioni nne na kadhalika. Kwa kweli mimi nasema kwa hili, wanahitaji pongezi.

Lakini basi pamoja na pongezi, naona kuna haja japo wamesema wanakusudia kujenga kituo kingine ni lini? Maana yake muda unazidi kwenda na Ngurdoto inaanza kuwapiku sasa hivi. Sisemi kwamba, Ngurdoto ni mbaya, hii ni sehemu ya Mtanzania mwenzetu, lakini ili tuweze kuwa na ile sura, basi twende kwa kasi. Hali kadhalika, pale pale tunaweza tukatangaza utalii na tunaweza tukakitumia kile kituo kwa kutangaza nchi za nje hapa kwetu Tanzania, yaani tukawa tunafanya maonesho ya mara moja moja, tukawa tunakwenda pale.

Kwa ujumla, kile kituo bado kinahitaji kazi kubwa, sijaona hapa sasa hivi kwa haraka aidha, sikuweza kukumbuka, lakini naona ni vyema tukaipa msukumo na Wizara ikaangalia kwa jicho la ziada ili kuhakikisha kwamba, zile *facilities* zinaendana na wakati wenyewe.

Mji wa Arusha umekuwa ni mji wa msongamano sasa hivi, hata wanapofika Marais wawili au watatu, inakuwa ni shughuli ndani ya mji ule. Hebu twende na mawazo ya kwenda na wakati, tufikirie kupanuka na kwenda sehemu za nje kidogo.

Yapo mengi ambayo yamesemwa kuhusu Ofisi zetu za Ubalozi nje ya nchi, nisingependa kuyarudia kwa sababu hata Kanuni haziruhusu kurudiarudia yaliyosemwa. Naomba nisisitize na mwaka jana tulisema tena, nichukulie mfano wa nchi moja ya Nigeria. Ubalozi wetu wa Abuja pale ndiyo unaowakilisha nchi 13 za Afrika ya Magharibi, yaani West Africa. Sasa nimeangalia hata hapa kwenye bajeti yao ni shilingi

milioni 573. Kwa kweli nikifikiria tunazungumzia kuitangaza Tanzania na rasilimali zake, itawezekana kwa kiwango hicho na ukizingatia ni nchi 13? Mimi naona kuna haja bado ya kutafakari, *let us walk on our talk,* yaani tutende yale tunayoyazungumza. Tuone ni kwa jinsi gani hasa pale ambapo tunajua tunaweza tukapata manufaa Fulani, najua West Africa, pamoja na mambo mengine, akini kiuchumi pia tungeweza kufaidika sana kutoka kwao.

Tanzania katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa nimeona ni moja ya nchi 31 maskini, lakini mimi nasema kwa viwango vya kimataifa na vilivyowekwa, naiomba Wizara kwa makusudi mazima, ijaribu ku-*link up seriously* hata kama siyo na Wizara, hata na Taasisi au hata na *commission.* Mbona kuna vituo vingi ambavyo havipo, ambavyo sijui kama vimetathminiwa, kimoja kikiwa najua mtashangaa lakini Kilindi. Kilindi tuna mbuga ya wanyama, ambayo haina hata maelezo, hadi sasa hakuna mtu ambaye amefika pale kuangalia.

Wanyama ni wengi kwa sababu ya vurugu za kule wanakotoka upande wa pili, kutoka Simanjiro, lakini pale kwangu wamejaa na watu wanaingia wkuwinda na kutoka. Hii ni mbuga nzuri, ambayo ingepewa wawekezaji wa uhakika na ukizingatia kwamba, kuna mito ambayo inamwaga maji wakati wote, ingekuwa nzuri zaidi, lakini sidhani kama mna takwimu zake?

Misitu yake, madini na tuna milima, ambayo ina vijito vya ajabu, yaani ni milima ya kihistoria lakini hakuna anayejua, wala hakuna anayetafuta. Kwa hiyo, mimi naiomba sana Wizara kwamba, hii ni sehemu moja tu labda ziko sehemu nyingine nyingi, hebu jaribuni kutafuta kwa kutumia aidha ni watu gani mtawatumia kwenye Wizara zenu ili tuwe na tathmini kamili ya yale tuliyonayo ili tunapouza nje, tuuze tukiwa na uhakika.

Lakini vilevile niwapongeze sana Wizara na Serikali kwa ujumla katika ushiriki wetu katika migogo mbalimbali. Tanzania tunafahamika katika hilo, lakini naomba sana niwapongeze, nimeona pale katika ukurasa wa 12 – 14, Mheshimiwa Waziri, umeweza kueleza kuhusu migogoro mbalimbali ya nchi mbalimbali ambayo na sisi tumeshiriki.

Nakupongeza Mheshimiwa Waziri, ila tu nisisitize moja kwamba, alikuja hapa Mwakilishi wa Palestina, aliweza kuongea na Kamati kwa uchungu sana, akionesha ya kwamba, haoni ule msukumo kama ambavyo angestahili, wa sisi kuweza kushiriki katika mgogoro huu wa Mashariki ya Kati. Labda na hili ulitazame kwa jicho lingine na pengine kama Wizara mtajitahidi ili angalau muweke sura ambapo na wao wataona kwamba, kwa kweli tunashiriki katika hayo.

Lakini pia ninaomba taarifa zaidi hata kama ni semina, Mheshimiwa Waziri, kwa hapa unaona ratiba ilivyokuwa imejaa, lakini nadhani wakati mwingine hata tukiwa Dar es Salaam, unaweza ukapanga semina kwa ajili ya Wabunge wote, halafu uweze kutupatia hizi taarifa kwa kina ili watu wote wazielewe, kwa sababu sisi tukizielewa ndiyo wawakilishi wa watu na watu watakuwa wameelewa.

Mwaka jana tulizungumzia sana tatizo la *Visa* hasa Ubalozi wa Uingereza kwamba, watu wanasumbuliwa sana na kadhalika. Kamati yetu iliweza kutembelea

Ubalozi wa Uingereza na ninafurahi na ninawapongeza Ubalozi wa Uingereza, sasa hivi ule uliokuwa mlolongo na mambo mengine ya mahojiano na kadhalika, yamekwisha na watu wetu wanapata *Visa* bila usumbufu ambao tulikuwa tumeuzungumzia. Kwa hiyo, nawapongeza sana ndugu zangu wa Ubalozi wa Uingereza kwa sababu pia wapo hapa.

Asubuhi ya leo Naibu Waziri, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, alijibu swali kuhusu *consulate*, nilileta kwenu maombi Mheshimiwa Waziri, nadhani utakuwa umeyaona, ya mtu ambaye amejitokeza kutoka Malta, ambaye anakuja mara nyingi Tanzania na anawafahamu wawekezaji wengi. Nilileta maombi haya kwenu, akisema yeye yuko tayari kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Tanzania, kuwatafuta watu hao. Najua maombi hayo yanafanyiwa kazi lakini ili kuonesha basi tunafanya kitu, naomba kasi kidogo kwenye maamuzi.

Lingine ni kwamba, mara ya mwisho, tulizungumzia Ubalozi wa India, kwa sababu wagonjwa wetu wanakwenda wengi, tupate aidha *Senior Officer or Minister Plenipotentiary*, ambaye atashughulika na masuala ya afya tu ili kujua bili zetu. Hivi juzi nilikwenda pale nikaona bili zimeongezeka sana. Sasa hii ni kwa sababu wanapokwenda pale hatuna mtaalamu wetu, ambaye kazi yake ni kuangalia bili zinakwendaje, kwa hiyo, tunaweza tukapewa bili yoyote kwa mtu yoyote bila kuweza kufahamu. Hili tuliliomba mwaka jana na ninaomba nilisisitizie tena ni muhimu ili zile bili ziendane na ukweli na kile ambacho kimepelekwa na hali kadhalika tutakuwa tunapeleka wahusika kwa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakaribia kumaliza lakini suala la Itifaki ni kwamba, siyo ya nje tu na hata itifaki ya ndani. Huwa tunapata utata sana, wanapokuja wageni wa nje kwenye Wilaya zetu huko au hawa Viongozi Wakuu wa Serikali, wakifika unakuta mnakanyagana, hamjui nani aende wapi na vipi, mwishoni mnaona kama mmedhalilishwa kumbe ni kukosa kujua itifaki. Naomba Wizara hii, ifanye utaratibu hata humu ndani, kuweza kupitisha pengine semina kwenye Mikoa halafu Mikoa itaita Wilaya zake na kutoa semina hizo ili kuelewa itifaki katika Wilaya zetu na chini zaidi hususan wanapokuja Viongozi wengine.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, niko kwenye Kamati hii, yangu yalikuwa zaidi ni pongezi lakini kukumbusha hayo mawili, matatu na zaidi kusisitiza uhusiano wa Wizara hii na Watanzania wote wajue, wao pia ni sehemu ya Wizara hii.

Kwa kuhitimisha naomba niunge mkono hoja kwa kusema bajeti ni ndogo sana kulingana na majukumu yaliyopo.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ninaomba sana hata kama kutakuwa na *reallocation* baadaye na kadhalika, basi Wizara hii iweze kufikiriwa ili iweze kutimiza majukumu yake na kuleta ile sura ya Tanzania huko tuendako.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii nikiomba na Wabunge wengine, kwa niaba ya Kamati muunge mkono. Asanteni.

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo na msemaji wetu wa mchana huu atakuwa ni Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa msemaji wa mwisho kwa mchana huu. Kabla ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, niwapongeze vilevile Naibu Mawaziri wawili katika Wizara hii na vilevile niwapongeze watumishi wote, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje. Kazi wanayofanya ni kubwa lakini niseme tu kwamba, watumishi katika Wizara hii hawatoshi kukidhi haja na matakwa mazima ya kuweza kutekeleza kwa ufanisi wa shughuli zote za Wizara.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kusema ninavyofahamu au inavyoeleweka imo ndani ya Serikali, kwa maana ya kuzitambua hizi Wizara kwa kusema kwamba, hii ni *key Ministry* na hii *non-key Ministry*. Ubaguzi huu siyo mzuri, pamoja na kwamba, Wizara zote ni sawa lakini zinatofautiana majukumu, lakini sasa tusizipe majina au tukazibagua tukasema hizi ni *key Ministries* na hizi ni *non-key Ministries*. Hata hivyo, wafanyakazi wa Wizara hizi wanaweza wakakata tamaa kwa kuonekana kama wao siyo muhimu katika Wizara ile kwa kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, niseme wazi kwamba, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, kwa mtazamo ulivyo, inaonekana kama *non-key Ministry* na hii siyo haki. Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, ukilinganisha na nchi zote duniani ni Wizara ambayo ina umuhimu mkubwa katika kutekeleza majukumu yake. Wizara hii inaweza ikaiweka nchi yetu katika hali nzuri zaidi na ikafanikisha mafanikio ya Wizara nyingine zote ambazo zipo katika Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa sitaki niseme kwamba, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ni *key Ministry* au ni *non-key Ministry,* nitakuwa narudia katika ubaguzi uleule. Lakini nasema hii Wizara ni muhimu na tuache kusema kwamba, *it is a non-key Ministry* kwa sababu historia inasema kwamba, hii Wizara ilianza kama Idara sasa haimaanishi kwamba, iwe ni Idara. Sasa hivi ni Wizara kutokana na kukua kwa nchi yetu na majukumu ambayo Wizara hii imepewa na hapa tulipofika sasa hivi kuonekana kwamba hii Wizara labda siyo *key Ministry*.

Kigezo kimojawapo cha kuonekana kwamba hii Wizara labda inaonekana siyo muhimu ni kutokana na bajeti iliyotengewa. Bajeti ya Wizara hii ni shilingi bilioni 59 za Kitanzania. Matumizi makubwa ya Wizara hii ni fedha za kigeni, hatimaye unachukua hizi shilingi bilioni 59 unazibadilisha kuwa ni fedha za kigeni, tutapata hapa dola milioni 37. Sasa basi hizi zingekuwa ni dola milioni 59, afadhali kungekuwa na mantiki kidogo ya kusema kwamba, hizi pesa kidogo zinaweza zikafanya kazi yake na tunaelewa mfumuko wa uchumi duniani na kadhalika, sarafu yetu kupungua thamani, hatimaye kila siku shilingi inapungua. Itafika mahali Wizara hii itakuwa inapata dola milioni 30 na shughuli zake zote takribani 90% ni matumizi ya fedha za kigeni, kwa sababu Balozi zetu zote huko nje zinatumia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kinachonisikitisha ni kwamba, shilingi bilioni 47.5 ni matumizi ya kawaida, lakini katika hizi shilingi bilioni 47 kuna zile fedha

wanazotegemea kukusanya kama maduhuli kutoka Balozi mbalimbali, tayari zimeshaunganishwa hapa katika shilingi bilioni 47. Kwa hiyo, hatuwezi tukasema kwamba ni shilingi bilioni 47.5, inabidi utoe zile shilingi bilioni 9, kwa sababu bado hazijakusanywa. Hata hivyo, tunafahamu kwamba, bajeti hizi ni *cash budget,* zitakapopatikana ndipo zitakapotolewa, lakini sasa kwa nini tunajumuisha maduhuli yale ya shilingi bilioni 9 iwe ni miongoni mwa bajeti ya Wizara hii wakati hawajakusanya? Wanaweza wakakusanya shilling bilioni 9 na wanaweza wasikusanye kwa hiyo, ni kutoitendea haki Wizara kwa kuunganisha shilingi bilioni 9 kama maduhuli ya kukusanywa huko nje ya nchi, hatimaye iunganishwe katika bajeti.

Lingine ambalo mimi sikubaliani nalo ni kwamba, shilingi bilioni 5 ya Mkutano wa Sulivan, kuingizwa kama Bajeti ya Wizara hii wakati Mkutano ule utanufaisha Wizara nyingi na wananchi wengi na wadau wengi sana. Inakuwaje sasa inakuwa ni Bajeti ya Wizara? Kwa kweli pia tutakuwa hatuitendei haki, kwa sababu Wizara kazi yake ni kuandaa mkutano tu na gharama zake ni shilingi bilioni 5, hatimaye kitakachopatikana kitakwenda Hazina katika matokeo ya mkutano ule, kama tutafanikiwa katika Mkutano ule hili ni suala lingine.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna shilingi bilioni mbili kwa ajili ya mchakato wa *APRM* na shilingi bilioni mbili nyingine ni kwa ajili ya uanzishwaji ya Makao Makuu ya Mahakama ya Haki za Binadamu, bado zimeingizwa katika bajeti ya Wizara. Kwa nini hii miradi isiwe ni miradi ya Serikali? Hazina wenyewe wa-*finance* kwa ajili ya kutengeneza hizi Mahakama na miradi hii mingine na Mkutano wa Silvan, hatimaye at *least* hizi pesa nyingine shilling ibilioni 5, bilioni 2 na bilioni 2 nyingine kukawa na shilingi bilioni 9, ambazo zitakwenda *direct* katika Wizara kwa ajili ya kushughulikia matatizo mbalimbali yaliyokuwepo katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, bila shaka wewe unatembea katika nchi mbalimbali na unapokewa na Mabalozi mbalimbali, nina uhakika hata Waheshimiwa Wabunge wanaotembelea katika Balozi zetu, malalamiko makubwa ya Balozi zetu ni kwamba, bajeti haitoshi na ukitazama ni kweli. Sisi hapa shilingi 3,000 au 4,000, utakula chakula cha asubuhi, mchana na jioni, lakini huwezi ukatumia dola 5 ukiwa kwenye nchi kama Japan hata kwa *breakfast* haitoshi. Sasa hivi tuna-*justify* kitu gani katika suala zima la bajeti ya hii Wizara? Halafu tunaipa majukumu mazito Wizara hii ili iweze ikatuweka mahali pazuri duniani, kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja katika suala zima la utalii. Wizara ya Maliasili na Utalii, inapopeleka makabrasha yake kwenye Balozi kwa ajili ya kutangaza utalii na Balozi zile wakiitisha mikutano ya Wadau kutangaza utalii ni mkutano mmoja tu zile *pamphlets* zote zinakuwa zimekwisha ambazo ni za *quality,* zenye rangi na zenye kuvutia. Baada ya hapo Wizara haipeleki tena, kinachofanyika Balozi wanatoa *photocopy* ya zile *pamphlets* zinakuwa tena siyo za rangi bali zinakuwa ni za *black and white,* hata yule mtalii akitaka kuja haoni kivutio halisi cha rangi na hali halisi ya lile eneo ambalo linatangazwa.

Kwa hiyo, kwa kweli Mabalozi wetu, wanafanya kazi ngumu sana, pamoja na kwamba haya mengine yamekwisha zungumzwa kwenye Taarifa ya Kamati,

Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Mimi nisisitizie tu kwamba, hizi Balozi ambazo zina nchi nchi nyingi kama Japan na *Scandinavian Countries,* nchi kama Japan Balozi mmoja anasimamia nchi sita, lakini ndani ya hizo nchi sita kuna nchi moja inaitwa Australia ni *continent* nzima ile ambayo hatuna Balizi; sasa inakuwaje? Ukichukua ukubwa wa Australia na ukubwa wa Japan ni vitu viwili tofauti.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nisisitize tu kwamba, hii Wizara lazima itazamwe upya katika suala zima la bajeti ili iweze kukidhi haja ya shughuli ambazo wamewekewa hawa Mabalozi na hata ikibidi bajeti ya Wizara hii sasa hivi iwe ni kwa fedha za kigeni ili iweze kukidhi haja halisi, lakini siyo kwa fedha za Tanzania wakati kila siku zinapungua thamani.

Mheshimiwa Spika, lingine limeshazungumzwa hapa ni kuhusu *Visa* katika Balozi mbalimbali wanazotoa kwa wananchi wetu. Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, ameshazungumzia suala la Ubalozi wa Uingereza, lakini pia kuna Balozi nyingine bado zinaleta usumbufu.

Nisisitize tu kwa mfano, Ubalozi wa Uingereza wanatoza *Visa* karibu shilingi 150,000 lakini baada ya hapo unaweza ukanyimwa *Visa* ile ni haki yao nchi ya Uingereza kukunyima *Visa* kukubali au kukataa, mimi sina tatizo na hilo lakini sasa unamchukulia mtua ambaye amekaa karibu miezi sita au saba anachangachanga apate hela ya *Visa* shilingi 150,000, anaipeleka Ubalozi wakimkatalia na ile fedha hairudi. Kwa kweli hili ni tatizo sisemi tu Uingereza.

Nimetoa mfano wa Uingereza, lakini ziko Balozi nyingine. Fedha za *Visa* zikishaingia kule wakikukatalia, hazirudi tena; hivi kweli Ubalozi wa Uingereza una shida ya shilingi 150,000?

Sidhani, mrudishieni yule mtu amechanga, mwambie bwana tumekukatalia *Visa* lakini hela yako hii chukua, basi ibaki zile fedha labda ni za gharama za makaratasi na kadhalika, ambazo ni asilimia ndogo sana. Lakini wanazichukua zote, anaondoka pale *Visa* wamemnyima na hela imepotea ni sawasawa na kuchukua hela na kuitumbukiza chooni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Balozi wa Uingereza yupo, mimi naiomba tu Balozi hiyo kupitia kwako, Mheshimiwa Waziri, mkae mwone jinsi mtavyotumia utaratibu wa kurudisha zile fedha za *Visa* kwa wale wanaokataliwa katika Balozi zile. Nitafurahi sana pamoja na Balozi nyingine ambazo wanafanya utararibu huo.

Mheshimiwa Spika, mengi yamekwisha zungumzwa kwa hiyo, sina haja ya kurudia, pamoja na hivyo muda uliobaki ni mdogo. Lakini niseme mara ya mwisho kwamba, ndugu zangu wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, msikate tama, sisi tutasimama na Mheshimiwa Waziri kuwatetea na hatimaye tuone tunafanikisha kuwa na bajeti nzuri katika hii Wizara, majukumu ya Wizara hii yaweze kutekelezwa vizuri na tuweze kuona kama kweli Wizara hii ni kioo cha Tanzania huko nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautuwezeshi kumpa fursa ya kuongea yeyote anayefuata lakini niseme tu jioni tutakuwa na wachangiaji wawili; ataanza Mheshimiwa Charles M. Kajege, halafu atahitimisha Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na baada ya hapo utaendelea utaratibu wa kawaida; Naibu Mawaziri watajibu sehemu za hoja zinazowahusu na mwisho mtoa hoja ataitwa, kuweza kujibu zile hoja na tutaendelea na utaratibu wa Kanuni.

Kwa sasa hivi nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11:00 jioni.

*(Saa 6.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika orodha yangu hapa kwa mchana huu, tuna mchangiaji mmoja tu, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Awali ya yote, naomba kuungana na wenzangu, kumpongeza Waziri, Manaibu wake na Katibu Mkuu, pamoja na Watumishi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutimiza majukumu yao hasa kuitangaza nchi yetu na vilevile kuwahudumia Watanzania hasa walioko kule nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza niende kwenye Kitabu cha *Revenue.* Katika Kitabu cha *Revenue,* Wizara ilikuwa inakusanya kama shilingi bilioni 9 kutokana na wageni, *Visa* na kadhalika, lakini mwaka huu pesa hizi zimepungua. Kwa hiyo, napata mashaka kidogo kuona kwamba, kama idadi ya gharama ya makusanyo ya *Visa* zitaongezeka kutokana na idadi ya watu, lakini mapato yanapungua. Labda wangetusaidia hii kazi ya diplomasia ya kibiashara na kiuchumi; je, imekwama au vipi, maana kama inaendelea vizuri mapato yangekuwa yanaongezeka? Sasa ukitazama Kitabu chao cha *Revenue,* mapato yao yatakuwa yamepungua kwa wastani wa shilingi nusu bilioni kama hivi mwaka huu. Hilo lilikuwa ni jambo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, Rais wa Jamhuri kabla hajakuwa Rais, alipokuwa Waziri wa Mambo ya Nje, moja ambalo alipata tabu sana lilikuwa suala la kisiasa la Zanzibar, wakati huo alikuwa akijibu maswali mengi sana. Kwa bahati nzuri katika kipindi hiki sasa tumekuwa shwari kwa kiasi fulani, wakati mazungumzo yanaendelea. Kutokana na hali halisi ilivyo hivi sasa, bado ufumbuzi wa jambo hili haujapatikana. Nilikuwa nataka kuishauri Serikali ijue kwamba, kama wenyewe ndani

tuna matatizo hatujayamaliza, tunakosa ile nguvu na ari ya kuweza kuwasuluhisha wenzetu. Kwa hivyo ni jambo la busara sana tukatumia hekima zetu zote, tukalimaliza hili tatizo kwa haraka iwezekanavyo ili hii kazi nzuri tunayoifanya ya usuluhishi na wenzetu wa nje iwe na nguvu kwamba, sisi wenyewe ni safi. Huwezi kumwambia mwenzako nyumba yake ni chafu, kumbe ya kwako ni chafu zaidi na kwamba una uwezo wa kutatua lakini huwezi kutatua. Kwa hiyo, inakuwa chafu zaidi kwa sababu uwezo wa kutatua unao lakini huwezi kutatua. Mimi nafikiri hili ni jambo ambalo nilitaka niliseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni suala la Burundi na Rwanda. Wenzetu hawa tumewaingiza katika *East African Community* na sasa hivi tunazungumzia suala zima la Shirikisho la Kisiasa. Wenzetu wa *European Union,* wamekuwa wakiweka vigezo vya nchi kujiunga na Jumuiya yao na kama hujatimiza hivyo vigezo, basi hupati nafasi ya kuingia. Sasa sina hakika kama Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, tunavyo vigezo vya kuwaambia wanachama hasa waingie. Maana yake leo kuna wenzetu baada ya kuingia ndiyo kwanza migogoro inaanza, migogoro hiyo ambayo inaweza kuhamishwa kabisa katika nchi yetu. Mimi nafikiri tunalo tatizo la msingi. Sasa vingine Waziri angetusaidia kuna vigezo gani vinavyotumika ili kumwambia mwanachama mpya aingie katika Jumuiya yetu. Kama kweli vigezo hivyo vimefuatwa na kama vimefuatwa kwa nini basi wenzetu bado wanaendelea na migogoro ambayo najua sharti moja la kuingia katika Muungano wowote ule ni kwamba, nchi yako kuna misingi fulani ifuatwe moja ikiwa ya kidemokrasia lakini amani na utulivu nafikiri ni msingi. Kwa sababu msingi wetu mkubwa wa maendeleo ya Tanzania na sifa tunayopata kubwa ni suala zima la amani na utulivu tulionao. Sasa ningetaka Waziri anisaidie kupata vigezo gani walivyotumia hata wenzetu haraka haraka, wakaingizwa wakati bado wako kwenye matatizo makubwa ya mazungumzo ya migogoro na leo bado wanakuja katika Jumuiya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne ni suala zima la matumizi. Ni kweli bajeti ya Wizara ni ndogo, hakuna anayebisha hata kidogo. Tumeona shughuli wanazozifanya, matumizi yao yanabadilika kutegemea nchi na nchi. Huko Japan gharama zake ni tofauti na ukiwa Ufaransa au Ujerumani, lakini nafikiri vilevile suala la kudhibiti matumizi nalo ni la msingi sana. Kumekuwa na tatizo hili la udhibiti wa matumizi na tuliwahi kushauri wakati fulani katika Bunge lililopita, pamoja na wakati mwingine, tunaambiwa sisi Wapinzani hatusemi lakini tuliwahi kushauri kwamba ni vizuri Wizara ikawa na *task force* ya kwenda kufanya *performance auditing* katika Balozi zake zote. Mkifanya *performance auditing* kwa *experience* tuliyoipata, ambayo tuliwahi kwenye Kamati ya *Public Accounts Committee,* nina hakika mtagundua matumizi ya ovyo sana, tuliwahi kutoa mifano, hata simu afisa mmoja anaweza kutumia dola 1,500 kwa simu, tumeshuhudia hizo. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri hilo mkaliangalia. Fanyeni *performance auditing,* pamoja na kidogo kinachopatikana lakini matumizi mazuri ya rasilimali ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano ni suala zima la *direct investment*. Tuna watu wengi wanawekeza nchini kwetu, tulianza na kama Dola milioni 185,000,000 sasa tuko 420,000,000 milioni, kwa hiyo, watu wanakuja kufanya *investment* katika nchi yetu. Lakini jambo moja ambalo hatujalifanya Tanzania na tunaendelea kufanya makosa kila siku ni kumpokea kila mtu anayekuja kufanya *investiments.* Sina uhakika kama Ofisi

zetu za Ubalozi, wanakaa kitako au wanapata taarifa kwamba, fulani anakuja kufanya *investment* hapa Tanzania, hebu mchunguzeni hali yake ikoje? Ndio, tumepata makampuni yanatuuzia umeme na wengine lakini hatukufanya utafiti wa kutosha kwa kutumia Ubalozi wetu, maafisa wetu kujua kama hiyo Kampuni inayokuja kuwekeza Tanzania kweli ni Kampuni ambayo ina uwezo wa kuwekeza au fedha zake wamezipata kwa njia gani kuweza kuja kuwekeza. Nafikiri hili ndilo tatizo la msingi, tunasifia tu *direct investments* zinazokuja lakini kwa kweli hatufanyi uchambuzi wa kina, kujua wanaokuja kuwekeza ni watu wa aina gani. Katika ulimwengu wa sasa huu, kuna matatizo mengi kwa hiyo ni vizuri tukapata uhakika wa wale wanaokuja kufanya *investments*.

Sasa ili ufanye hilo, unahitaji kabisa kuiongezea uwezo Wizara ya Mambo ya Nje, kwa njia ya fedha lakini vilevile ya *manpower.* Kunahitajika *Manpower* ambayo itakuwa na uwezo wa kuweza kufuatilia hizi *investments* ili ile *cooperation* na *coordination* wanayofanya na Taasisi nyingine za nchi iweze kuwa *effective.* Vinginevyo, tutakuwa kila siku tunapata *investors* hapa, wengine ni *bogus* tu, wanakuja na Dola zao laki moja, laki mbili, basi wanalangua hapa nchini. Pengine wengine hawapitii *Tanzania Investments Centre,* wanakwenda huko Mikoani na tumepata hiyo *experience*.

Nafikiri Wabunge wanakumbuka, tulipokwenda ziara ya Wenyeviti wa Bunge Hongkong, tulikuta Watanzania wakilia kwamba, sasa wanunuzi wa vito wa Kichina, wa ki-Hongkong na kadhalika, wanakwenda kwenye mashimo wenyewe, matokeo yake watu wetu wanapokwenda kule kuuza bidhaa, wao wanapiga simu wanasema huku sisi tunanunua kwa shilingi mbili; kwa nini wanakuuzieni kwa shilingi tano? Vijana tumewakuta chungu nzima, wamekaa na mawe wamekosa soko kwa sababu ya *information* zinazotoka kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa Kichina, tuliowaruhusu kwenda katika machimbo. Sasa nasema haya ni mambo yanayohitaji kuangaliwa na kuzingatiwa ili Watanzania waweze ku-*enjoy* rasilimali zao zilizoko nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la itifaki. Niliwahi siku moja kuangalia kwenye televisheni na Spika alikuwa amekwenda Ikulu, basi mara akaondoshwa kwenye Kiti hiki akawekwa kwenye Kiti kingine, haieleweki eleweki kidogo. Kuna tatizo la itifaki ndani na nje. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, atupatie hasa orodha ya itifaki ya ndani na ya nje. Kuna masuala mengi, sasa hivi tunajiuliza je, Rais wa Zanzibar anapokwenda nje anapokewa kama nani? Maana katika Katiba ukisoma haonekani nafasi yake katika itifaki na kwa hiyo, kuna masuala mengi yanayotokea kila wakati.

Mimi nafikiri hili tungelipata tukawa-*clear,* tukajua hivi nafasi yake hasa ni ipi, lakini hata hapa ndani sio watu wote wanaofahamu itifaki ikoje? Inawezekana kiongozi amealikwa mahali, wahusika wa *Foreign Affairs* hawapo wapo, watu wengine kwa sababu hawana utaratibu wa kuelewa itifaki ikoje, wakaona mtu amekuwa hakutendewa vizuri. Mimi nafikiri kuna haja ya kutoa orodha hasa ya utaratibu wa itifaki ili ueleweke

ndani na nje, haya masuala ambayo tunayauliza kila siku yawe tena yamekwisha. Hilo ni moja ambalo nafikiri ni vizuri tukalizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho sina mengi leo ni suala zima la *investments* za majengo tunayonunua nje. Kwa bahati mbaya katika utaratibu wetu wa *Foreign Affairs*, hakuna *Development Budget* yao, wanatumia ile *recurrent* au Mfuko Mkuu wa Hazina. Mimi nafikiri kwa utaratibu wa sasa, tungependa kuona na wao wana *Development Budget* yao iko wazi. Nimeangalia hiki kitabu hapa sikuiona, basi kama ipo mahali mtanionesha tuelewe wanataka kutumia kiasi gani.

Mwisho kwa hilo, nimekuta katika Kitabu cha Waziri kwamba, mwaka huu kulikuwa na safari za nje za viongozi mbalimbali karibu 32, lakini Waziri hakutueleza ni katika ngapi zilizopangwa kwa mwaka huu. Hili ndilo tatizo moja ambalo naliona la msingi sana la matumizi kwamba, kama tungekuwa na bajeti tukajua kabisa viongozi wetu kwa mwaka huu watasafiri mara ngapi, basi ingetusaidia sana sisi Wabunge kujua kama hizo safari ni zile ambazo tumeziidhinisha. Lakini hapa unaambiwa wamesafiri mara 32, hujui Serikali ilipanga kiasi gani, Bunge liliidhinisha safari ngapi na kadhalika. Mimi nafikiri si utaratibu mzuri sana. Tungejulishwa safari ambazo sio tu hazikufanyika, lakini zilizotakiwa kufanyika kwa mwaka huu, ngapi zimefanyika na ngapi hazikufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, singoji kengele ya pili, nakushukuru sana. Mimi ninaiunga mkono hoja ya rafiki yangu. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema mchangiaji wetu mchana huu alikuwa huyo peke yake. Sasa tutaanza kuwaita Waheshimiwa Naibu Mawaziri, waanze kujibu hoja zetu, kila Naibu Waziri atapata dakika 15, mtoa hoja atapata dakika 45.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. DR. CYRIL A. CHAMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa zawadi ya uzima na afya, aliyotujalia na anaendelea kutujalia sisi waja wake katika Bunge lako hili Tukufu ili tuifanye kazi ya kuwaongoza wananchi waliotuchagua, tukiwa wazima wa afya na hivyo wayapate kutoka kwetu mafanikio wanayotazamia. *(Makofi)*

Napenda kukupongeza sana wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge hili Tukufu, kwa namna mnavyoliongoza Bunge hili kufanya kazi yake. Nampongeza pia Katibu wa Bunge na Watumishi wote, kwa jinsi wanavyoweka mipango mizuri inayolifanya Bunge hili lifanye kazi zake vyema. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuniamini na kunipa muda zaidi ili niendelee kulitumikia Taifa letu katika nafasi hii ya Unaibu Waziri. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais kuwa, nitaendelea kuchapa kazi kwa uadilifu, utii na uaminifu kwake.

Namshukuru pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa uongozi, maelekezo na ushauri wake wa mara kwa mara kwangu, katika utekelezaji wa

majukumu yangu. Napenda kumpongeza sana Waziri wangu Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

Namshukuru pia kwa uongozi wake na maelekezo yake ya mara kwa mara, yanayoniongoza katika utendaji wangu wa kazi. Kama nilivyofanya kazi kwa karibu na mtangulizi wake Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, napenda kumhakikishia utayari wangu na kulitumikia Taifa letu chini ya uongozi wake ili matarajio ya Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kwa Wizara yetu yatimizwe. *(Makofi)*

Shukrani zangu pia nazitoa kwa Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Katibu Mkuu Balozi Patrick Mombo, Naibu Katibu Mkuu, Balozi Sanga, Mabalozi, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru kwa dhati, Wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini, kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa katika kutekeleza kazi zangu za Ubunge. Napenda kwa kupitia Bunge lako Tukufu, niwathibitishie kuwa nitaendelea kuwawakilisha kwa bidii katika Bunge hili na niwapo nje ya Bunge, nitaendelea kuchapa kazi pamoja nao kuhakikisha kuwa, matatizo sugu tuliyokuwa tumeyazoea muda mrefu, yanapatiwa ufumbuzi katika Serikali hii inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. Napenda kumalizia maneno yangu ya utangulizi kwa kuishukuru familia yangu, kwa upana wake wa kunielewa na kunivumilia ninapokuwa natumia muda mwingi mbali nao katika utumishi wangu kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijibu hoja mbalimbali kati ya nyingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwa kuchangia hoja ya Waziri wangu. Kabla sijaanza kuzijibu, napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Hoja ya kwanza ilitolewa na Mheshimiwa James D. Lembeli, wakati anachangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naye alikuwa anaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupeleka maofisa wenye taaluma ya utalii kwenye Ofisi za Ubalozi ili kuongeza ufanisi katika biashara hii ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwa ushauri wake. Napenda kumhakikishia kwamba, kadri hali ya uchumi inavyoboreka na kuimarika, Wizara yangu itawaajiri wataalamu wa kada mbalimbali sio tu hii ya utalii ila kada mbalimbali za uchumi, siasa na jamii katika Balozi zetu, ikiwa ni pamoja na hawa wenye taaluma hii ya utalii.

Napenda sasa kujibu hoja ya Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka CHADEMA, ambaye amejikita katika taasisi yetu ya *Arusha International Conference Centre (AICC)*. Kwanza, amekiri mchango wa *AICC* katika kuwaingiza wageni nchini Tanzania. Pili, alikiri ukweli kwamba, *AICC* haikujengwa

rasmi kama Kituo cha Mikutano na kubainisha hoja ya kujengwa ukumbi mwingine mpya. Tatu, alipendekeza kwamba, ukumbi mpya ujengwe Bagamoyo kwa ajili ya historia yake na ukaribu na Zanzibar, kuhakikisha wageni wanaokuja wanaweza kutembelea pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, kwa kutambua mchango wa *AICC* kuwaleta wageni wengi nchini. Hali kadhalika, ninamshukuru Mbunge kwa kukiri ukweli kwamba, kwa *AICC* kujengwa kama ofisi inashindwa kukidhi kwa kiwango kikubwa, mahitaji yanayoendana na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano na hivyo kuwepo kwa hitaji la ujenzi wa kituo kipya cha kisasa kitakachokidhi mahitaji ya wakati huu. Hata hivyo, kuhusiana na ushauri wake kwamba kituo kipya kijengwe Bagamoyo, kwa sababu nzuri alizozitoa, ningependa kutoa maelezo yafuatayo: Moja, kwamba ujenzi wa kituo kama hicho, huhitaji kukidhi na vigezo vingine vingi. Hili linahitaji utafiti wa kina kabla ya uamuzi wa ujenzi kufikiwa kwamba, kwa kuzingatia mifano katika nchi nyingine sio jambo la ajabu kwa vituo kama hivi kujengwa katika miji mbalimbali. Hata hivyo, ujenzi wa vituo hivi ni uwekezaji mkubwa na hufanyika tu pale ambapo vigezo vingi vinakidhiwa. Kwa kutambua upungufu wa *AICC* kujengwa kama ofisi, mchakato wa ujenzi wa kituo kipya umekwisha anzishwa na Uongozi wa *AICC*, ikiwa ni pamoja na kuliingiza wazo hilo rasmi katika Mipango ya *AICC* kupitia Mpango Mkakati wa mwaka 2007 - 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mbunge wa Jimbo la Kilindi kwa tiketi ya CCM, naye alikuwa na mchango wake kuhusu *AICC.* Alisema kwamba, pamoja na pongezi kwa *AICC* ni lini kituo kipya cha Mikutano cha Kimataifa ambacho kitakuwa pia na sehemu ya maonesho *(Exhibition Space)* kitajengwa? Pia alitahadharisha haja ya kituo kujengwa nje ya miji ili kupunguza msongamano mijini mara kunapokuwepo na ugeni wa viongozi. Mheshimiwa Mbunge, ameshauri kuwepo na msukumo zaidi ili ujenzi wa kituo kipya ufanikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimwa Beatrice M. Shellukindo, kama ifuatavyo: Mkakati wa Shirika wa mwaka 2007 – 2012, umeelekeza kwamba maandalizi yaanze na yameshaanza na sasa hivi yanaendelea vyema kwa kushirikiana na Kituo cha Ushauri cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(University Consultancy Bureau)*, upembuzi yakinifu unakaribia kukamilika. Pia Baraza la Mazingira *(The National Environmental Council),* wamekwisharidhia Mradi huu kuendelea kufanyiwa kazi. Hali kadhalika, zabuni ya kuwapata wataalamu wa kuandaa *Architectural Concept* imekwishatangazwa, yaani *expression of interest*. Ili kusimamia mchakato huu, kikao cha wadau kilikutana tarehe 23 Machi, 2007 Dar es Salaam na kiliteua Kamati Maalum ya Kusimamia suala hili. Kamati hii Mwenyekiti wake ni Profesa Mwajabu Posi, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *AICC,* inahusisha pia wadau wengine kama ifuatavyo; *NSSF, PPF, PSPF, LAPF, TANAPA, NCCA,* Manispaaa ya Arusha, *TTB, TIC* na *AICC* wenyewe. Wizara husika ni pamoja na Wizara yangu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mipango na Uwezeshaji, Maliasili na Utalii na Wizara ya Fedha.

Kuhusu kituo kujengwa nje ya mji ili kuepuka msongamano, naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo: Kwa kawaida vituo vya namna hii, huwa vinajengwa katikati

ya miji. Hii ni ili kuwezesha wageni kuwa karibu na huduma mbalimbali na kuwapa uchaguzi katika mahitaji yao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na malazi. Uongozi wa Mkoa wa Arusha kwa kushirikiana na Manispaa ya Arusha, inalifanyia kazi tatizo la msongamano wa magari mjini Arusha. Ni imani yangu kwamba, hiki hakitakuwa kikwazo cha kufanikiwa kwa Mradi huu muhimu.

Mwisho, namshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa kuona haja ya kuwepo msukumo mkubwa ili Mradi huu ufanikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine hii tena imetolewa na Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, nayo inahusu ufunguzi wa Balozi zetu mpya uzingatie maslahi ya kiuchumi ya nchi yetu. Napenda kumhakikishia kwamba, Sera yetu ya Mambo ya Nje, imeweka bayana msisitizo mkubwa katika kuendeleza maslahi ya nchi. Maslahi haya ni pamoja na kutafuta masoko ya mazao yetu, kuwashawishi watalii watembelee nchi yetu, kuwavutia wawekezaji na kutafuta misaada. Kwa hali hiyo, Balozi zetu tunazifungua katika zile nchi rafiki na ambazo tunaweza kuwa na maslahi ya kiuchumi nazo kama vile ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imetolewa na Mheshimiwa Felix N. Kijiko, ambaye ameshauri kwamba, uwepo ushirikishwaji mkubwa zaidi wa wananchi waishio nje ya Tanzania Balozini. Yaani katika zile Balozi zetu, wale Mabalozi wawe na utaratibu wa kuwafanya wale Watanzania washirikishwe zaidi katika mambo ya pale. Imekuwa ni sera ya Wizara yangu, kuwahamasisha Watanzania waishio ughaibuni au wanaotembelea maeneo yenye vituo vyetu kutoa taarifa katika Balozi zetu ili wajulikane walipo, kwa bahati mbaya kwa baadhi ya wengine hili halifanyiki.

Tukio kubwa lililowafanya Watanzania wengi waishio nje kufahamika, ilikuwa ni wakati wa kubadilisha hati za kusafiria. Kwa hiyo, mtu anapotaka pasipoti ndiyo anakwenda pale anafahamika. Wale waliofanya hivyo, taarifa muhimu ziliingizwa kwenye mtandao wa kompyuta, lakini wapo wengi ambao hawapendi kujitambulisha. Jitihada zinaendelea na hili tunalichukulia kama changamoto kwa mwaka ujao, kuwatafuta na kufanya wawe na Jumuiya za pamoja za kusaidiana ikiwa ni pamoja kuwa na ushirikiano wa karibu zaidi na Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Naibu Waziri mwenzangu, anazo ahadi za kujibu na Mheshimiwa Waziri, mimi naomba niishie hapa kwa kuunga tena mkono hoja kwa asilimia mia moja. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ningependa nitamke kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu walionitangulia, kwa kutoa rambirambi zangu kwa familia ya Mheshimiwa Juma Akukweti, aliyefariki kwa ajili ya ndege na pia kwa familia ya Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Kitope, kwa ushirikiano wanaonipa katika kuliletea maendeleo jimbo letu. Nawaomba waendelee kunipa ushirikiano wao huo. Vilevile napenda nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, kwa ushirikiano, maelekezo na miongozo mbalimbali anayonipa ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, kwa namna tunavyoshirikiana katika kutekeleza kazi zetu. Michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni mingi, ambayo ilikuwa na faida kubwa kwetu. *(Makofi)*

Michango hiyo tunaamini ilitolewa kwa nia ya kuisaidia Wizara yetu kufanikisha shughuli zake. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, michango ilikuwa mingi lakini kwa muda nilionao, naomba nijibu michango michache kama ifuatavyo: Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo na Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, wamezungumzia uchache wa Mabalozi Wanawake. Kulingana na Maazimio ya Kimataifa, wanawake wanapaswa kuchukua nafasi za juu za uongozi, angalau asilimia 30.

Nchi yetu imekuwa ikitekeleza hili kwa kutoa nafasi zaidi kwa Wabunge, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Makatibu Wakuu. Miongoni mwa wengi na katika baadhi ya maeneo tayari tumevuka lengo hilo. Kwa upande wa uteuzi wa Mabalozi, mamlaka ilikuwa ikitoa nafasi kwa wanawake kila fursa zinapojitokeza. Kwa mfano, idadi ya Wanawake Mabalozi kwa sasa ni watatu, baada ya kuwepo wawili tu kwa kipindi cha miaka mingi iliyopita. Nakiri kuwa, bado wapo wanawake wengi wenye sifa za kuwa Mabalozi na tutashauri wateuliwe kila fursa zitakapojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo pia amezungumzia Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iwe Idara ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Hadi mwaka 2005, Wizara ya Afrika Mashariki au Afrika Mashariki ilikuwa ni Idara ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, baada ya hapo iliamuliwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba, kila nchi mwanachama iunde Wizara ili iweze kusimamia shughuli za kukuza Jumuiya hiyo. Kwa maana hiyo, kuwepo kwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kumetokana na maamuzi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, ameulizia ni sifa zipi zinazotumika katika kuteua Mabalozi na Maafisa. Uteuzi wa Mabalozi ni mamlaka iliyo chini ya Rais na ana uwezo wa kuteua Balozi yeyote, ambaye anamwona ana sifa na uwezo wa kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje. Uteuzi wa Maafisa umo ndani ya uwezo wa Wizara yangu na Katibu Mkuu na Menejimenti huteua Maafisa kutoka Wizarani, wenye uwezo, sifa na haiba. Hawa lazima wawe na ujuzi na uelewa wa kutosha katika

masuala ya siasa ya mambo ya nje, uchumi na sheria na kupangwa katika Balozi kutegemeana na nafasi zilizoko Ubalozini na mahitaji yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, ameulizia kwa nini Ubalozi wa Uingereza nchini, haurudishi fedha za maombi ya *Visa* hata kama mwombaji hakupata *Visa* hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila nchi ina utaratibu wake wa kuhudumia maombi ya viza, Uingereza, Marekani, Ufaransa na nchi nyingine wanatumia mtindo huu wa kutorudisha ada ya viza kwa muombaji aliyekataliwa. Sababu mojawapo wanayoitoa ni wingi wa maombi ya viza ambayo inawafanya kuweka maofisa wengi kwa shughili hii tu ya viza. Mantiki yake ni kwamba hawataki kutoa fedha za kodi za wananchi wao kuhudumia watu wanaotoka nchi nyingine kuingia nchini mwao. Hata hivyo leo asubuhi wakati hoja hii ikitolewa vile vile kwa kuzungumza Mheshimiwa Ubalozi wa Uingereza alikuwepo hapa na alisikia kilio hiki cha Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya wananchi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed aliuliza ipi nafasi ya Rais wa Zanzibar kiitifaki nje ya nchi kwa kuzingatia Katiba ya nchi, anayempokea katika nchi hizo anazokwenda? Mheshimiwa Rais wa Zanzibar hufanya safari za nje kwa nyadhifa mbalimbali, kuna safari anazomwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Safari hizi hupokelewa na kupewa wadhifa kama mwakilishi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Katika safari zinazohusu masuala ya Zanzibar wenyeji hufahamishwa wadhifa wa Rais wa Zanzibar nchini na wao huamua stahili gani ya kumpa na utaratibu wa kumpokea. Utaratibu huu umefanywa na Korea Kaskizini na China. Viongozi hao wanapokuja nchini wanatueleza wadhifa wa kiongozi wao nchini kwao na sisi huamua ngazi ipi kiitifaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia imezungumzia nini tamko la Serikali kuhusu kuanzisha viza yaani *Uni-visa*. Katika kikao cha wakuu wa nchi na Serikali wa *SADC* kilichofanyika Maseru, Lesotho Agosti, 2006 kiliagiza utaratibu wa viza moja utumike katika nchi za *SADC* ifikapo mwaka 2008. Msimamo wa Serikali uliotolewa katika Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa *SADC Organ* uliofanyika Dar es Salaam tarehe 26 hadi 29 Julai, 2007 ni kwamba Serikali bado haijawa tayari kuingia kwenye *Uni-visa* na majadiliano bado yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee pamoja na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid wamezungumzia upungufu katika Ofisi ya Mambo ya Nje ya Zanzibar. Upungufu wa watendaji, upungufu wa vitendea kazi na pia uchakavu wa jengo. Ofisi ya Mambo ya Nje ya Zanzibar ambayo ni moja ya Idara tisa za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa hivi sasa inawatendaji 14 ambao kwa hivi sasa ndiyo wanaoendelea na kazi Idarani hapo. Kati ya watendaji hao watatu ni maafisa mambo ya nje ambapo wawili kati yao wamerejea hivi karibuni kutoka Balozi zetu za China na Saudi Arabia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa makusudi iliamua kuwarudisha Zanzibar ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Idara hiyo. Mbali ya hao watatu Idara pia ina maafisa wengine watano ambao bado wanaendelea na kazi katika ofisi zetu za Kibalozi nchi za nje. Maafisa hao watarejea nchini baada ya kumaliza muda wao wa kazi katika vituo vyao. Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha Wizara imeshapata kibali cha kuajiri maafisa 60 wakiwemo maafisa ambao watapelekwa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la vitendea kazi mfano kama magari Idara ina magari mawili kati ya hayo, moja kwa ajili ya Mkurugenzi na moja kwa ajili ya shughuli nyingine za ofisi zikiwemo za kuwapokea Mabalozi na viongozi wengine stahiki. Wizara itaongeza idadi ya magari hayo wakati wowote hali itakapo ruhusu. Kuhusu ukarabati wa jingo, Wizara imetenga fedha za ukarabati wa jengo hilo kama inavyofanya kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, ameuliza Wizara kusaidia kutangaza utalii na biashara ya Zanzibar, kwa kupitia Balozi zetu zilizopo nchi za nje Wizara imekuwa na inaendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi zote za biashara na utalii za pande zote mbili za Muungano katika kutekeleza sera yetu ya mambo ya nje ikiwa ni pamoja na kukuza biashara, kutangaza utalii na kuongeza kasi ya uwekezaji kwa pande zote mbili za Muungano. Majarida na machapisho mbalimbali ya biashara, utalii na uwekezaji ambayo tumekuwa tukiyapokea kutoka *ZIPA* na Kamisheni ya Utalii Zanzibar yanaendelea kusambaza katika Ofisi zetu za Kibalozi zilizoko nje kwa madhumuni ya kutangaza utalii wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sitaki kengele ya pili inifikie naomba niishie hapa ili nimpishe mtoa hoja apate nafasi ya kutosha na naunga mkono hoja tena. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza kabisa napenda nishukuru kwa ujumla michango mizuri sana iliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi zote za CCM na Upinzani. Lakini kabla sijaenda kujibu maalumu, naomba nitoe sasa shukrani zangu kwa watu wote waliochangia na naomba niwatambue kwanza watu waliochangia kwa kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu kumi na moja wamechangia kwa mazungumzo, wazungumzaji hao ni kwanza, Msemaji wa Kamati Mheshimiwa Juma Killimbah, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Rished Abdallah na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. *(Makofi)*

Lakini pia naomba niwatambue Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Dr. Cyril Chami na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, waliomalizia kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina orodha ya wachangiaji 28 waliochangia kwa maandishi na ningependa niwatambue kuwa ni Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Kaita Telele, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Charles Kajege na Mheshimiwa Dorah Mushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nikiri kwamba michango yao ni mikubwa na katika dakika 40 nilizopewa sitaweza kuyajibu yote. Lakini napenda niahidi kwanza kwa ujumla kwamba yote yaliyojibiwa yatapatiwa uzito wake. Tutakwenda Wizarani, timu ya wataalamu itayatayarisha majibu na ninaahidi kwamba Bunge lako Tukufu yale mengine ambayo sitaweza kuyajibu sasa tutayaleta kwa maandishi ili kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru Kamati ya Mambo ya Nje kwa kazi nzuri ya hoja walizojenga. Moja kati ya hoja kubwa walizojenga ni kwamba baada ya kuona kwamba Wizara ina fedha finyu wamekuja na pendekezo kwamba mikutano kama ya *Sullivan APRM* na uanzishwaji wa *Africa Court* ni mzigo mkubwa na wameomba kwamba mfuko unaolipia madeni Serikalini ujaribu kusaidia kulipia gharama hizi. *(Makofi)*

Mimi kama mwenye dhamana ya Wizara nasema tumelipokea hili na najua kwamba Mwenyekiti wa Mambo ya Nchi za Nje amekwishazungumza na Waziri wa Fedha kuhusu pendekezo hilo na najua kwamba mazungumzo yanakwenda vizuri na sisi tunawaombea waendelee vizuri ili baadhi ya gharama hizi kama alivyoahidi Mheshimiwa Anna Abdallah pamoja na Mama Zakia Meghji kwamba wanalishughulikia hasa suala la *Sullivan,* Wizara itashukuru sana iwapo fedha za *Sullivan* kama nilivyoeleza zitachukuliwa na Serikali Kuu ili kulipia gharama za *Sullivan* ili fedha tulizopata ziweze kufanya kazi nyingine. Kwa hiyo, hili tunalifikiria na tunadhani litafanikiwa. Lakini liko pia pendekezo la Kamati linalosema, kwa kuwa fedha ni chache kwa nini tusipunguze baadhi ya Balozi yaani tuwe na Balozi chache ya kuziendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili lina matatizo yake, si jambo rahisi sana kupunguza Balozi zetu hata kama zilikuwa ni za kisiasa na kwamba sisi tunaamini kwamba matatizo yanayotupata ya Bajeti finyu ni ya muda mfupi na si vyema tukaanza kufunga Balozi tunaamini baada ya muda si muda mrefu, baada ya mwaka huu kupita katika hii tutakuwa na fedha zinazotosha na zitakazoiwezesha Serikali kuendelea sio tu

kuendesha Balozi zilizopo 31 lakini kuongeza Balozi zaidi. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kufunga Balozi kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imekuja na swali lini Mahakama ya Afrika itaanza kazi yake Arusha? Napenda kujibu swali hili kwamba Mahakama itaanza shughuli zake mwezi Septemba, 2007. Lakini ni vizuri Watanzania wakaelewa heshima ambayo tumepewa na Umoja wa Afrika wa kuamua kwamba Makao yake Makuu ya Mahakama Kuu ya Afrika yawe Tanzania na yawe Arusha. Sasa kutakuwa na awamu mbili, awamu ya kwanza ya muda mfupi ambayo itagharimu bilioni 19.3 itahusu ununuaji na upangishaji majengo kwa ajili ya viongozi wa Mahakama kuweza kufikia na kuanza kazi zake pale *AICC* na sehemu nyingine. Shughuli hii itaanza mwezi Septemba, 2007. Lakini tunao mpango wa muda mrefu ambao tumeshauriwa na Umoja wa Afrika kwamba ni vizuri tukawa na eneo kubwa Arusha litakalojengwa jengo ambalo wanasema ni *symbolic building* ambalo litakuwa ni kielelezo cha Umoja wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kutafuta wafadhili kwa ajili ya ujenzi huo umeanza na tuna mategemeo makubwa kwamba baada ya muda mfupi tutawaletea taarifa hasa Kamati ya Mambo ya Nje, taarifa ya maendeleo ya mchakato wa kujenga jengo la Afrika litakalohusika na Mahakama ya Afrika Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, limeulizwa pia swali na upande wa Upinzani kuhusu suala la Ubalozi wa Afrika Kusini kwamba Ubalozi wetu wa huko unao matatizo, kuna pesa pale zimepotea na kwa kweli hii lugha ya kusema basi hati zimeshapatikana liishe tupate maelezo.

Napenda kujibu hivi kwa kweli kulikuwa na utata kwenye Ubalozi wetu wa Afrika ya Kusini kuhusiana na matumizi ya pesa hasa katika ununuzi wa nyumba. Tumelifuatilia suala hili kwa karibu, Kamati iliwaunganisha watu wangu wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, watu wanaohusika na ardhi Wizara ya Miundombinu pamoja na Wizara ya Fedha walikwenda Afrika Kusini kufanya uchunguzi na utafiti wa suala hili na jibu lililopatikana ni kama ifuatavyo kwamba ni kweli tulikuwa tumenunua nyumba yenye thamani ya Randi 850,000 kwa sababu ile nyumba ilikuwa imekaa kwenye eneo ambalo huwezi kwenda na gari yaani *land road*, aliifunga ikawa kama jiko la nyuma ambayo huwezi ukaingia kwa mbele, busara za Ubalozi na Wizara ni vyema tukaiuza nyumba hiyo ili kununua nyumba ambayo kiusalama ni safi inaweza kuingilika na bila matatizo. Kwa hiyo, ikaamuliwa kwamba nyumba ile iuzwe ili inunuliwe nyumba mpya. Kwa hiyo, nyumba ile iliuzwa kwa Randi 850,000 lakini tukanunua nyumba nyingine mpya kwa Randi 1,600,000 kwa hiyo tuliongeza pale. *(Makofi)*

Sasa tumepata nyumba mpya Afrika Kusini, Mdhibiti Mkuu baada ya kupata haki zote na maandishi yote ameridhika kwamba *transaction* zile zilikwenda kihalali na angependa niuombe upande wa Upinzani ukubaliane na upande wa Serikali kwamba habari hii sasa imekwisha, tumeshanunua nyumba mpya na hati zile zimekubalika tuangalie ya mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kuhusu Bunge la *SADC*. Sasa ni kweli kwamba *SADC* kama Jumuiya ya Kanda ya nchi zaidi ya 13 inahitaji kuwa na Bunge lake na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa anataka kujua iwapo kikao cha mwezi huu kitakachofanyika na wakuu wa nchi wanachama Lusaka, Zambia watalizungumzia suala hili. Kutokana na ajenda tulizonazo suala hili halitazungumziwa lakini nalijua lipo, mchakato wa kuanzisha Bunge katika upande wa *SADC* upo lakini wajumbe wa nchi hizi mbili bado wanatafakari kuelewa mipaka, kuelewa shughuli na kuelewa nchi nyingine zinafanya nini. Tanzania tunafaida kwa sababu Afrika Mashariki tutajifunza kutoka huko. Lakini mchakato huu umeanza, nyaraka zote zinazohusu uanzishwaji wa Bunge la *SADC* zimeshafika katika nchi zote na nina hakika baada ya kikao cha Lusaka, Zambia, kikao kitakachofuata kitaanza na mchakato wa kuangalia uwezekano wa kuanzisha chombo kinachoitwa Bunge ili kuweza kuratibu mikataba mbalimbali na shughuli mbalimbali ili kufanya *SADC* iwe *effective organisation* au chombo hasa kinachoweza kutumainiwa.

Mheshimiwa Lazaro Nyalandu amezungumzia masuala mawili, suala la *Visa abolition* na *dual nationality*. Kuhusu suala la kuondoa viza ili kuwezesha wananchi wa Tanzania wanaokwenda kwenye nchi nyingine waweze kwenda kirahisi bila matatizo naweza kujibu kwamba mchakato huu umekwishaanza. Tanzania na nchi jirani zimeamua kupeleka *protocols* yaani kusaini mikataba itakayowaondolea wananchi usumbufu wa kila mara kuomba viza wanaposafiri katika nchi hizo.

Napenda kulitangazia tena Bunge lako Tukufu kwamba nchi kama ya Msumbuji sasa hivi tumeshaondoa viza zote, wananchi wetu sasa wanaweza kwenda Msumbiji bila bughudha yoyote ile ya kwenda kuomba viza. Nchi ya Afrika Kusini tumeshaanza, hivi sasa ninavyoongea viza za Kiserikali pamoja na za diplomasia zimekwishafutwa watu wote wenye *Diplomatic Passports* na wale wanaotoka Serikalini sasa hivi wanaweza kwenda Afrika Kusini bila bughudha ya kuomba viza. Mkakati wa kuendeleza wigo huo ili uwafunike wafanyabiashara na sehemu nyingine unaendelea na ni matumaini yangu kwamba mbele ya safari wananchi wa nchi hizi mbili watakuwa wanakwenda bila viza na tunafanya hivyo kwa nchi nyingine ambazo zinatuzunguka.

Kuhusu suala la *dual nationality*, napenda kwanza nisema namshukuru sana Waziri wa Mambo ya Ndani kwa sababu suala hili alilieleza kwa upana na kwa umahiri mkubwa. Lakini ningependa tu ndugu Watanzania nisiisitize jambo la msingi kubwa kwamba suala la msingi kubwa tunaloliuliza kwenye *dual nationality* yaani uraia wa nchi mbili swali kubwa la msingi ambalo Watanzania hatuna budi kujiuliza mpaka hapo uamuzi utakapochukuliwa ni hili. Inapotokea Mtanzania anayeishi nje kwa sababu yoyote ile anachukua uraia wa nchi ile je, aendelee kuhukumiwa kwa kunyang'anywa uraia wake wa kuzaliwa wa Tanzania? Hilo ndilo swali la msingi, tumnyang'anye au tumpokonye uraia wake wa Tanzania kwa sababu tu huyu mtu kachukua uraia wa nchi nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo swali la pili kwamba je, wale wageni wanaokuja Tanzania kwa mfano katika kipindi cha mwaka 2005/2006 wageni 101 tuliwapatia uraia wa Tanzania maana wanayo haki pia ya kuomba uraia wa

Tanzania. Swali la pili ambalo Watanzania ni lazima kujiuliza kama kuna *justification*, kama kuna uhalali wa kuwapatia wageni hati za uraia Tanzania wale waliotekeleza masharti mbalimbali na wanapata uraia kwa nini Mtanzania aliyopo nje na ametekeleza masharti huko nje tusimruhusu apate uraia ili moja, aweze kupata matibabu kirahisi, pili aweze kupata ajira ili aweze kusaidia familia yake na kuleta fedha nchini, tatu, aweze kusomesha ndugu zake au watoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tunaamini kwamba ndiyo mazingira yanayoweza kumfanya Mtanzania anayeishi nje aweze kuipenda Serikali na nchi yake, aweze kuleta fedha ndani ya nchi hii na aweze kulitumikia Taifa lake kwa mujibu wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2005.

Lakini hayo ndiyo mapendekezo, mapendekezo haya sasa yanagusa Tanzania ambayo ni Jamhuri yenye pande mbili za Muungano na ndiyo maana Waziri wa Mambo ya Ndani akasema pamoja na mapendekezo mazuri na shughuli nyingi kwenda Serikalini lakini suala hili lazima lipate sasa uzito kuhusu na upande wa pili wa Muungano ili walidhie na wakubali halafu lirudi tena kwenye Serikali Kuu kuona kama kuna uhalali ya kuendelea na *dual nationality* ili kuweza kufikia malengo yaliyotamkwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nilijibu swali linalohusu *Sullivan.* Mkutano wa *Sullivan* ni Mkutano wa Waamerika weusi ambao wanasifa tatu. Sifa ya kwanza kwamba Waamerika hawa wana-*business* na *investments.* Sifa ya pili ni kwamba Waamerika hawa ni *professionals* ni wataalamu wa masuala mbalimbali na sifa ya tatu ni kwamba Waamerika hawa ni Wasomi. Kwa hiyo, wamejiwekea utaratibu wa kuwa kundi kubwa Amerika ambalo linasema kwamba lina *moral obligation* yaani linawajibika kuisaidia Afrika kwa sababu na wao wametambua kwamba asili yao ni Afrika. Kwa hiyo, wakapendekeza na wamejiita sasa *The Sullivan* kutokana na kiongozi aliyeanzisha utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakapendekeza kwamba kwa kuwa *root* yao ni Afrika wangependa kuja Tanzania, kuwaleta wasomi wao, wachumi na *investors* wao ili kuja kujadiliana na Tanzania pamoja na viongozi wa nchi nyingine zinazoizunguka Tanzania wapatao 30 lakini wanaleta ujumbe wa watu wasiopungua 3,000. Ni Mkutano mkubwa mno utakaofanyika mwakani mwezi wa sita. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni Mkutano mkubwa ambao utaleta fursa ya Waamerika weusi kuja kuwekeza Tanzania na nchi nyingine katika maeneo ya utalii na biashara na mambo mengine. Kwa hiyo, ni Mkutano ambao Mheshimiwa Rais ameufungua rasmi wiki chache zilizopita Jijini Dar es Salaam na ningependa sasa kusema wazi kwamba ni Mkutano ambao utakuwa mkubwa sana lazima tutumie nafasi hiyo wafanyabiashara wetu wadogo wadogo, Wizara na sekta mbalimbali ambazo zina nia ya kupata *partners* wawekezaji kutoka nchi za nje ya Marekani na sehemu nyingine waje na wenyewe wakae chonjo watapata ratiba zote ili wageni hawa watakapofika kwa wingi wa namna hii waweze kuingia *partinership* ya kuweza kulete biashara, ku-*promote tourism* katika nchi yetu bila kuchelea. Hiyo ndiyo inayoitwa *Sullivan* na kuna pesa nyingi na kuna pesa

nyingi zinahitajika kama mlivyoambiwa kwenye Bajeti na tumekubaliana na nasema tena Mheshimiwa Anna Abdallah pamoja na mama Zakia Meghji na Serikali kwa ujumla inaangalia kuona ni namna gani tunaweza kuwezesha Mkutano huu ufanikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia lipo suala la, *African Peer Review Mechanism (APRM)*. Huu ni utaratibu wa nchi kujipima yenyewe katika masuala ya utawala bora na demokrasia. Kama nchi inafanikiwa kufanya hivyo, *donors* wapo tayari kuisaidia nchi hiyo maradufu zaidi. Kwa hiyo, zipo nchi katika Bara la Afrika kujipima zenyewe namna zinavyojiongoza, namna zinavyoendesha shughuli za Serikali. Uenyekiti upo chini ya Waziri Mkuu wa Ethiopia Mheshimiwa Zenawi. Sasa Tanzania tumeungana na Senegal, Afrika Kusini na sisi wenyewe kwamba tuko tayari kujipima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukijipima kwa sababu hatuna sababu ya kujiogopa, hakuna sababu ya kuhofia tuko tayari kujipima, kama tulivyojipima UKIMWI ili wenzetu watuoene kwamba sisi hatuna tatizo na ili tuweze kupata *partners* na *donors* wanaoweza kusema kwamba Tanzania udhaifu wake ni huu, umaarufu wake ni huu, nguvu zake ni hizi na tuisaidie kufanya shughuli hizo na sisi tunasema tutafika huko na tunajipima na tayari tuna chombo kinachohusika na *APRM* na kimekwishaanza kazi zake na viongozi wameshachaguliwa na ni matumaini yangu kwamba mambo haya yatakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja ya dada yangu Mheshimiwa Fatma Mikidadi na kwa sababu swali hili linatoka Lindi ni vizuri nikalijibu kwa sababu linahusu huko huko ninakotoka. Mama Fatma Mikidadi anasema tuna mjusi wetu Ujerumani atarudi lini Lindi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme tena kwamba suala la mjusi wa Lindi ni suala kubwa. Mjusi aliyopo Ujerumani ana urefu wa mita 22 na kwenda juu ana urefu wa mita 13, sio futi tunazungumzia mita. Mjusi huyu alichukuliwa mwaka 1905 na Namitumbo ambaye anaitwa *Dinosaur* na yuko Berlin. Ndiyo kivutio kikubwa cha Utalii Berlin. Mtoto wake ana urefu wa mita nne na mita nne kwenda juu, yupo pale. Mjusi peke yake duniani ambaye alikutwa *intact* kasoro nyama lakini mifupa yote kuanzia kichwani hadi mkia wake imekutwa *intact.* Sasa Profesa Mshegeni wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ametuletea taarifa ya awali na taarifa ya awali hii nimempelekea Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma *debate* ilikuwa je, Ujerumani itakuwa tayari kumrejesha mjusi huyu na mwanae, lakini pili tutamweka wapi, tatu tutarudishaje? Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tumearifiwa na *UNESCO* kwamba mchakato huu kumbe unawezekana. Lakini taarifa ya pili tumearifiwa na *Pan African Parliament* imepitisha sheria inayosema kwamba Afrika iungane mkono na *UNESCO* na Umoja wa Mataifa ili kurejesha vitu vyote vyenye thamani ikiwemo mifupa ya mjusi huyu, kurejesha kwenye nchi zinazohusika ili viendelee kuwa vivutio.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshauriana na Profesa Mshegeni kwamba akamilishe utafiti wake ili tuweze kuufikisha rasmi, ili Serikali ione namna ya

kuzungumza na watu wa *UNESCO*, namna ya kushirikiana na watu wa Umoja wa Afrika ili kuweza kurudisha mjusi huyu ili awe ndiyo ngome ya Utalii mpya wa mjusi Mkoa wa Lindi. Kwa hiyo, dada yangu Mheshimiwa Fatma Mikidadi, mchakato utafika lakini lazima kwanza taarifa tuipeleke kwenye Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ameniuliza swali la kusema hizi safari za viongozi kwenda nchi za nje, tungezijua halafu ndio tungezifanyia Bajeti. Inakuwa ni vigumu Mheshimiwa kuzijua hizi safari. Kwa sababu ziko safari za aina tatu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, safari za kwanza ni zile za kupanga ambazo ziko kwenye ratiba maalumu. Kwa hiyo, kwa mfano, naweza nikasema kuna safari za *AU* ambazo tayari Mheshimiwa Rais ameshazifanya, maana zinajulikana kwa kalenda. Kuna safari ya Umoja wa Mataifa ya kuzungumza na Baraza la Umoja wa Mataifa ambayo itafanyika mwezi Septemba na kuna safari anazoalikwa Ufaransa na Serikali ya Italy. Sasa mialiko hii inakuja wakati Bunge hili halipo na wakati mwingine wakati hatupo. Ni mialiko ambayo inakuja tu, hata hivi ninavyozungumza, mialiko inakuja tu. Kuna mialiko ya Waziri Mkuu pia, mialiko ya Makamu wa Rais, inakuja bila sisi kuipanga! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kilichofanyika na Idara ya *Protocol* na Wizara yangu, ni kuangalia wastani wa safari zinazotakiwa kufanywa na viongozi kila mwaka halafu tunazifanyia *budgeting*. Kwa hiyo, ndicho tulichokifanya na ndio maana mwaka huu tumeomba shilingi bilioni nane kwa kuangalia wastani wa safari za viongozi wetu wa Kitaifa kwa safari hizo zilizopangwa kiratiba, safari zinazokuja kidharura na safari zinazokuja kwa ajili ya mialiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu asubuhi, viongozi wetu wa Kitaifa wana sifa kubwa ya kuheshimika duniani, ni matumaini ya matatizo mengi duniani na wanaalikwa sana na viongozi duniani na nafurahi viongozi wote na Waheshimiwa Wabunge sasa tunaelewa kwamba viongozi wetu hawa hawaendi tu kucheza, wanakwenda kuhemea. Mimi ningeomba tulielewe hilo ili safari wanazozifanya tuzione katika upande wa *plus* na siyo kuziangalia upande wa *negative*. Nashukuru swali hili limekuja kwa mtindo huu, ninapata faraja kwamba kinachoulizwa hapa ni idadi ya safari, lakini siyo manung'uniko ya kwa nini mtu anasafiri! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako viongozi wa Afrika ambao hawajasafiri hata siku moja kwa sababu hawapendwi. Wapo viongozi wa Afrika hawajasafiri hata siku moja huko duniani kwa sababu hawana mchango na hawana ushawishi maalumu wa kuiwezesha dunia kuwasafirisha viongozi hawa. Sisi tuna viongozi wenye mvuto, ushawishi na vitendo vya kweli. Ni lazima tuitumie nafasi hii ili watembee, wahemee ili tuweze kupata *partners*, tuweze kupata wafadhili, tuweze kuendeleza *partnership* na *smart partnership* ili tuweze kuiendeleza nchi yetu. Ni jambo jema na siyo balaa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko swali ambalo liliulizwa kuhusu ziara za Rais wa Zanzibar, lakini, Mheshimiwa Naibu Waziri alilijibu. Ningependa niongeze tu kwamba wala tusiwe na wasiwasi za safari za Rais wa Zanzibar. Rais wa Zanzibar anajulikana

Kimataifa kwa sababu moja ya jukumu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni kuitangaza Zanzibar. Tunaitangaza Zanzibar kwamba ni sehemu ya Muungano na tunaitangaza Zanzibar kwamba ina Mamlaka na ina Uongozi, ina Rais, ina Baraza la Wawakilishi na ni sehemu ya Muungano ambayo imeshamiri demokrasia ya kweli ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Zanzibar anapotakiwa kusafiri kwenda duniani, anapata *protocol* zote zinazotakiwa na Wizara yangu mapema iwezekanavyo inapeleka wadhifa unaompeleka kule nje. Kama anakwenda kwa mfano China, kama Makamu Mwenyekiti wa chama chetu cha Mapinduzi na anapokewa vizuri sana na Jamhuri ya watu wa China ambao wanathamini kwamba chama ndicho kinachoshika hatamu na kina uongozi mkubwa katika mwenendo mzima wa Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatujapata matatizo na ziara za Mheshimiwa Amani Abeid Karume na wale wote waliomtangulia na tunazidi kuimarisha tu zaidi *protocol* ili kuhakikisha kwamba anaposafiri hapati matatizo yoyote yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la Mheshimiwa Felix Kijiko kuhusu Burundi na *PALIPEHUTU*. Tulipata taarifa hivi karibu kwamba baada ya jitihada zote za usuluhishi wa *PALIPEHUTU – FNL* kuondoka Bujumbura na kuingia mitini, tulitoa wito kwa chama hicho kurudi kwenye meza ya mazungumzo ili *PALIPEHUTU – FNL* warudi Burundi, washiriki kuiongoza Burundi ambayo sasa hivi ni ya amani kwa mujibu wa taarifa zote na ushahidi uliopatikana wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoifanya mwezi mmoja karibu na nusu uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali lake lilikuwa wakishakwenda porini, si ndio wakimbizi wanaanza kuja?

Ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Felix Kijiko, kwamba jitihada za Serikali ya Tanzania za bado kutaka kuwaunganisha watu hawa kwa namna ya mazungumzo ili wafikie suluhisho badala ya kwenda kupigana zinaendelea kwa kasi kubwa na ni matumaini yangu kwamba *PALIPEHUTU – FNL* pamoja na Chama cha Burundi kinachotawala watafika tena kwenye mazungumzo ya amani ili kuweza kumaliza tofauti hizi kidogo zilizotokea kwa sababu kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, mwezi uliopita zilikuwa ni kubwa mno na hatutaki kuamini kwamba hawa watu watakuwa wametokomea moja kwa moja. Watarudi kwenye mazungumzo, tutawahitaji warudi kwenye mazungumzo na tunawataka kama wananisikia, warudi kwenye mazungumzo kwa sababu tuna ajenda ya maendeleo na siyo ajenda ya mapigano yanayozidi kuongezeka siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, kuhusu Makampuni ya Madini ambayo yanazuia Watanzania wenyewe kupata nafasi hiyo, hili suala tunaliangalia na nina hakika litapatiwa ufumbuzi na Wizara inayohusika ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna swali limeulizwa kuhusu wanafunzi wetu nje wanasaidiwaje na Balozi zetu? Suala hili pia, Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu,

sayansi na Teknolojia analishughulikia kwa kasi kubwa hasa kuhusu wanafunzi wetu wa Ukraine na Urusi. Sisi katika Wizara yetu tutarekebisha kasoro zote zilizopelekea mtafaruku huu, lakini naamini Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia italimaliza suala hili kwa amani na kwa utulivu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liliulizwa swali na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, kuhusu *argument* kwamba *negotiating configuration* nzuri kwake yeye ingeweza kuwa ni ya Afrika Mashariki kuingia kwenye *EPA*.

Mimi nataka niseme kwamba maelezo ya Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi nayakubali mia moja kwa mia moja kwamba, moja ni kweli tunapozungumzia *EPA – SADC*, inazungumzia tu nchi zile nne ambazo ni Botswana, Namibia, Lesotho na Afrika Kusini ambazo zimeingia kwenye *Customs Union* ambacho ni kigezo kikubwa sasa cha wafanyabiashara wa *European Union* kuingia majadiliano na *Regional Grouping* kama za kwetu. Kwa hiyo, ni *SACCO* tu ya nchi nne iliyo-*qualify,* Angola, Mozambique na Tanzania ni kweli hatuja-*qualify* kwa maana hiyo. Lakini nakubaliana na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, kwamba *effectively* Afrika Mashariki ndiyo inayotakiwa ikubaliwe na *European Union* kuingia kwenye majadiliano haya ya biashara na *investment* kwa sababu tume-*meet* vigezo vyote.

Kwanza, sisi ni nchi tano, tuna soko la watu zaidi ya milioni 100, tuna bidhaa muhimu tunazoweza kusafirisha nje, tumeishafikia *Customs Union* na tuko *Independent* na *Solid* na tumeungana kweli kweli, hakuna sababu kwa nini tusifikie majadiliano na *EPA*. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na kaka yangu Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, kwa muhtasari huo na napenda nimhakikishie kwamba wakati muafaka ukija, Wizara yangu itapanga semina maalumu ya kuelewa haya matatizo na masuala ya *EPA*, tusije tukatukanwa tukanwa bure na watu wengine wanaojitia kujua. Lakini pili, kila tutakapopata nafasi, tutaunganisha zile Kamati za *Foreign* na Kamati za Biashara na Uwekezaji ili ziweze kukutana ili ndugu yangu na kaka yangu Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, uje uweke vitu vyako, waweze kuelewa vizuri ili tuelewe wapi tunachezewa, wapi tunakwenda sawa ili maslahi ya Taifa letu na maslahi ya Afrika Mashariki yaendelee kudumishwa daima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, anasema Bajeti yetu ni ndogo. Tumekubali na tumeielezea. Amezungumzia suala la *gender balance*, nimekupata. Sasa hivi tutajitahidi, tuna Mabalozi wachache, lakini, kama mnavyomjua Mheshimiwa Rais ni shabiki mkubwa wa *gender balance*, mimi pia ni shabiki mdogo wa hiyo *gender balance*, nina hakika tutakuwa tunalirekebisha hili mbele ya safari ili kuhakikisha kwamba wenzetu nao wanatusemea huko nje kama wanavyotusemea wenzetu katika Umoja wa Mataifa, Bara la Afrika, *Washington DC* pamoja na kwenye Ukanda wa Maziwa Makuu. *(Makofi)*

Kuhusu suala la Mbuga za Wanyama wa Kilindi kwamba hazifanyiwi tathmini, Waziri mhusika mwenzangu atakuwa ameshasikia na tutampelekea taarifa hii ili iweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Kuhusu pendekezo la Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kwamba India pale ni vyema tukawa na mtu maalumu atakayeshughulikia masuala ya afya, suala hili ni zito na ni suala muhimu sana. Tayari tumeshalipokea ili tulipeleke kwa wenzetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii waliangalie tuone kama katika utaratibu wetu wa Balozi pale tunaweza tukawa na *Health Attachée* ambaye atashughulikia masuala mazima ya afya ya wazee na vijana wanaokwenda kutibiwa kule India. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, basi nadhani mengi nimeyagusa. Kama nilivyosema…ooh! Lipo moja hapa ambalo inabidi lisemwe sasa hivi kwamba tuwe na *Mwalimu Nyerere Annual Lectures*. Hili nadhani alikuwa amezungumzia Mheshimiwa Susan Lyimo, kwamba *Mwalimu Julius Nyerere Annual Lectures* ni vizuri zikawepo kama zlivyo za Mandela. Ni wazo zuri sana na tunalipokea na tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Kuhusu suala la *Mwalimu Nyerere Foundation* imilikiwe na Serikali, hili inabidi liangaliwe tena kwa umakini kuangalia historia yake, pale ilipofikia, matatizo waliyonayo. Ni suala pia la kuliangalia na tuone kama tutapokea ushauri kutoka kwenye *Foundation* inayohusika kuhusu hilo na wala hatutasita kulitolea ushauri ili kuhakikisha kwamba mambo haya yanakwenda vizuri. Nimebakiwa na dakika ngapi? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kengele bado haijalia!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA.** Mheshimiwa Naibu Spika, basi vizuri. Sasa liko suala la migogoro ya Palestina kwamba Mheshimiwa Balozi wa Palestina alipofika kuzungumza na Kamati, alinung'unika kidogo kuhusu mchango wa Tanzania unavyopungua, tunapozungumzia suala la Palestina, zamani tulikuwa na moto tunaitetea Palestina, lakini sasa hivi tumepunguza kasi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu kama kwamba Tanzania bado inathamini kwamba katika Mashariki ya Kati suala la Palestina halina budi kupatiwa uzito unaostahili. Tunaunga mkono jitihada zote za Umoja wa Mataifa zinazotaka kwanza, kusuluhisha matatizo yaliyopo kati ya Israel na Palestina. Lakini pia tunatambua umuhimu wa Palestina kuwa na Serikali yake na nchi yake yenyewe bila bughudha ya aina yoyote, lakini tofauti na huko miaka ya nyuma. Sasa hivi Tanzania haina adui, ina marafiki na tuna marafiki karibu dunia nzima. Tunaangalia pande zote zainazogombana kama marafiki wetu wa kweli na urafiki huu unaisadia Tanzania kuingia katika mazungumzo ya kuweza kutatua baadhi ya migogoro hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunao uhusiano na Israel mzuri wa kidiplomasia, tunao uhusiano mzuri wa kidiplomasia. Tunaamini kuwa kwa kuwa na uhusiano mzuri wa kidiplomasia na nchi hizi zote hata kama zinagombana, inasaidia kwa kiwango kikubwa kuleta suluhu au kuleta muafaka baina ya hivyo vyombo vinavyogombana. *(Makofi)*

Ningependa nimhakikishie pia kaka yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba Wizara inajitahidi sana kutoa uzito na kipaumbele kwa masuala yote ya usuluhishi ndani na nje. Tuvute subira, mambo haya yatajitokeza vizuri zaidi. Lakini sifa ambayo Tanzania inapata ni hii kwamba Tanzania ni nchi peke yake katika Afrika kama siyo dunia nzima inayoweza kutatua matatizo yake yenyewe bila kumhitaji mtu kutoka nje ya nchi kuja kuleta suluhu ya matatizo yetu na hili ni jambo la kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napata ushauri na Madiwani…na Manaibu wangu! *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mara uko Mtama, mara uko hapa! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maana Madiwani wangu wa Mtama wananisikiliza kwa hiyo,…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, bado dakika tatu!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata ushauri wa Naibu Mawaziri wangu kwamba baada ya kumaliza kuyajibu haya, nitoe tu tena ahadi kwamba vipengele vyote na maswali yote ambayo sikuweza kuyajibu, tutayajibu pengine wakati wa vifungu, lakini mengi zaidi nimesema tutayajibu wakati tutakapokuwa tayari kama Wizara kuyaandika yote na kuleta kitabu cha majibu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda nionyeshe furaha zangu kwa michango mizuri sana ya Waheshimiwa Wabunge waliyoitoa na sasa napenda kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtatambuka kwamba Wizara hii hatuna *Volume IV. Volume IV* ndio ile ye Bajeti ya Maendeleo, Wizara hii haina.

**Fungu 34 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa**

Kifungu 1001 – *Administration and General*... .. ... ... Sh.4, 001,879,600/=

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika *Vote 34, Programme 10, Subvote 1001*.

Kwanza kabisa nimeshukuru sana kusikia kuwa angalau sasa Mjusi wetu anayefahamika kama *Dinosaur* atarudi nyumbani pale watakapomaliza kukubaliana kati ya hizi nchi mbili. Kwa kuwa lilikuwa swali langu la mwaka 2000 na nikajibiwa kuwa hawezi kurudi kwa sababu ni mkubwa mno. Lakini nikaambiwa *cast* yake tunaweza kuipata. Lakini kabla hatujampata Mjusi huyo, nataka kujua Mheshimiwa Waziri anaonaje kuwa kutoka hivi sasa kwa sababu Wajerumani wamefaidika sana na mapato kutokana na Mjusi huyo, je, anaonaje sasa kama tukiwabana mapato wanayoanza kupata kutoka hivi sasa mpaka atakapokuja, tugawane? Ahsante sana!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Janet Kahama, kwa hoja hii ya kuunga mkono mchakato wa kumrejesha Mjusi mkubwa ambaye anashabikiwa sana na yeye na dada yangu Mheshimiwa Fatma Mikidadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mchakato huu utakapoaanza, kutakuwa na timu ya *negotiations*, timu ya mazungumzo baina ya Tanzania, Ujerumani na *UNESCO* na moja ya ajenda itakuwa ni namna gani uwezekano wa *compensation* au fidia inayoweza kulipwa au gharama za kuweza kumsafirisha kwa gharama ambazo nchi inayohusika ya Ujerumani kwa mfano inaweza kuhusika. Kwa ufupi ni kwamba kutakuwa na *negotiating team* yaani timu ya mazungumzo na moja ya ajenda itakuwa ni hiyo ya kuangalia masuala ambayo Mheshimiwa Janet Kahama, ameyatoa. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! Wananichekesha juu ya Mjusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mjusi yule, ile hela tugawane badala ya kurudi.*(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimegundua kwamba huenda Mawaziri hawasomi michango yetu ile tunayopeleka kwa maandishi kwa sababu kuna mambo ambayo ni ya msingi kabisa ambayo nime-*raise*, lakini nitazungumzia mawili na sikuona Waziri ameshituka kabisa juu ya mambo hayo.

La kwanza, nimezugumzia juu ya mali zilizoko nje kwa mfano, hususan majengo na zaidi Maputo. Maputo tumepewa jengo refu kwa heshima na Hayati Samora Machel na hali yake ni mbaya kabisa ukienda pale. Sisi tulikuwa kule mwezi Mei, 2007 unaona huruma kwamba tumepewa hili jengo refu lenye thamani nzuri, lakini hakuna anayeliangalia. Pia tuna kiwanja karibu hapo hapo *(prime area)*, chenye thamani. Hata ile kupeleka pesa kidogo tu kuanza angalau kuonyesha kwamba una-*plan* ya kujenga, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Waziri aeleze Bunge hili, tunaangalia namna gani mali zilizo nje? Siyo hivyo tu, si ajabu kuna sehemu zingine pia zenye matatizo kama hayo. Lakini naona hili kwa Waziri halikuwa jambo la maana, kitu ambacho kusema kweli mimi kimenisikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; tumezungumzia juu ya Chuo chetu cha Diplomasia, Kurasini kwamba tangu mwaka 2003/2004 na jambo hili liko hata kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwamba Chuo hiki hakikaguliwi na anayepeleka mabilioni kule ni Tanzania. Tutawezaje kuendelea kupeleka pesa ambapo hazikaguliwi kwa sababu ya Mfumo wa Sheria kwamba nchi zote lazima zikae, hazikai! Nilifikiri jambo hili pia ni la maana kwa sababu ni fedha za Watanzania zinakwenda pale. Tunahitaji maelezo ni kwa nini Taasisi hii haikaguliwi kama vile inavyopaswa kukagua fedha zingine za Serikali? Kwa kuwa ni mambo mawili ndiyo nimeshauriwa nijikite, lakini nigewashauri Mawaziri wasome yale tunayowaandikia pia badala tu ya kujikita kwa mambo ambayo tunazungumza. Ahsante sana!

**MWENYEKITI:** Wakati mwingine mkipeleka jioni sana, inakuwa vigumu. Ndio maana huwa tunashauri mapema tu mnapojua Wizara kama hutapata nafasi uandike kusudi wapate muda mrefu.

**WAZIRI WA MABO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru umenijibia sehemu ya swali hilo. Lakini ningependa nieleze hivi kwamba ni kweli kabisa kama Mheshimiwa John Cheyo anavyoeleza, jambo hili ni kubwa na linagusa heshima ya nchi yetu. Ni kweli tunayo maeneo ambayo ama hayana majengo mazuri ya Ubalozi na mengine yamechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tumebaini maeneo yote ambayo yana Balozi chakavu ikiwemo Msumbiji na Msumbiji imezungumziwa sana na Geneva na hata London katika makazi ya Balozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubaini yote hayo na timu kutuletea taarifa, Wizara sasa imeingia mkataba na *NSSF*. Shirika hili limeingia mkataba na Wizara yangu baada ya kupata vibali vyote vya Wizara zinazohusika ili kuweza kuanza mchakato wa kuweza kujenga majengo na baadaye kukarabati majengo hayo. Hivi ninavyozungumza, wiki moja iliyopita, tayari tumekwishawekeana mkataba wa ujenzi wa jengo jipya kwenye Ubalozi wetu Nairobi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua itakayofuata itakuwa ni kuelekeza nguvu zetu sasa Msumbiji na sisi wenyewe hatujisikii vizuri na tunapenda kulihakikishia Bunge hili kwamba tunafuatilia majengo yote na tumepeleka timu. Tuvute subira na sisi inatuuma zaidi. Tutarekebisha na mambo yatakuwa mazuri, tunakoenda tuwe tunaenda huku tuko kifua mbele baada ya muda wa kufanyiwa kazi kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Chuo cha Diplomasia na taarifa za ukaguzi, ningependa kutoa majibu mawili hapa, la kwanza, ni kweli kwamba kuna wakati taarifa za ukaguzi hazikuwepo. Lakini ningependa sasa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya Kamati ya Mambo ya Nje kubaini hilo, Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Diplomasia tayari wamekwishakukamilisha taarifa ya ukaguzi na kuifikisha mbele ya Kamati ya Mambo ya Nje. Kwa hiyo, ipo taarifa ya ukaguzi na ningependa kuahidi tena kwamba kuanzia mchakato huu ulipoanza mpaka mwisho wa dunia, hatutaacha kuikagua hiyo na tutapata taarifa za ukaguzi wa Chuo kile wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tena kusema kwamba tunazungumza sasa hivi na Serikali ya Msumbiji kuhusu hatima ya hati miliki ya Chuo kile. Ningependa kutoa taarifa kwamba tumebakiwa na kitu kidogo sana ili kuweza kumaliza tatizo hili ili miliki sasa irudi Tanzania ili tuweze kwenda kwa mujibu wa matakwa ya *propertis* na namna ya ku-*control finances* na kila kitu bila ya kisingizio au kuwa na tatizo ya kuihusisha Serikali ya Msumbiji. Chuo chetu cha Diplomasia ni muhimu sana katika

Kanda na tunawaomba nchi za jirani kama wananisikia walete wanafunzi wao pale ili waweze kusomea masuala mbalimbali ya Kidiplomasia na ya Kidemokrasia. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu fasaha na mazuri. Kitu kimoja tu kidogo, kama Wizara yake inajenga, inakarabati, ni misingi gani ambayo inazuia Wizara hii kuwa na kasma au na *Vote* ya Maendeleo ili hata namna ya kuweza kuangalia mahesabu yake iwe rahisi zaidi kwa sababu sasa hivi inaonekana fedha anatumia kawaida, lakini anafanya shughuli ambazo ni za kimaendeleo. Nipeni maelezo! *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kasma ya Maendeleo *(Development Budget)* ni suala ambalo limetusumbua muda mrefu, lakini liko katika ngazi ya juu ya majadiliano na Serikali. Ninaamini mbele ya safari Wizara zote ikiwemo ya kwangu tutakuwa na *Development Budget*. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo amejibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Ninaamini ni kwa sababu ya muda ameshindwa kujibu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masuala mawili tu ya *clarification*. Nakumbuka wakati nachangia na pia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, akichangia aliuliza sababu ya mapato ya *visa* kupungua katika mwaka huu, lakini sikulisikia. Kwa hiyo, naomba maelezo.

La pili, ni suala zima la *dual nationality* au *citizenship,* nadhani Waziri amelizungumzia vizuri na inaelekea kabisa hata katika yale maswali yake mawili, hayana utata, yana majibu. Lakini katika hiki kitabu chake anaeleza kwamba kupitia upya sheria ya uraia wa Tanzania ili kuona uwezekano wa kuruhusu uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani sasa hivi ni muda muafaka kwamba basi uletwe huo Muswada ili tuweze kupitisha kwa sababu kwa kweli wananchi wengi wanateseka na mimi mwenyewe ni shahidi kwamba nina kaka yangu ambaye amepata matatizo toka mwaka 1976 amekuwa raia wa nchi nyingine. Kwa hiyo, akija hapa Tanzania anakuwa kama *expatriate*. Kwa hiyo, nadhani bado watu hawa wana mchango mkubwa sana katika nchi yao. Kwa hiyo, nadhani hamna utata wowote, hivyo tunaomba Muswada uletwe ili tuweze kupitisha. Mheshimiwa Waziri atuambie tu ni lini anategemea kuuleta?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maneno mazuri, Mheshimiwa Susan Lyimo aliyotoa. Naomba nijibu hoja zake mbili kama ifuatavyo kwamba sababu ya mapato ya *visa* kupungua, moja ya sababu ni huu mchakato tunaosema kwamba upo umuhimu wa kuondoleana *visa* kati ya nchi na nchi. Tutakapokuwa tunaondoa *visa* kati ya nchi na nchi, moja ya sehemu ambayo itaathirika ni mapato. Kwa hiyo, kwa mfano sasa hatuna

tena mapato ya *visa* yale tuliyokuwa tunazoea kupata kutoka kwenye Serikali ya Msumbiji. Pia hatupati tena mapato ya *visa* kutoka kwenye Serikali ya Afrika Kusini. Kwa hiyo, kila tunapo-*sacrifices,* kila tunaposema tuwe na *visa* na nchi zinazotuzunguka ndivyo mapato ya *visa* yatakavyoweza kupungua.

Kuhusu suala la *nationalities* kama Waziri wa Mambo ya Ndani alivyolielezea kwa umakini, tuvute subira ili alipeleke kwenye vyombo vinavyohusika kama alivyotuambia na nina uhakika kabisa tutafikia muafaka mbele ya safari.

*(Kifungu kilichotajwa hapo Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Account* … … … … ... ... ...Sh. 468,143,600/=
Kifungu 1003 – *Foreign Affairs Office Zanzibar* … … …Sh. 164,434,000/=
Kifungu 1004 – *Policy and Planning* … … … … ... ... ... Sh. 515,844,800/=
Kifungu 1005 – *International Cooperation* … … … …Sh. 808,782,200/=
Kifungu 1006 – *Europe and America* … … … … ... ... ... ..Sh. 205,041,100/=
Kifungu 1007 - *Asia and Australia* … … … … ... ... ... ... Sh. 158,975,100/=
Kifungu 1008 – *Africa and Middle East* … … … … ... ..Sh. 8,537,969,800/=
Kifungu 1009 – *Regional Cooperation* … … … …... ... Sh. 2,067,687,200/=
Kifungu 1010 – *Protocol* … … … … .... ... ... ... ... ... ... Sh. 7,617,802,800/=
Kifungu 1011 – *Legal Service* … … … … ... ... ... ... ... ..Sh. 2,103,736,500/=
Kifungu 1012 - *Information, Education and Communication* … ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 107,146,700/=
Kifungu *1013 – Middle East Division* … … … … ... ... ..Sh. 193,970,100/=
Kifungu 2001 - *Embassy of Tanzania – Addis Ababa* …Sh. 797,715,500/=
Kifungu 2002 - *Embassy of Tanzania – Berlin* … … … Sh. 1,256,320,000/=
Kifungu 2003 – *Embassy of Tanzania – Cairo* … … … ...Sh. 549,334,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2004 – *Embassy of Tanzania – Kinshasa* … … Sh. 628,180,200/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote 260400*, nilikuwa naomba kujua hawa wanaofanyakazi katika Ubalozi wakiugua wanatibiwaje maana yake naona pale hakuna *amount* yoyote.

**MWENYEKITI:** *Sub vote* gani?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** *Item 260400, Medical Supplies and Service.*

**MWENYEKITI:** Ni *sub vote 2003* siyo? *Item* gani?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** *260400 Medical Supplies and Services*

**MWENYEKITI:** Ndiyo hakina fedha kwa mwaka huu lazima kitakuwa mahali pengine hebu eleza.

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali hilo la Mheshimiwa Susan Lyimo, ni kweli kwamba pale haionyeshi hela kwa ajili ya matibabu ya watu wale. Lakini matatizo ya matibabu kwa kweli ni kwa Balozi zote na hata vifungu vyote vya fedha zinazotolewa kwa ajili ya matibabu mara nyingi huwa hazitoshelezi. Kwa hiyo, kinachotumika pale inapotokea tatizo kubwa la matibabu taarifa hutolewa Wizarani na Wizara ikishapokea maelezo hayo tunapata fedha, au tunatafuta fedha kutoka hazina na baadaye kuweza kufanikisha matibabu ambayo kwa kweli yanahitajika katika maeneo ambayo mnaona hakuna maelezo yoyote.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2005 – *High Commission of Tanzania – Abuja*.. Sh. 573,837,800/=
Kifungu 2006 – *High Commission*
*of Tanzania – London*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 1,575,508,800/=
Kifungu 2007 – *High Commission*
*of Tanzania – Lusaka* … … ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 656,012,900/=
Kifungu 2008 – *Embassy of Tanzania – Maputo*… … … Sh. 568,284,600/=
Kifungu 2009 – *Embassy of Tanzania – Moscow* … … Sh. 954,765,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2010 - *High Commission*
*of Tanzania – New* Delhi… ... ... ... ... ... ... ... .... ... ... ... Sh. 1,416,556,300/=

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo tu kwenye *item 270100 - Maintenance Physical Infrastructure*.

**MWENYEKITI:** *Sub vote* kwanza.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** *Vote 34, sub vote 2010, item 270,100.* Pale *New Delhi* tunaambiwa tuna kiwanja ambacho tumekuwanacho kwa miaka mingi sana bila kukiendeleza. Sasa ningeomba maelezo je, hizi shilingi milioni 14 kwanza zinatosha ku-*maintain what type of physical infrastructure* na tuna mipango gani ya kuendeleza kile kiwanja tulichokuwa nacho kule? Nashukuru.

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli zimetengwa hizo shilingi milioni 14 kwa ajili ya *infrastructure,* kama nilivyoeleza sasa hivi tuko kwenye mchakato na shirika la *NSSF* ili kuweza kukamilisha na kutujengea majengo katika sehemu mbalimbali za Balozi ikiwemo India hasa kwa upande *residence* kwa sababu ofisi tayari imeshajengwa.

Kwa hiyo, ni katika mchakato huo huo kwamba fedha zinakuwa zinatengwa za kuanzia ili tuweze kukamilisha baadaye mkataba na watu wa *NSSF* kuweza kujenga majengo hayo. Kwa hiyo, hazitatoshi lakini zinatosha kwa sababu tuna watu wanakuja kutusaidia. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2011 – *Permanent Mission to the UN – New York* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 2,876,123,700/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipata nafasi, pamoja na kwamba sikusoma *International Relations* lakini naelewa kwamba katika diplomasia suala *hospitality* ni la muhimu sana. Lakini katika hii *sub vote 2011, sub item 260300* hiki kitengo cha *hospitality* hakijapatiwa fedha. Sasa nilikuwa naomba maelezo kidogo kutoka kwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba katika masuala ya kidiplomasia na *international relations hospitality* ndiyo nguzo moja ya maelewano na upataji taarifa mbalimbali na wema na heshima, kwa hiyo, ni kweli kabisa. *(Makofi)*

Sasa unapoona kwenye kifungu hiki hakina hela kwanza ni kutokana na ufinyu wenyewe wa Bajeti kwamba maeneo ambayo unaweza uka-*scarifices* ni sehemu ya *hospitality*. Lakini hata hivyo siyo kwamba tunakaukiwa sana, hapana, yakitushinda sana tutarudi tena kuja kuomba na tutazungumza na watu wa Hazina pale inapobidi. Lakini ningependa tena kusema kwamba mara nyingi kwenye kituo kama cha *New York* ambacho kinapata wageni mbalimbali kutoka Wizara mbalimbali za Serikali yetu huwa wanakwenda na kitu kinachoweza ku-*take care* masuala ya *hospitality* kwa kutambua kwamba kituo kile pale huwezi ukawa na *hospitality* kwa wingi na wimbi la wageni wanaokwenda kila siku *New York* kikatosheleza. Kwa hiyo, Wizara zenyewe wakati mwingine zinapokwenda pale anakuwa na kiasi fulani cha hela kwa ajili ya *hospitality* ili kuweza kukidhi mahitaji ya kituo kikubwa kama kile.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ni *New York* tu kwingine zipo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Kidogo kidogo.

**MWENYEKITI***:* Kwa hiyo, mkienda pale msipokarimiwa Waheshimiwa Wabunge, muelewe sababu ndiyo hizi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2012 – *High Commission of Tanzania – Ottawa* … … ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 1,270,269,700/=

Kifungu 2013 – *Embassy of Tanzania – Paris* - … … …Sh. 1,432,691,600/=
Kifungu 2014 - *Embassy of Tanzania – Beijing* … … … Sh. 841,729,000/=
Kifungu 2015 – *Embassy of Tanzania Rome* … … … Sh. 1,117,082,100/=
Kifungu 2016 – *Embassy of Tanzania – Stockholm* … Sh. 1,181,476,400/=
Kifungu 2017 – *Embassy of Tanzania – Tokyo* … … … Sh. 1,282,167,000/=
Kifungu 2018 – *Embassy of Tanzania – Washington* … Sh. 1,496,770,000/=
Kifungu 2019 – *Embassy of Tanzania – Brussels* … … Sh. 1,139,332,800/=
Kifungu 2020 *Embassy of Tanzania Permanent Mission to the Un Geneva*… … ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh.1,286,437,500/=
Kifungu 2021- *Embassy of Tanzania- Kampala* … … … Sh. 635,304,500/=
Kifungu 2022 – *Embassy of Tanzania – Harare* … … … Sh. 751,828,500/=
Kifungu 2023 – *Embassy of Tanzania – Nairobi* … … Sh. 1,401,763,200/=
Kifungu 2024 – *Embassy of Tanzania – Riyadh* … … … Sh. 670,069,800/=
Kifungu 2025 – *Embassy of Tanzania – Pretoria*… … … Sh. 903,185,100/=
Kifungu 2026 – *Embassy of Tanzania – Kigali* … … …Sh. 522,605,900/=
Kifungu 2027 – *Embassy of Tanzania -Abu -Dhabi* … Sh. 1,050,436,000/=
Kifungu 2028 – *Embassy of Tanzania – Bujumbura*... … Sh. 633,335,400/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2029 – *Embassy of Tanzania – Muscat* ... ... ... ..Sh. 677,104,800/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, toka tunaendelea nilikuwa napata tatizo katika hiyo *sub vote 2029, sub item 250500 contribution to pension and welfare scheme,* naamini haya ni makato yanayopelekwa kwenye *pension services,* sasa nashangaa kwamba kuna Balozi nyingine wafanyakazi hawa wamekatwa lakini sehemu nyingine hakuna. Je, hatima yao itakuwa ni nini?

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama mtakavyoona kuna maeneo tumeweka kiwango cha *pension* na kiwango kingine hakipo. Lakini labda niseme tu kwamba kutokana na utaratibu wa kila mara maafisa kurejea nyumbani na wengine kwenda nyumbani, tunapata mwanya katika mpango huo wa kuwa na kifungu cha fedha kinachobaki ama kutoka na maafisa kurejeshwa nyumbani na kuweza kukipeleka sehemu zinazotakiwa. Mara nyingi hizi *pension* ni pale pale kwenye Wizara zaidi, Wizara yenyewe mama kwa maeneo yale ambayo tunanyofoanyofoa ndipo tunapoweza kutekeleza suala la *pension*.

Kwa hiyo, fedha ambazo tunaziomba kutoka Hazina na katika mfumo huu wa Bajeti kuwa finyu, maeneo yote ambayo unaona sifuri sifuri Wizara mama ina-*take care* kwa sababu maafisa hao wengine wanakuwa kule kituoni miaka miwili halafu anarudishwa Makao Makuu na pale Makao Makuu tunatafuta hela za kuhakikisha kila ofisa ambaye yupo nje na anarejeshwa na *pensionable.* Kwa hiyo inaji-*sort out.*

**MWENYEKITI:** Kwa nini *uniformity* hakuna?

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna *uniformity* kutokana na idadi ya maafisa wenyewe kwenye *station* na hali ya maisha kwenye *station* hizo. Sehemu kama Japan hali ni ngumu zaidi na kutenga kiasi hicho inakuwa kikubwa zaidi afadhali utengee nyumbani na maeneo mengine hali ya maisha ni nzuri, ni ndogo, kwa hiyo, unaweza uka-*scarifices* ukaondoa kabisa na kuacha maeneo yale ambayo *life style* na hali ya maisha ni magumu zaidi hapo ndiyo tunajaribu kupeleka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2030 – *Embassy of Tanzania – Lilongwe* ... ... ..Sh. 573,110,300/=
Kifungu 2031 – *Embassy of Tanzania – Kuala Lumpur*..Sh. 563,788,200/=
Kifungu 2032 – *Embassy of Tanzania - Brasilia* ... ... ... Sh. 806,650,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Bunge lilirudia*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liyakubali makisio hayo.

**WAZIRI WA USALAMA WA URAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafika. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Nakupa hongera Mheshimiwa Waziri hata kama ni mara yako ya kwanza umejibu vizuri kwa sababu wewe diplomasia yako imebobea katika nafasi hiyo. Kwa hiyo, tunawapongeza wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pana matangazo matatu, kwanza kabisa, shughuli zinazohusiana na *Budget Session* hii tunayo Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

tarehe 7 Agosti, 2007 kesho itatolewa. Kesho kutwa ni sikukuu ya Nanenane hakutakuwa na Bunge.

Halafu tutakuwa na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwekezaji tarehe 9 Agosti, 2007 siku moja. Halafu tutakuwa na Wizara ya Fedha tarehe 10 Agosti, 2007 siku moja lakini pia tutakuwana Muswada wa Matumizi *(Appropriation Bill)* kwa hiyo, zile shughuli rasmi za Bunge kwa maana ya Bajeti hii itakuwa imekamilika. Halafu tutaendelea na shughuli zingine tutakavyopanga Kamati ya Uongozi kesho.

Halafu tunayo matangazo ya misiba. Nafikiri asubuhi tuliezwa kwamba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John Magufuli amefiwa na baba yake. Kwa hiyo, kama kawaida utaratibu wetu utahusika.

Lakini tuna tangazo la pili pia Mheshimiwa Spika, haonekani hapa kuna msiba wa kwake kwamba Marehemu Chifu Abdallah Fundikira amefariki leo mchana.

Mtakumbuka kwamba Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, tulikuwa naye Bunge lililopita na yeye alikuwa Chifu wa Wanyanyembe ndiyo Waziri wa Kwanza wa Sheria katika nchi hii baada ya Uhuru mwaka 1961 na katika mtindo wa zamani ndiyo alikuwa Mjumbe wa *Legco* wa *Western Region.* Lakini yeye alipata *degree* ya kilimo na alikuwa Waziri wa Kwanza lakini alikuwa ana shahada ya kilimo na wakati huo alikuwa ndiyo Afisa Kilimo katika maeneo yake.

Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira tulipokuwa naye hapa bado alikuwa ana nguvu na amefariki katika umri wa miaka 86. Sasa Mheshimiwa Spika, ni mpwa wa marehemu kwa maana ya kwamba mama yake Mheshimiwa Spika, ndiyo kaka yake Marehemu Chifu Abdallah Fundikira.

Kwa hiyo, Spika hatakuwa na sisi kesho ataondoka mchana kwenda Tabora kuzika na mazishi yanategemea kuwa kesho kutwa. Kwa hiyo, kama hamumuoni ana msiba hayo ndiyo maelezo.

Baada ya kusema hayo na mimi pia nichukue nafasi kuwapongeza kwa ajili ya mchezo wa mpira wa Jumamosi maana tulijipamba sana tukaogopa sasa msije mkashindwa ingekuwa aibu kali. Lakini Waheshimiwa Wabunge, wamefanyakazi nzuri sana tumeweza kushinda magoli mawili na kikombe tunacho nadhani mwaka mwingine tutashindania kikombe hicho. *(Makofi)*

Tangazo lingine watu wa *Celtel* wapo katika eneo letu lile wameleta simu ambazo zinaweza kufika hata vijijini mnaweza kujaza fomu pale wanaotaka kukopa, wanaweza kukopeshwa pia, wanaoweza kununua *cash* wanaweza. Kwa hiyo, kuna watu wanatoa fomu pale jengo la utawala. Anayetaka kukopa unajaza fomu halafu mtaelewena huko huko. *(Makofi)*

Sasa baada ya kusema hayo sina matangazo mengine Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.55 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 7 Agosti, 2007 saa tatu asubuhi)*